ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	**-**	**SPIKA**
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi

8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa

		Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni

23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe

31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani

52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando

53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu

54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni

55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae

57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini

59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake

60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole

61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani

62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake

64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani

65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani

66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni

67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde

68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni

70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake

71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi

72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu

73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tatu - Tarehe 9 Februari, 2018

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mezani Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Adhabu, Kutunga Sheria Mpya ya Adhabu, Kuweka Masharti Bora zaidi pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mezani Hutuba ya Maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Adhabu, Kutunga Sheria Mpya ya Adhabu, Kuweka Masharti Bora zaidi pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 24

Utekelezaji Wa Adhabu Ya Kifo

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny. Mhe. Machano Othman Said) - Aliuliza:

Pamoja na kuwepo adhabu ya kifo hapa Zanzibar, kumekuwa na mazoea ya kutokunyongwa watu waliohukumiwa adhabu ya kifo kwa miaka mingi sasa na yapo madai kwamba hata mnyongaji mwenyewe hayupo hali inayoleta mateso na simanzi kwa jamii ambazo jamaa zao wamehukumiwa kunyongwa.

(a) Kwa kuwa adhabu hiyo inaonekana haiwezi kutekelezwa hapa Zanzibar, Je, Serikali haioni kwamba wakati umefika wa kubadilisha adhabu hiyo.

(b) Je, ni mwaka gani wa mwisho adhabu hiyo ilitekelezwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 24 lenye vipengele (a) na **(**b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika**,** ni kweli usiopingika kwamba sheria ya Mwenendo wa Jinai Namba 7/2004 inatambua uwepo wa adhabu ya kifo chini ya kifungu nambari 305 (i) utaratibu wa utekelezaji wake umeelezwa katika kifungu 305-310 vya Sheria hiyo. Pamoja na uwepo wa adhabu hiyo na mazowea ya kutokunyongwa kwa watu waliohukumiwa adhabu ya kifo kwa miaka mingi, haina maana kwamba muda umefika wa kubadilisha adhabu hiyo.

a) Mhe. Spika**,** uwepo wa Sheria ni jambo moja *(theory)* na utekelezaji wa Sheria *(practice)* ni jambo jengine. Hii maana yake ni kwamba kutotekelezwa kwa Sheria

haimaanishi kwamba muda umefika wa kubadilisha adhabu hiyo. Lengo kuu la adhabu ni kuihadharisha jamii kutotenda kosa lenye kufanana au kunasibiana na kosa hilo.

Mhe. Spika**,** kama hiyo haitosha suala la utekelezaji wa adhabu ya kifo ni suala Mtambuka lililogusa sekta mbali mbali. Kwa hiyo, hata utekelezaji wake unahitajika ushirikishwaji wa taasisi na sekta husika. Kwa mfano, mara baada ya Mahakama kutoa adhabu ya kifo, adhabu haitatekelezwa mpaka pale ambapo Mhe. Rais ameridhia kutekelezwa kwa hukumu hiyo.

Mhe. Spika**,** kwa mantiki hiyo, adhabu ya kifo bado ipo kisheria na kwa upande wa Serikali bado haijaona haja ya kurekebisha mtazamo huo hata kama kwa muda mrefu haijatekelezwa.

b) Mhe. Spika, tokea Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya Tarehe 12 Januari, 1964 adhabu ya kifo haijawahi kutekelezwa hii ina maana kuwa hakuna mtu yeyote aliyetiwa hatiani kwa makosa yenye adhabu ya kifo na kutolewa hukumu ya kunyongwa na Mahakama na hukumu hiyo ikatekelezwa nashkuru.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, nchi kadhaa duniani zinatekeleza (baadhi ya nchi sio zote) zinatekeleza adhabu ya kifo kwa makosa mbali mbali, lakini na kwa hapa kwetu Zanzibar tuna adhabu hii ya kifo ambapo ipo

toka mwaka 1964 lakini hadi leo hakuna mtu hata mmoja aliyenyongwa.

Je, hivyo huko tulikotoka 64 mpaka leo hakuna visa vya kuhatarisha nchi yetu na ambao walifika hadi kumuuwa Rais wa Zanzibar wa mwanzo Marehemu Mzee Abeid Amani Karume hatuwa hiyo haikuchukuliwa pana siri gani hapa kwamba hii bora iendelee au ifutwe kwa sababu kiongozi wa nchi kauwawa hatuwa haikuchukuliwa ya kuwauwa wale wahalifu au wahaini. Hivyo hatuoni umefika wakati bora ikafutwa au ikaondoka.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Waziri naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika jawabu yangu mama kwamba pamoja na mambo yote ambayo yanatokezea lakini bado Serikali haijaona umuhimu wa kuondoa adhabu hiyo ya kifo, kwa hivyo tutaendele nayo kuwa nayo hadi hapo ambapo muda utakapofia wakutowa hiyo adhabu ya kifo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama na kufika salama usalimini Mwenyezi Mungu atujaalie turudi majumbani tukiwa salama usalimini, nashukuru kwa majibu yake mazuri.

a) Mhe. Waziri mimi nilikuwa namuuliza Mhe. Waziri nini tofauti ya adhabu ya kifo na kifungo cha maisha.

b) Zanzibar kwa sababu imeshapanga kwamba kuna adhabu ya kifo ilikuwa inataka kutumia *style* gani ya kuuwa au ya kunyonga kwa risasi, kwa kamba au kwa kitu gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake lenye (a) na (b).

a) Mhe. Spika, Mhe. Sarahan alitaka kujuwa tofauti ya adhabu ya kifo na adhabu ya kifungo cha maisha. Mhe. Spika, adhabu ya kifo kama inavyojieleza kwamba adhabu yake mtu huyo atatakiwa afe kwa maana kwamba anyongwe kwa sababu utaratibu wetu ulivyo sasa hivi adhabu ya kifo mtu huyo ananyongwa na kuhakikisha kwamba amenyongeka.

b) Lakini adhabu ya kifungo cha maisha kama kilivyo ni kifungo cha maisha, kwa hivyo unakuweko Gerezani maisha yote yale mpaka pale ambapo pengine Mhe. Rais katika misamaha yake atakayotowa inawezekana ukatoka katika njia kama hiyo lakini hiyo ni tofauti baina ya adhabu ya kifo na adhabu ya kifungo cha maisha lakini tuelewe kwamba inawezekana kwamba ukapewa au mtu akapewa adhabu ya kifo lakini kwa msamaha wa Mhe. Rais anawezekana kwamba adhabu ile ikabadilishwa na ikawa kifungo cha maisha.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kama ifuatavyo:-

Mhe. Waziri nilikuwa nataka kujuwa ni utaratibu gani ambao uanotumika baada ya mtu kuhukumiwa kunyongwa.

Je, akeshahukumiwa tu kunyongwa anapelekewa taarifa Mhe. Rais ili sasa atowe ruhusa anyongwe au mnatumia utaratibu gani ili Mhe. Rais aweze kutia saini. Lakini pamoja na hayo

naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendelea kuibakisha hukumu ya kinyongwa kwa sababu hata Dini yetu inasema kwamba mtu akiuwa na yeye auliwe ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hamza Hassan Juma swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, utaratibu ambao unatumika baada ya mtuhumiwa kutiwa hatiani kwa kifungo cha kifo basi pale Mrajis wa Mahakama anamwandikia Mhe. Rais kwa ajili ya kumpa hiyo taarifa.

b) Lakini vile vile tuelewe kwamba kuna chombo ambacho kinaitwa *Board of Parol*, hiki ni chombo ambacho pia huwa kinatowa ushauri kumpa Mhe. Rais kujuwa kile kinachoendelea katika swali lile. Kwa hivyo huwo ndio utaratibu baadaye Mhe. Rais yeye mwenyewe anachukuwa lile suala na anaangalia na kama ama anaweza kutekeleza basi lina tekelezwa kwa maana kwamba anaona bado kutekelezwa, kwa hivyo inakuwa linakaa vile vile. Kwa hivyo huo ni utaratibu kiufupi ambao unatumika hadi mtuhumiwa huyo au mshtakiwa huyo kufikiya hatuwa hiyo ya kunyongwa.

Mhe. Spika: Ahsante nafasi ya upendeleo ninampa Mnadhimu.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri nina maswali ya (a) na (b).

a) Nilitaka kujua hivi ni sababu gani zilizopelekea kutunga sheria ya hukumu ya kifo ambayo isiyoweza kutekelezeka.

b) Je, hamuoni kutokutekeleza adhabu ya hukumu ya kifo inapelekea watu kutokuhofu kufanya mauaji.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Salum Haji swali lake (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, sheria hii ambayo ndani yake mna hii adhabu ya kifo ni sheria inayotekelezeka kwa sababu kwamba nasema inatekelezeka utaratibu upo wa kwamba (a) (b) (c) ili tufikie hiyo (d). Sasa utaratibu upo umeelezwa kwa maana kwamba Mhe. Rais kutokutowa amri ya kwamba mtu huyu auliwe au anyongwe sio kwa maana kwamba haitekelezeki, yeye ana ridhaa yake mwenyewe na sheria bado ipo na itaendelea kuwepo kwa muda huu. Kwa hivyo Mhe. Rais akiamuwa leo sawa lifanyike hili basi litafanyika, kwa hivyo sheria ipo na inatekelezeka.

b) Lakini kuhusiana kutokuwepo kwa adhabu hii ya kifo si suala la wananchi kuwatoa hofu inawezekana hiyo hofu ikawa katika njia nzuri zaidi kwa sababu mtu tayari anapoona kwamba pana adhabu ya kifo kwa hivyo yeye mwenyewe ataendelea kujizuilia kuyafanya yale makosa. Lakini Mhe. Spika, tuelewe kwamba hii adhabu ya kifo ambayo tunayo ni kwamba makosa yake sio madogo madogo, makosa yake ni makubwa sawa.

Kwa hivyo siamini kwamba adhabu hii inatia hofu kwa maana kwamba wananchi wetu wataogopa, lakini wataweza kuogopa na kujenga hofu kutotenda hayo makosa ili jamii iweze kuishi vizuri.

Nam. 10

Ukosefu Wa Daktari Msaidizi Kituo Cha Afya Konde

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwenye ufunguzi wa Kituo cha Afya Konde aliagiza kuwepo kwa Daktari Msaidizi *"Asisstant Medical Officer",* kutokana na idadi ya watu wanaotumia kituo hicho na hadi leo agizo hilo bado halijafanyiwa kazi. Aidha, hakuna daktari wa meno katika kituo hicho.

(a) Je, ni sababu gani ya kutokuwepo kwa Daktari Msaidizi kama ambavyo Rais alivyoagiza.

(b) Je, ni lini Wizara italeta daktari wa meno katika Kituo cha Afya cha Konde ikizingatiwa kwamba kuna vifaa vya huduma ya afya ya kinywa na meno ambavyo vipo na havina daktari wa kuvitumia.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam 10 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza napenda nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Mwakilishi kwa juhudi zake na kwa kufuatilia hali ya utoaji wa huduma za afya kwa wananchi wanaokitumia Kituo cha Afya cha Konde. Wizara yangu inathamini na kufarajika sana pale anapoona changamoto inayohusu kituo na kushirikiana nasi kwa njia moja au nyengine katika kukipatia ufumbuzi.

Mhe. Spika**,** ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Konde hakina daktari msaidizi *(Assistance Medical Officer)*, hii inatokana na uhaba wa wataalamu hao na wachache tulionao wamepangiwa kufanya kazi katika hospitali badala ya Vituo vya Afya. Hata hivyo, Wizara yangu imempeleka Afisa Tabibu *(Clinical officer)*, katika kituo hivyo ambae kwa mujibu wa muongozo uliopo na mahitaji ya kituo anatosheleza kutoa huduma zinazostahili.

Mhe. Spika, Wizara yangu imelipokea na kulifanyia kazi na kulifanyia kazi agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchukuwa juhudi za kuwasomesha wataalamu wake wa ndani katika vyuo mbali mbali na tunaliahidi Baraza lako Tukufu kwamba mara watakapomaliza masomo yao watapangwa kufanya kazi katika vituo kikiwemo kituo cha Afya cha Konde.

Mhe. Spika, kuhusu kutokuwepo kwa daktari wa meno katika kituo hicho napenda kumthibitishia Mhe. Mwakilishi kwamba tumeshampeleka mtaalamu huyo ambapo kwa uhaba wa wataalamu wa meno tulionao amepangiwa kufanyakazi katika Kituo cha Konde siku mbili kwa wiki (siku ya Jumanne na siku ya Alhamis) tunawaomba wananchi waridhike na hali hii kwanza wakati Wizara tunafanya juhudi za kupata madaktari wa meno wa kudumu na kuwapeleka katika vituo mbali mbali ambavyo vinapaswa kutoa huduma hiyo kikiwemo kituo cha Afya cha Konde. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa sababu ya majibu mazuri na utekelezaji wa Wizara nimefuatilia tena leo nimegundua kweli kwamba daktari wa meno yupo anafanya kazi siku ya Jumanne na siku ya Alhamis,

kwa hiyo mimi ninatowa pongezi kwa Wizara kwa kukubaliana na kutekeleza hilo.

Lakini swali dogo lililopo pamoja na kwamba kwa kituo cha Konde tumepata tayari huyo afisa tabibu ambaye anatosheleza kwa mahitaji inavyosemekana hivyo, lakini tatizo kama hilo bado ninalo kwa kituo changu cha Afya cha Mkia wa Ng'ombe.

Je, Wizara inaniahidi nini juu ya kumpeleka Afisa Tabibu katika Kituo cha Afya cha Mkia wa Ng'ombe ikiaminika kwamba eneo lile limejitenga na kutokana na mazingira ya eneo lenyewe inabidi saa nyengine kufikika kule ni shida na wananchi wetu wanawajibika kusafiri kwa kutoka pale kwenda Makangale. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kwa ruhusa yako nimjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Kituo cha Mkia wa Ng'ombe ni kweli kina tatizo hilo lakini huwa tunamtumia daktari aliyepo katika kituo cha Makangale ambacho ni kituo kipo karibu, karibu ni kilomita mbili (2) kutoka hapo Mkia wa ng'ombe kutowa huduma katika kituwo kile. Lakini hata hivyo napenda nimthibitishie kwamba katika madaktari wataalamu ambao tunawa-*train* hivi sasa basi tumepanga katika kituo cha Mkia wa Ng'ombe pamoja na vituo vyengine ambavyo vina tatizo kama hilo kuwapeleka na kufanyakazi kutoa huduma kwa wananchi.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Lakini kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu fasaha ya swali mama ambalo ameuliza Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Spika, katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri alijibu kwamba kuna uhaba wa wataalamu wa meno, lakini mimi nafsi yangu katika jimbo langu nina vijana wawili ambao wamemaliza *course* hizi za meno. Je, ni lini wizara inaweza kutangaza suala la uajiri wa vijana hawa ambao wana utaalamu wa fani hiyo ambao wanadhurura mitaani. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, daktari wa meno ni daktari mtaalamu na Wizara ya Afya tulisharuhusiwa kuajiri wataalamu bila ya kipingamizi chochote. Kwa hivyo namuomba awape taarifa vijana wake ili wafike wizarani tuanze kuangalia kama kweli ni madaktari wataalamu na wanakidhi mahitaji katika vituo vyetu na hospitali ambazo tunawahitaji ili utaratibu wa kuwaajiri taratibu uanze.(*Makofi*).

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, pamoja na majibu ya kuridhisha kidogo niseme ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, kwanza naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Mhe. Rais makini, shupavu, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuhakikisha suala hili la afya analipa kipaumbele.

(a) Mhe. Naibu Waziri yeye mwenyewe atakumbuka kwamba wananchi wa Birikau wanapata tabu sana kwa kumaliziwa kituo

kile cha afya. Je, wizara yake ina mpango gani wa kuhakikisha kituo kile cha afya Birikau kimemalizika.

(b) Ndagoni kituo cha afya kimefunguliwa huu ni mwaka tena na Mhe. Waziri wa Afya yule pale ndiye aliyefungua kituo kile, hadi leo kituo kile kina daktari mmoja tu na anatoka Vitongoji. Je, wizara yake ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba amepatikana daktari angalau moja mkaazi wa kule Ndagoni kuhakikisha kwamba wananchi wa Ndagoni wanapata huduma wakati wote masaa 24.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kituo cha Ndagoni namuomba Mheshimiwa kama kweli yupo mtu ambaye hajaajiriwa na ana sifa za kuajiriwa kuwa daktari anayeishi katika kijiji cha Ndagoni basi atuletee, ili tuhakikishe kwamba kweli ni mtaalamu tuweze kumuajiri, hatutomuajiri mtu wa mbaye hana utaalamu kwa kutaka watu wenye utaalamu.

Kwa hivyo, tunamuomba kama yupo kweli atuletee ili tuangalie anakidhi vigezo vyetu na utaratibu wa kumuajiri uendelee. Kwa sababu hizo ni nafasi Waheshimiwa ambazo tumeruhusiwa kuziajiri bila ya kipigamizi chochote. Kwa hivyo, wizara kama wizara hatuna sababu ya kuzikalia, lengo letu ni kwamba waajiriwe na watoe huduma kwa wananchi kama zilivyotakiwa.

Mhe. Spika, kuhusu kituo cha Birikau. Kituo hicho nakumbuka mara ya mwisho nilipokitembelea nilitoa ushauri kwa wananchi waliokuwepo pale kwamba katika hatua ile kilivyo si rahisi sisi kuweza kukichukua kwa sababu kwa sasa tuna vituo vya kutosha, angalau wajichangamshe kidogo waongeze hatua *at least* wafikie

linta, lakini kituo wakati nakikagua kilikuwa hakijafikia katika hatua hiyo. Sasa kama kimeshafikia katika hatua hiyo naomba atupe taarifa twende tukaangalie tukiridhika basi utaratibu wa kuwatafutia wafadhili au kukichukua wizara utafanyika. Hatuwezi kuacha nguvu za wananchi zikapotea bura, lakini tunaomba waunge mkono pale walipoanza wafikie katika hatua ambayo inakubalika. Ahsante Mheshimiwa.

Nam. 2

Matumizi ya Jengo la Chuo cha Kiislamu Zanzibar

Mhe. Ussi Yahya Haji - Aliuliza:

Rais wa Kwanza wa Zanzibar Hayati Abeid Amani Karume chini ya Baraza la Mapinduzi aliamua kwamba nyumba iliyokuwa Chuo cha Kiislamu yaani "*Muslim Academy*", iwe nyumba ya kuhifadhia watoto yatima. Vile vile jengo lile ni sehemu ya historia ya Uisilamu hapa Zanzibar.

Je, kwa kuwa Zanzibar ina historia ya Uisilamu, kwa nini serikali isiliweke jengo hilo kuwa kumbusho maalum linaloonesha taarifa, historia na mambo yanayowahusu Mashekh mbali mbali waliokuwepo Zanzibar katika enzi hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 2 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, mara baada ya kuhamishwa watoto katika nyumba ya kulelea watoto Forodhani, tulidhamiri kuanzisha *"Museum of Islamic Scholars"*. Idara ilifanya tafiti mbali mbali na tulifanikiwa

kukusanya taarifa za Mashekhe wetu wakubwa wa enzi hizo pamoja na baadhi ya picha. Kwa hivyo, dhamira hiyo bado ipo ingawa jengo hili haliko mikononi mwetu.

Mhe. Spika, hata hivyo tayari jengo hilo tumeshaliomba kwa ajili ya kulifanyia kuwa Makumbusho ya Historia ya Kiisilamu hapa Zanzibar katika Mwambao wa Afrika ya Mashariki, Zanzibar ikiwa ndiyo kitovu chake. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Ussi Yahya Haji: Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuishukuru serikali kuwa ina dhamira hiyo ya kuweka *Museum of Islamic Scholars* hapa Zanzibar. Lakini nina maswali mawili ya nyonyeza.

a) Jengo hilo kwa sasa ni mali ya nani.

b) Amesema wamefanya utafiti, naomba tu katika utafiti uliofanywa wasije wakasahaulika Mashekhe wa vijijini. Kwa sababu kawaida utafiti huwa unafanywa mijini tu vijijini haufanywi. Kwa mfano, katika Mkoa wa Kaskazini kuna Mashekhe kama Ali bin Juma, Saleh Juma, Shekhe Shauri wa Donge. Je, hawa katika utafiti huo kama hawamo wawemo.

Katika Kaskazini 'A' kuna Mashekhe kama Mwadini Ussi Nahoda na Haji Muhamad na Faki Idi, ikiwa hao hawamo katika utafiti wafikiriwe waingizwe katika utafiti huo. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Ussi Yahya Haji lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

1. Mhe. Spika, jengo hili kwa sasa liko mikononi mwa Mamlaka ya Mji Mkongwe Zanzibar.

2. Mhe. Spika, ushauri wake nimeupokea kwa wale Mashekhe wa shamba ambao ametaka tuwaingize pale ambapo tutaanzisha skuli hii au *Museum* hii. Nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba ushauri wake tumeupokea na tutaendelea kuufanyia kazi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

(a) Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri alikuwa anaelezea maelezo hasa ya kuhamishwa wale watoto yatima na kupelekwa katika nyumba ya Mazizini, nilikuwa nataka kujua ni sababu zipi zilizofanya kuwahamisha wale watoto yatima katika nyumba yao ya asili na kupelekwa katika nyumba ya Mazizini.

(b) Inasemekana serikali iko katika mpango wa kuwahamisha watoto katika nyumba ya mayatima huko Mazizini. Je, nini kauli ya serikali juu ya kuwahamisha watoto hawa na umiliki wa hiyo nyumba waliopelekwa kutoka katika nyumba ya asili inamilikiwa na nani. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake Mhe. Mjumbe lenye kipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, sababu ambazo zimepelekea watoto wale kuhamishwa katika jengo lile la asili kwanza jengo lile lilikuwa haliko katika hali nzuri kwa mazingira ya watoto wetu, lilikuwa limeshaanza athari za kuharibika au ubovu wa jengo.

Lakini pia kwa upande wa kauli ya serikali ni mapema sana kwani jengo hili nina uhakika kwamba dhamira ya serikali ni kuwaweka watoto wetu katika sehemu salama na watoto wetu bado wapo katika sehemu salama. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Mwakilishi ni mapema sana serikali kutoa kauli kwa jengo lile kwani jengo lile bado watoto wetu wapo na bado linamilikiwa na serikali. Ahsante Mhe. Spika,

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa mara nyengine kunipa nafasi nikamuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri katika swali lake la msingi mwanzo kidogo alituchanganya aliposema kwamba lile jengo hawajui liko wapi, lakini baadae akaja akasema liko Mji Mkongwe. Mimi ninavyojua Mhe. Spika, kama alivyouliza swali la msingi Mhe. Ussi Yahya kwamba lile jengo liliwekwa maalumu na kama hidaya ya Mzee Abeid Amani Karume kwa ajili ya kuwahifadhia watoto mayatima. Sasa kwa kuwa utaratibu ule kuwa umeondoka umehamishiwa sehemu nyengine lile jengo tunaambiwa liko Mji Mkongwe, lakini lile jengo sasa hivi linatumika kwa shughuli za hoteli. Je, Mji Mkongwe wameliwekeza katika uwekezaji wa hoteli na wana miradi kama hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Mwakilishi kwamba asichanganyikiwe kutokana na majibu mama ndio usahihi wake ulivyo. Majengo yale yote ya Mji Mkongwe yale majengo wenzetu wa Mamlaka ya Mji Mkongwe ndio ambao wanaoudhibiti kwa sasa.

Lakini Mhe. Spika, kwa biashara ambazo zipo pale tumeona kwamba jengo lile lisikae likiwa vile vile kwa ile sehemu ya chini na wamekodishwa wafanyabiashara na wanaendelea na biashara zao. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 4

Kijiji cha Shamiani, Mwambe Kupatiwa Huduma ya Boti

Mhe. Mussa Foum Mussa - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi kwa kuchukuwa hatua za kuimarisha huduma kwa wananchi wanaoishi katika visiwa vidogo vidogo kwa kuanza ununuzi wa boti maalum, *(Landing Crafts)* kwa ajili ya kutoa usafiri wa uhakika wa kuunganisha visiwa hivyo. Na kwa kuwa boti zimeshaanza kufikishwa katika kisiwa cha Makoongwe na Kisiwa Panza.

Je, ni lini wananchi wa Kisiwa cha Shamiani, Mwambe na wao wataletewa boti hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 4 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli serikali kupitia Wizara yetu ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ina mpango wa kununua boti maalumu *(Landing Crafts*), kwa ajili ya kutoa huduma za usafiri wa uhakika kwa wananchi wanaoishi visiwa vidogo vidogo kwa Unguja na Pemba. Mpango huu umepangwa kutekelezwa kwa awamu.

Kwa awamu ya kwanza, bajeti ya mwaka huu wa fedha 2017/2018, serikali imetenga fedha kiasi cha "TZS Milioni 800,000,000" kwa ununuzi wa boti mbili (2). Mpango huu ni endelevu utaendelea hadi kufikia malengo ya kuwafikishia huduma hii wananchi wote wanaoishi katika visiwa vidogo vidogo vya Unguja na Pemba ikiwemo kisiwa cha Tumbatu, Kojani, Fundo, Makoongwe, Kisiwa Panza na Shamiani - Mwambe. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mhe. Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa serikali imetenga shilingi milioni mia nane kwa awamu ya kwanza kununua boti mbili.

(a) Je, boti hizo zikinunuliwa zinategemewa kupelekwa kisiwa kipi na kipi katika alivyovitaja.

(b) Mhe. Naibu Waziri kwanza nimpongeze kwa juzi tu kufanya ziara ya kwenda kukitembelea Kisiwa cha Shamiani-Mwambe. Je, Mhe. Naibu Waziri alipokwenda aliona kwamba hakuna uwezekano wa kisiwa kile kujenga daraja ili kupunguza masafa na kwa kuwa sehemu ile ni ukanda wa wawekezaji wa hoteli za kitalii. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mussa Foum Mussa maswali yake ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a)Kuhusu ni visiwa gani ambavyo vitaanza kupelekewa hizo boti baada ya kununuliwa, mimi napenda kumwambia kwamba zitakapofika hizi boti tutaangalia mahitaji kwa mujibu wa visiwa

vilivyo. Lakini kwa mujibu wa mpangilio huu tuliyouona hapa basi visiwa ambavyo vitapewa kipaumbele ni Tumbatu na kama nilivyosema na baadae Kojani na tutaendelea katika hali ambapo fedha zitaruhusu. Nina imani kubwa sana na wananchi wa Shamiani-Mwambe nao watakuja kunufaika hapo baadae na mradi huo.

b)Kuhusu ujenzi wa daraja. Niliwahi kulijibu swali hili katika Baraza lako tukufu nilipoulizwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said kwamba kwa hali ya kiuchumi tulivyo hivi sasa hatujakuwa na mpango wa kujenga madaraja bali tumewekeza zaidi katika kununua hizi *land crafts.* Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nakumbuka hivi karibuni Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dkt. Ali Mohamed Shein alikwenda katika kisiwa cha Fundo kwenye ufunguzi wa umeme. Alikuwa na hamu sana au aliagiza kwamba katika maeneo yale ya Fundo na Kokota na maeneo mengine kama yale yaweze kufanyiwa utaratibu maalumu wa kuweza kuweka kama gati ndogo ndogo ambazo zitaweza kuwa na usafiri wa haraka.

(a) Je, wizara naiuliza kwamba ina mpango wa kupeleka boti tu au ina mpango wa kuweka daraja ili wale wananchi wakati wa kuvuka wasiweze kuvuka kwa shida.

(b) Ni visiwa vingapi ambavyo vinahitaji kuwekewa boti na visiwa vingapi ambavyo vinaweza vikaunganishwa ili kuondokana na tatizo hili kabisa kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana, Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua

nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a)Kama nilivyokuwepo na mimi katika ziara hiyo ya Mhe. Rais kule Fundo ni kweli alisema kuna umuhimu wa kuangalia au kufanya utafiti wa namna gani wa kujenga zile gati. Wizara yetu kupitia Shirika la Bandari ipo katika mpango huo wa kufanya utafiti ili kuangalia namna gani tutajenga gati na sio daraja, bali ni gati ili hivi vipando vyetu tutapofika pale vifunge bila ya tatizo lolote kama ilivyokuwa tulipokwenda Fundo na mwenyewe alijionea.

b)Kama nilivyosema visiwa hivi vyote ni muhimu na sisi tumeweka kwa utaratibu maalumu kuhakikisha kwamba, kila kisiwa ambacho kitakuwa kinahitaji *land craft* basi hatua kwa hatua tunawapelekea ili kuhakikisha sasa kunakuwa na usafiri salama kwa wananchi wetu, ili na wao waendelee na shughuli zao za kijamii na kiuchumi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili majibu ya nyongeza.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kuna marekebisho madogo naomba niyafanye ambayo yamekuwa yakijitokeza katika Baraza letu.

Hivi punde Mhe. Suleiman Sarahan Said alipokuwa akiuliza swali la nyongeza alimtaja Rais kama ni Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sio jina halisi, ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi sio Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri yaliyoelekea kutupa faraja katika kutatua changamoto ya visiwa vidogo vidogo, lakini anakubaliana na mimi kama ziko changamoto pia katika hivi visiwa vikubwa vya Unguja na Pemba. Tulikuwa tuna usafiri wetu na inasemekana umeharibika. Sasa ni nini kauli ya serikali katika kutatua changamoto ya hivi visiwa vikubwa hasa kupitia meli yetu ile ya MV. Mapinduzi inasemekana inataka kufanyiwa *overhaule* ni kweli au si kweli.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Spika, kwa ruhusa yako napenda kumuhakikishia kwamba Mhe. Miraji Khamis Mussa serikali itaendelea kuhakikisha kwamba inatatua changamoto za usafiri hatua kwa hatua.

Ndio maana hivi sasa serikali katika bajeti yake ya mwaka huu kupitia wizara yetu tumeanza na ujenzi wa Meli ya Mafuta na baadae tutaendelea na meli nyengine ya abiria na vile vile MV. Mapinduzi ambayo ina hitilafu kidogo kidogo hivi vile vile inasaidia sana katika kuondosha hiyo changamoto anayoisema na nina imani kubwa sana na kuna wawekezaji ambao wanataka kuja kuekeza Zanzibar nao tunawakaribisha kwa ajili ya kuondosha hii changamoto ya usafiri kutoka kisiwa kimoja kwenda chengine hasa vya Unguja na Pemba. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 13

Hatua Madhubuti za Kukarabati Barabara ya Kibonde Mzungu

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Aliuliza**:**

Kwa kawaida kila msimu wa mvua, maeneo ya Kibonde Mzungu panajaa maji kiasi cha kusababisha maafa mbali mbali ikiwemo vifo.

Kwa vile sasa mvua za Vuli zinanyesha na Mamlaka ya Hali ya Hewa inatahadharisha kwamba mvua zitakuwa kubwa.

(a) Je, Wizara mmeshakwenda kuangalia hali ya Kibonde Mzungu ilivyokwisha kuharibika.

(b) Baada ya maharibiko yaliyopita, ukarabati uliofanyika wa kujaza mchanga bila ya kufanya ukarabati madhubuti, si kupoteza fedha za Serikali bure na kuendelea kuhatarisha maisha ya wananchi.

(c) Je, ni lini Serikali itachukua hatua madhubuti kwa kukifanyia ukarabati wa uhakika angalau kipande kile cha Kibonde Mzungu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 13 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli nimekwenda kuangalia hali ya Kibondemzungu ambapo kusema kweli kipindi kile hasa cha mvua ndio ilikuwa hali hatarishi zaidi.

(b) Mhe. Spika, hatua za dharura zilizochukuliwa na wizara yangu ni uwekaji wa mawe makubwa na kifusi kwenye eneo la barabara liliochimbika kwa maji na siyo kujaza mchanga kama alivyosema Mhe. Mjumbe. Lengo lilikuwa ni kunusuru maisha kwa kuimarisha usalama wa watumiaji wa barabara hiyo. Vile vile, hatua ilivyochukuliwa na wizara ilikuwa ni kuepusha kutokea kwa ajali zaidi

kwenye eneo la barabra lililoharibika na si kupoteza fedha za serikali kama anavyodai Mhe. Mjumbe

(c) Serikali ina mpango wa kujenga madaraja na kuinua barabara sehemu ya Kibodnemzungu ili eneo hilo sasa liweze kupitika kwa usalama wakati wote. Kazi hizo zitafanyika mara baada ya kupata fedha kutokana na kwamba matengenezo ya sehemu hiyo yatahitaji fedha nyingi. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza suala la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Je, pesa hizo unatarajia kupata lini ukizingatia mvua zinazotarajia kunyesha baadae zinaweza kuteletea maafa zaidi kuliko yaliyojitokeza.

(b) Mhe. Naibu Waziri katika suala lako ulilotujibu umetwambiwa kwamba njia ile ya Kibondemzungu umetengezwa kwa mawe. Sasa je, wizara yako pale patakapotokezea maafa ya kuharibika tena ile njia kama wizara yako imejipanga vipi kutafuta njia mbadala ambayo haitotumia pesa nyingi ili kuona wakati huo ukifika inawaondeshea usumbufu wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa suala lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Napenda kulieleweshe Baraza lako tukufu kwamba barabara ya sehemu ya Kibondemzungu inatokea kuanzia barabara pale tulipoacha kutengeneza barabara hii Fuoni Polisi mpaka Tunguu ambayo ipo katika mpango. Kwa hiyo, tunaendelea kufanya

jitihada za kuhakikisha tunapata pesa hizo na si pesa kidogo zinatakiwa zaidi ya bilioni ishirini kwa barabara ile na vile vile bilioni nne kwa ajili ya kuinua daraja sehemu ile.

Kwa hiyo, tuendelee na mchakato wakati huo huo tukijua kwamba tunachukuwa hatua za dharura kuhakikisha kwamba barabara basi inapitaka. Sisi tulienda tukaufungua mlango mmoja ule lakini maji yalikuwa mengi na bado tutaendelea kufungua milango yote na kusafisha ili baadae basi sasa ile barabara iweze kupitika na kipindi cha masika kikija basi kusitokee dhara yoyote. Sisi ni lengo letu ni kuhakikisha kwamba barabara zote zinapitika na kuhakikisha kwamba maisha ya wananchi wetu tunawajali. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii nimuulize Mhe. Naibu Waziri suala la nyongeza.

Kwa kuwa hatua za dharura huchukuliwa katika wizara yako katika kuweka vifusi barabara zilizochimbika na ni lini mtaifanyia ukarabati kuitia kifusi barabara ya Chukwani maeneo ya River Tiba baada ya barabara ya Uwanja wa Ndege nyuma kule ambapo walikuwa wanaitumia na kuwaondoshea usumbufu wananchi wale wa Chukwani. Ahsante.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri suala jipya lakini hebu lijibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukuwa nafasi hii kumjibu Mhe. Mwanaasha Khamis Juma suala lake kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli na tumetoa ahadi kwamba barabara ile baada ya kufunga barabara inayoenda Uwanja wa Ndege kwa ajili ya

kuendelea na ujenzi tutaifanyia ukarabati. Kwa vile, tuna vifaa vichache na hivi sasa vifaa vyetu viko Mgonjoni basi nina imani kabisa vikitoka Mgonjoni na Mgelile basi tutakwenda kwa Mhe. Mwanaasha Khamis Juma kumtengenezea barabara yake ile. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, na mimi nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuuliza suala dogo la nyongeza.

Kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake lakini na mimi ningependa kumuuliza suala dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri kama unavyoifahamu barabara ya kutoka Mndo mpaka Miwani-Kiboje, ile barabara maeneo ya Miwani ni sehemu ambayo ina mabonde ya mpunga na ambayo yanajaa maji na mpaka sasa hivi ile barabara baada ya kutiwa fusi tayari imeshakatika kwa mvua ndogo ambazo zimepita hapa karibuni na tunajua kwamba siku za mbele hapo zitakuja mvua kubwa za masika.

Je, unawaambia nini wananchi wa Miwani kuhusu barabara ile kabla ya mvua za masika kuanza matengenezo. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukuwa nafasi hii kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame suala lake kama ifuatavyo:-

Ni kweli juzi tu mimi nilitembelea ile barabara na barabara nyingi za *MIVAP* katika shughuli zangu za kila siku na nimeona imeshaanza kuathirika. Kama ulivyosema kuna sehemu kuna milima na kuna sehemu kuna mabonde, hiyo ni kazi ambayo sisi tunaendelea kufanya endelevu katika wizara yetu na pale ambapo

tutakuwa na uwezo wa kifedha basi na zile sehemu korofi tutazifanyia matengenezo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuniona na kunipa nafasi ya upendeleo na mimi naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Waziri katika daraja lililopo Zawadini ni daraja ambalo linaleta hatarishi kubwa mno wakati wa mvua na tukiwa pamoja mimi na wewe tumeona jinsi gani ambavyo limeleta taharuki kwa wananchi na vile vile hata skuli ikaweza kufungwa kutokana na maji ya mvua yaliopo pale. Lakini pia tuliwaambia pale wananchi kwamba serikali itachukuwa hatua kuona kwamba lile daraja limefanyiwa matengenezo ili ile athari isiweze kujirudia tena.

Je, wizara yako imechukuwa hatua gani kuona kwamba lile daraja limefanyiwa matengenezo. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukuwa nafasi hii kumjibu Mhe. Bahati Khamis Kombo suala lake kama ifuatavyo:-

Ni kweli tulikuwa pamoja mimi na yeye na tukaona ile athari iliyokuwepo pale kiasi ya kwamba tulishindwa kupita pale hadi yale maji yalipopungua. Nia ya serikali kuhakikisha kwamba zile sehemu ambazo zinatuwama maji wakati wa mvua hasa za masika tuziinuwe. Lakini kama nilivyosema mwanzo hii inategemea na uwezo wa kifedha ambapo sisi tuna imani kubwa sana pale hali ambapo itaruhusu hatua kwa hatua kila sehemu ambazo zinahitaji madaraja kuinuliwa basi kuhakikisha tunayainua yale madaraja ili kuhakikisha kwamba wananchi wanavuka kwa salama na amani. Ahsante sana Mhe. Spika.

HOJA ZA SERIKALI

Hotuba ya Mswada wa Kufuta Sheria ya Adhabu Kutunga Sheria mpya ya Adhabu Kuweka Masharti Bora zaidi pamoja na mambo mengine

(Kusomwa Kwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa heshima naomba sasa kuwasilisha mswada huu ambao unakusudiwa kuwasilisha mapendekezo ya Kufutwa Sheria ya Adhabu namba 7 ya mwaka 2004 na kutunga sheria mpya ya adhabu ya mwaka 2018 na kuweka masharti bora zaidi kwa madhumuni ya kuifanya iweze kukidhi mahitaji wa watumiaji katika upatikanaji na utoaji wa haki ndani ya mfumo mzima wa kijamii.

Mhe. Spika, Sheria ya Adhabu ni muhimili mkuu wa haki za raia katika kushughulikia makosa ya jinai. Sheria hii kama zilivyo sheria nyingi za Zanzibar ilipokelewa kutoka India mwaka 1917 yaani una umri wa miaka kama 101 hivi na imekuwa ikifanyiwa marekebisho ili iendane na maendeleo mapya ya kulinda maslahi ya jamii katika matumizi yake.

Mhe. Spika, marekebisho ya kwanza ya sheria hii yalifanywa mwaka 1934 yaliyofuatiwa na marekebisho mengine mnamo mwaka 2004 ambapo sheria hiyo iliandikwa upya. Hata hivyo, marekebisho hayo yote hayakuweza kuondosha kasoro zote zilizomo humu kwani bado sheria imeonekana kuwa na kasoro nyingi na kutoendana na wakati uliopo.

Sheria ya adhabu ya sasa haitambui baadhi ya makosa, baadhi ya vifungu vyake muhimu vimepitwa na wakati na inajumuisha

vifungu vingi ambavyo vimeshafutwa na sheria mbali mbali. Baadhi ya mafungu yaliyokuwepo kwenye sheria ya adhabu ya sasa.

Mhe. Spika, wizara kupitia programu ya mageuzi katika sekta ya sheria ya mwaka 2014/15/18/19 ilifanya mapitio ya Sheria ya Adhabu Namba 7 ya mwaka 2004 na kubaini kasoro tofauti katika sheria hiyo.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri kumradhi kidogo naomba nimpishe Mhe. Naibu Spika ili aje achukuwe nafasi. Mhe. Naibu Spika, karibu. (*Makofi*)

(Hapa Mhe. Naibu Spika alikalia kiti)

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, wizara kupitia programu ya mageuzi katika sekta ya sheria ya mwaka 2014/15 hadi 2018/19 ilifanya mapitio ya Sheria ya Adhabu Namba 7 ya mwaka 2004 na kubaini kasoro tofauti katika sheria hiyo. Baadhi ya sheria hizo ni kama zifuatazo:-

(1) Matumizi ya lugha ngumu ya kisheria
(2) Sheria ya kutokuainisha baadhi ya makosa
(3) Sheria ya kutoendana na wakati
(4) Mpangilio wa sheria mzima kuwa ni wa kizamani
(5) Baadhi ya adhabu kutoendana na makosa husika.

Mhe. Naibu Spika, aidha kuwepo kwa Sheria mpya ya Ushahidi Namba 9 ya mwaka 2016 inayotambua ushahidi wa kielektronic na kukubalika ushahidi wa mtoto ndogo bila ya kuungwa mkono na ushahidi wa mtu mzima, unapelekea baadhi ya sheria kufanyiwa mabadiliko ili kurahisisha utekelezaji wake na kupunguza migongano ya kisheria hizo na sheria ya ushahidi.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali mapendekezo haya ya kufutwa na kutungwa upya kwa Sheria ya Adhabu ni sehemu ya utelezaji wa programu wa mageuzi katika sekta ya sheria kama ilivyoainishwa kwenye mkakati wa tatu wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini Zanzibar. Pia ni utekelezaji wa kifungu cha 7.0 cha Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020.

Kuhusu Zanzibar kuimairisha Utawala Bora na Utawala Bora ya Sheria. Mhe. Naibu Spika, mapendekezo ya sheria hii yataongeza ufanisi katika usimamizi wa masuala ya jinai hapa Zanzibar. Aidha mapendekezo haya yatapelekea kuwa na sheria mpya itakayojumuisha vifungu vipya ambavyo vimekosekana katika sheria ya sasa.

Mapendekezo haya pia yatapelekea kuondosha vifungu vingi vya zamani ambavyo vimeshafutwa na sheri nyengine kuwa ni sheria inayoendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia na inayokubalika na Sheria mpya ya Ushahidi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mapendekezo ya sheria hii yanatarajiwa kuleta faida kadhaa zikiwemo:-

(1) Kuwa na Sheria inayojumuisha makosa mapya ambayo hayakujumuisha katika sheria iliyopo sasa.
(2) Mahakama kutoa adhabu stahiki kwa wahalifu kulingana na uzito wa kosa.
(3) Kuzingatia baadhi ya haki za msingi zinazowajibika kulindwa na baadhi ya waathirika wanaohusika moja kwa moja na Sheria za Jinai.
(4) Kuwa na sheria yenye mpangilio mzuri unaozingatia Kanuni na uandishi wa kisasa ili kurahisha matumizi yake.
(5) Kuondoshwa vifungu ambavyo vimepitwa na wakati.
(6) Kuwa na sheria inayoendana na wakati wa mabadiliko ya sayansi na teknolojia

(7) Kuondosha vifungu ambavyo kwa mazingatio yetu ni vigumu kutumika.
(8) Kupunguza malalamiko ya wananchi kuhusiana na adhabu ndogo zinazotolewa kwa wahalifu na mambo mengine yanayohusiana na adhabu.

Mhe. Naibu Spika, mapendekezo ya sheria hii yataongeza ufanisi katika usimamizi wa masuala ya jinai hapa Zanzibar. Aidha mapendekezo haya yatapelekea kuwa na sheria mpya inayojumuisha vifungu vipya ambavyo vimekosekana katika sheria ya sasa. Mapendekezo haya pia yatapelekea kuondosha vifungu vingi vya zamani ambavyo vimeshafutwa na sheria nyengine kuwa ni sheria inayoendana na mabadiliko ya sayansi ya teknolojia na yanayokubalika na sheria mpya ya ushahidi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mapendekezo ya sheria hii yanatarajiwa kuleta faida kadhaa zikiwemo:-

(1) Kuwa na sheria inayojumuisha makosa mapya ambayo hayakujumuisha katika sheria iliyopo sasa.
(2) Mahakama kutoa adhabu stahiki kwa wahalifu kulingana na uzito wa kosa.
(3) Kuzingatia baadhi ya haki za msingi zinazowajibika kulindwa kwa baadhi ya waathirika wanaohusika moja kwa moja na Sheria za Jinai.
(4) Kuwa na sheria yenye mpangilio mzuri unaozingatia Kanuni za uandishi wa kisasa ili kurahisha matumizi yake.
(5) Kuondoshwa vifungu ambavyo vimepitwa na wakati.
(6) Kuwa na sheria inayoendana na wakati wa mabadiliko ya sayansi na teknolojia.
(7) Kuondoshwa vifungu ambavyo kwa mazingira yetu ni vigumu kutumika.

(8) Kupunguza malalamiko ya wananchi kuhusiana na adhabu ndogo zinazotolewa kwa wahalifu.
(9) Mambo mengine yanayohusiana na adhabu.

Mhe. Naibu Spika, sheria mpya inahusisha mapendekezo mbali mbali baadhi ya mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo:-

(1) Jina la Sheria ya Adhabu ya Mwaka 2018 (2) Kuweka adhabu kwa makosa ambayo hayakuwekewa adhabu katika sheria ya sasa, mfano kosa la mtu kutokutimiza wajibu wake wa kulinda afya na maisha ya mtu.
(3) Kuondoa vifungu vya sheria vilivyofutwa mfano *Approval School Decree cap 59* inayofutwa na Sheria ya Mtoto Namba 6 ya mwaka 2011. Sura ya 41 na Sheria ya Adhabu imefutwa na Sheria namba 1 ya mwaka 2012 yaani *Zanzibar Anti-Corruption and Economic Crimes Act*
(4) Kubadilisha *proviso* kuwa vifungu vipya vinavyojitegemea ili vilete maana halisi.
(5) Maeneo ambayo hayakuwekewa tafsiri katika sheria ya sasa yamewekewa tafsiri mfano mtoto, madhara makubwa, wanandoa na kadhalika.
(6) Kuondoa maneno raia wa Zanzibar na kuweka raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
(7) Kuongeza adhabu ya fidia kwa baadhi ya makosa yakiwemo ya uchapishaji wa taarifa za mwenendo wa kesi zinazohusiana na mahusianao ya ndoa bila ya idhini ya Mahakama.
(8) Kuweka kifungu kinchojumuisha msichana kuwa ni sehemu ya waathirika wa makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu.
(9) Kutambua makosa ya kutekanyara mtoto kwa lengo la kutaka pesa

(10) Kuweka kifungu kinachotambua ujambazi na kutumia silaha.
(11) Kuweka kifungu kinachotambua makosa ya kukutwa na kumiliki silaha bila ya halali.
(12) Kuweka adhabu kwa kulingana na uzito wa makosa husika.
(13) Kufuta Sheria ya sasa ya Adhabu Namba 6 ya mwaka 2004.

Mhe. Naibu Spika, rasimu ya sheria inapendekeza ina sehemu 40 na ina muundo wake kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza: Imeweka masharti ya awali yanayojumuisha jina fupi na kuanza kutumika kubakiza baadhi ya sheria kanuni ya jumla ya tafsiri ya maneno yanayotumika katika mswaada huu.

Sehemu ya Pili: Inahusika na masharti yanayohusiana na eneo la matumizi ya sheria hii ambapo inaeleza ukomo wa mamlaka ya Mahakama katika kushughulikia makosa hayo.

Sehemu ya Tatu: Inahusisha inahusu kanuni za jumla za uwajibikaji wa kijinai inafafanua utetezi unaokubalika katika Sheria ya Jinai.

Sehemu ya Nne: Inahusika na ushiriki katika makosa inaelezea washirika wakuu, washiriki wa pamoja na washiriki wa aina nyengine katika makosa.

Sehemu ya Tano: Inaorodhesha adhabu zinazoweza kutolewa na Mahakama ndani ya Zanzibar.

Sehemu ya Sita: Inahusika na kosa la uhaini na makosa mengine dhidi ya serikali.

Sehemu ya Saba: Inahusu makosa yanayoathiri uhusiano wa nchi za kigeni na utulivu wa nje pia inaanzisha kosa la uharamia na adhabu yake.

Sehemu ya Nane: Imeweka masharti kuhusu mikusanyiko isiyo halali, fujo na makosa mengine dhidi ya utulivu wa jamii pia imeweka masharti yanayokataza jumuiya zisizo halali.

Sehemu ya Tisa: Inahusu makosa yanayohusiana na utoaji wa haki kama vile kutoa ushahidi wa uongo, kusadia kutoa ushahidi wa uongo, kutengeneza ushahidi wa uongo, kula kiapo cha uongo na kudharau Mahakama.

Sehemu ya Kumi: Imeweka masharti kuhusu kuokoa, kutoroka na kuzuia watumishi wa Mahakama.

Sehemu ya Kumi na Moja: Inahusika na makosa mbali mbali dhidi ya mamlaka ya umma kama vile kutoa taarifa za uongo kwa watumishi wa umma, kutokutii jukumu la kisheria na kutokutii amri halali.

Sehemu ya Kumi na Mbili: Imeweka makosa yanayohusiana na Dini ambayo inajumuisha kukashifu Dini yoyote, kufanya fujo kwenye mikusanyiko ya Dini, kuandika au kutoa maneno kwa nia ya kuumiza imani na kukashifu Dini.

Sehemu ya Kumi na Tatu: Inahusu makosa dhidi ya maadili, sehemu hii imeweka masharti ya sheria inayokwenda sambamba na wakati wa sasa kuhusu makosa ya ubakaji, ubakaji wa kikundi, kutorosha, kunajisi watoto wa kiume, kunajisi mtu mwenye ulemavu wa akili, makosa ya kuingilia kinyume na maumbile, usagaji, fumanizi na kuingilia maharimu.

Sehemu ya Kumi na Nne: Imelezea kwa kina makosa yanahusiana na ndoa na mahusiano ya kifamilia, imeweka masharti za kijinai kuhusiana na ndoa za hadaa, kuoa kinyume cha sheria, ukatili wa watoto na kutelekeza watoto au watu wenye ulemavu, pia inapiga marufuku usafirishaji wa binadamu.

Sehemu ya Kumi Tano: Imeweka masharti kuhusu maudhui ya makosa dhidi ya afya na utulivu kama vile maudhi kwa jamii, usafarishaji wa machapisho machafu na makosa dhidi ya sare za kijeshi.

Sehemu ya Kumi na Sita: Inahusika na makosa ya mauaji kama vile kuua kwa makusudi, kuua bila ya kukusudia na kuua kwa mtoto mchanga.

Sehemu ya Kumi na Saba: Inahusu wajibu unaohusiana na kuhifadhi maisha ya afya.

Sehemu ya Kumi na Nane: Inaweka makosa yanayowendana na kuua kwa makusudi na kujiua.

Sehemu ya Kumi Tisa: Inahusika na makosa ya kuhatarisha maisha au afya kama vile kuhataarisha usalama wa vyombo, kujaribu kudhuru kwa kutumia vitu vya mripuko na kumpa mtu sumu makusudi kwa nia ya kumdhuru.

Sehemu ya Ishirini: Inahusika na makosa yanayohusiana na harakati za makundi ya kihalifu.

Sehemu ya Ishirini na Moja: Inaelezea jinai kwa kutojali na kuupuza kama vile kuondoa viungo vya binadamu na kusafirisha watu kwa njia ya maji kwa malipo katika chombo kisicho salama au kilichojaa sana.

Sehemu ya Ishirini na Mbili: Inaweka masharti kuhusu mashambulio kama vile mashambulio ya kawaida, shambulio la kuumiza mwili au aina nyengine ya mashambulio.

Sehemu ya Ishirini na Tatu: Inahusu makosa dhidi ya uhuru wa mtu ikijumuisha kuteka nyara, kutorosha na kazi ushuruti.

Sehemu ya Ishirini na Nne: Inaweka masharti ya kosa la wizi.

Sehemu ya Ishirini na Tano: Inahusu makosa yanayohusiana na wizi kama vile kuua mnyama kwa lengo la kumuiba, wizi wa umeme na kuficha hati.

Sehemu ya Ishirini na Sita: Inahusika na makosa ya unyang'anyi na uporaji kwa nguvu, pia najumuisha unyang'anyi wa kutumia silaha, kutaka mali kwa vitisho vya maandalizi ya shambulio na shambulio kwa nia ya kuiba.

Sehemu ya Ishirini na Saba: Inahusu kuvunja nyumba usiku na kuiba, kuvunja nyumba mchana na kuiba na makosa yanafanana na hayo.

Sehemu ya Ishirini na Nane: Imeweka makosa yanayohusiana na udanganyifu kama vile hadaa, kula njama ya kufanya udanganyifu na kujifanya mtabiri.

Sehemu ya Ishirini na Tisa: Inahusu kupokea ya wizi au mali iliyopatikana bila halali na makosa yanaofanana na hayo.

Sehemu ya Thalathini: Inaweka makosa kuhusu udanganyifu unaofanywa na wadhamini au na watu walio kwenye nafasi ya udhamini na kufanya marejesho wa uongo.

Sehemu ya Thalathini na Moja: Inahusu makosa yakusababisha madhara kwa mali kama vile kuchoma moto, kupeleka mrama vyombo, kuchoma moto mazao na miti, kujaribu kuharibu mali kwa kutumia miripuko na kueneza maradhi ya kuambukiza.

Sehemu ya Thalathini na Mbili: Inahuika na makosa ya kughushi, kutengeneza sarafu, kutengeneza fedha bandia na makosa yanayofanana na hayo.

Sehemu ya Thalathini na Tatu: Imeweka masharti yanahusu makosa yanayohusiana na sarafu na noti kam vile sarafu za bandia, kuwasilisha sarafu bandia na kutoa noti bila ya halali.

Sehemu ya Thalathini na Nne: Inaeleza masharti kuhusu *stamp* bandia.

Sehemu ya Thalathini na Tano: Inahusu makosa yanayoandamana na kompyuta ikijumuisha kuingilia taarifa, kuuingilia mfumo wa kompyuta na kuingilia kati taarifa kinyume na sheria.

Sehemu ya Thalathini na Sita: Inahusika na makosa ya alama bandia za biashara.

Sehemu ya Thalathini na Saba: Imeweka makosa ya kujifananisha kama vile kujifananisha na mtu aliyetajwa kwenye cheti, kuazimisha waraka wa cheti kwa ajili kujifananisha na kukubali dhima kwa uongo.

Sehemu ya Thalathini na Nane: Imeweka masharti kuhusu kujaribu kutenda makosa.

Sehemu ya Thalathini na Tisa: Inaeleza masharti ya makosa ya kula njama.

Sehemu ya Arubaini na ya mwisho inahusu kusaidia baada ya kosa kutendeka.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili rasimu hii ya sheria na hatimae kupitisha ili tupate sheria mpya ya adhabu itakao yosadia kuondoa matatizo yaliyopo katika sheria ya sasa.

Mhe. Naibu Spika, ahsante nakushukuru. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri tunakushkuru sana. Sasa nimwete Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria na Utawala Bora na Idara maalum. Makamo Mwenyekiti karibu.

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis (Mhe. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha hutoba ya maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum, kuhusu Mswada wa Sheria wa kufuta sheria ya adhabu, kutunga sheria mpya ya adhabu, kuweka masharti bora zaidi pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma mwenye kurehemu kwa kutujaalia uhai na afya njema ambayo imetuwezesha kukutana tena katika Baraza hili tukufu, kwa ajili ya kutelekelza matakwa ya Katiba ya nchi yetu kiujumla. Namuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kutubariki pamoja na kutupa neema zake ambazo kwa hakika sote ni wategemezi na wahitaji wake kwa kila jambo.
Mhe. Naibu Spika, pia natoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi, Mhe. Spika pamoja na wenye viti wa baraza hili tukufu kwa namna mnavyoliendesha Baraza kwa umakini na umahiri mkubwa. Namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekma na

busara katika kutekeleza jukumu lenu la kutungooza ili tuweze kutekeleza vyema wajibu wetu katika chombo hichi muhimu kwa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, aidha nitangulize shukrani zangu maalum kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano mkubwa na Ofisi ya Muendesha Mashtaka, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuupitia, kurekebisha na hatimae kuuandika upya Mswaada huu wa Sheria ya kufuta Sheria ya Adhabu, kuweka masharti bora zaidi pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Ili utekelezaji wake uwe rahisi na uwe wenye kuleta ufanisi kwa wasimamiaji wa sheria na haki ya kila mmoja.

Mhe. Naibu Spika, kuletwa kwa Mswada huu kutaweza kupunguza kilio cha muda mrefu kwa watetezi wa haki na wasimamizi wa adhabu katika makosa ya jinai kwa vile changamoto kubwa inaonekana kuendelea kuongezeka kwa makosa ya jinai kutokana na adhabu ziliopo kuwa ndogo na kwa kiasi fulani kushindwa kwenda sambamba na makosa yenyewe katika jamii.

Mhe. Naibu Spika, madhumuni ya Mswada huu ni kukusudia kuanzishwa Sheria ya Adhabu aambayo itaanisha makosa na adhabu pamoja na kuweka mashrti bora yanayohusiana na makosa. Aidha Mswada huu unapendekeza masharti ya sheria ili kwenda sambamba na wakati, unaondoa adhabu, unaondoa masharti yaliyofutwa na sheria nyengine, unarahisha lugha na umetumia namna mpya ya uandishi wa sheria. Vile vile Mswada huu unaainisha masharti ya sheria hii na masharti ya sheria mpya wa mwenendo wa jinai na unakusudia kuleta ufanisi katika usimamizi wa haki, jinai ndani ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, pia napenda nitumie fursa hii kuwashukuru wadau mbali mbali ambao kamati yetu ilikutana nao kwa

mashirikiano yao makubwa ambayo walitupatia na kuweza kutoa maoni yao mbali mbali kwa lengo la kuuboresha Mswada huu. Kamati inawashauri wasichoke kutoa maoni yao pale wanapona inafaa kufanya hivyo, kwani sote tuna lengo la kuitetea jamii na tunapenda kuikinga kuingia katika makosa ya kijinai yenye kuleta matatizo katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Sheria Utawala Bora na Idara Maalum, imeuupitia Mswada huu ukurasa kwa ukurasa kutoka mwanzo hadi mwisho na kuelewa dhana nzima na mantiki ya Mswada huu, ambapo marekebisho mbali mbali yamependekezwa kufanya na kamati kwa kuzingatia umuhimu wa sheria hii katika Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa uwatambue Wajumbe waliounda kamati hii kama ifuatavyo:-

Mhe. Machano Othman Said	Mwenyekiti
Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	Makamu Mwenyekiti
Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf	Mjumbe
Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	Mjumbe
Mhe. Ali Khamis Bakar	Mjumbe
Mhe. Suleiman Makame Ali	Mjumbe
Ndg. Ali Alawy Ali	Katibu
Ndg. Haji Jecha Salim	Katibu

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa uniruhusu nieleze baadhi ya marekebisho mbali mbali ambayo kamati yetu imefanya na pia naomba kuwatanabahisha Waheshimiwa Wajumbe wako wa Baraza lako tukufu ya kwamba, hotuba hii natoa tu ufafanuzi wa baadhi ya vifungu ambavyo vimependekezwa na kufanyiwa marekebisho na kamati. Hivyo maelezo zaidi ya mapendekezo

hayo yamo katika muhtasari wa marekebisho yetu ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari mumeshapatiwa.

Mhe. Naibu Spika, katika sura ya tano ya Mswada huu, kichwa cha habari kinarekebishwa kwa kufuta neno sura na badala yake kuweka neno sehemu. Merekebisho haya yatasaidia kuleta mpangilio mzuri wa sehemu katika sheria hii na kusomeka sehemu katika kila ilipojitokeza neno sura katika kichwa cha habari cha Mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 54 kamati inashauri kiweze kurekebishwa kama ifuatavyo:-

a) Maneno ya pembeni kwa kufuta neno "fujo" na badala yake kuweka neno "ghasia".

b) Kifungu kidogo cha tatu kwa kufuta neno "fujo" na badala yake kuweka neno "ghasia" kila lilipojitokeza katika kifungu hicho. Aidha kamati inapendekeza kufanyika marekebisho neno hilo fujo na kuweka neno ghasia kutokana na ukubwa na upana wa maana ya neno hili na jinsi lilivyozoeleka katika jamii. Hivyo itasaidia jamii kujua athari za mikusanyiko isiyo ya halali ni kosa na inaweza kusababisha makosa mengine dhidi ya utulivu wa jamii.

Mhe. naibu Spika, kamati inashauri katika kifungu cha 115 kifungu kidogo cha pili, kurekebishwa kwa kuongezwa muda wa adhabu badala ya miaka 25 iliyopo iongezwa na kufikia miaka 30.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inapendekeza kifungu cha 116 kinafutwa na kuandikwa upya na kufanya kuwa kifungu kidogo cha 1 na kifungu kidogo cha 2 kama ifuatavyo:-

116 (1) Mtu yeyote ambaye anajua kwamba mwanamke, mwanamme, mtoto wa kike au mtoto wa kiume ana ulemavu wa

akili bila ya halali anamuingilia katika mazingira ambayo hayahesabiki kuwa ni kubaka, lakini mazingira ambayo yatathibitisha kwamba mkosaji alijua wakati wa kutenda kosa kwamba mwanamke huyo, mwanamme, mtoto wake au mtoto wa kiume alikuwa mwenye ulemavu wa akili, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

116 (2) Mtu yeyote ambaye anajua kwamba mwanamke, mwanamme mtoto wa kike au mtoto wa kiume ana ulemavu wa akili bila ya halali anajaribu kumuingilia katika mazingira ambayo hayahesabiki kwamba ni kubaka lakini mazingira ambayo yatathibitisha kwamba mkosaji alijua, wakati wa kutenda kosa kwamba mwanamke huyo mwanamme, mtoto wa kike au mtoto wa kiume, alikuwa ni mwenye ulemavu wa akili atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka thalathini.

Mhe. Naibu Spika, mtoto ni mtoto iwe mwenye ulemavu au asiwe na ulemavu, Kamati inaona sio busara adhabu za anaemfanyia makosa mtoto mwenye ulemavu zitafautishwe na mtoto au mtu asiyekuwa na ulemavu. Na kwa kuwa katika jamii yetu imekuwa suala la kawaida kubakwa kwa watoto au watu wazima wenye ulemavu wa akili, hivyo jamii hii haioni kuwa kufanya kitendo hichi kwa mtu mwenye ulemavu wa akili ni kumuongezea mzigo. Vile vile kuongeza jukumu kwa wazazi na walezi wa watoto au mtu huyo pindipo atapewa ujauzito kumuathiri kimwili au kumsababishia maradhi kwa makusudi kwa vile mja huyu hana uwezo wa kujitetea au kueleza kuwa nani aliyehusika na kutenda kitendo hicho.

Mhe. Naibu Spika, kamati inasisitiza kuwa katika utekelezaji wa sheria hii watu wenye kutenda makosa ya udhalilishaji kama yalivyoainisha katika sehemu ya kumi na tatu, kuanzia kifungu cha 107 hadi kifungu cha 145 ndani ya Mswada huu ambao wapo

kwa lengo la kuwadhalilisha watu wenye ulemavu wa akili, watoto wadogo wa kiume na watoto wadogo wa kike au wengineo wasiojiweza basi ni vyema hukumu yao ikatekelezwa kama ilivyopanga katika Mswada huu wa Sheria baada ya kupitishwa katika Baraza lako Tukufu bila ya kuoneana muhali wala kupeana dhamana ili kuhakikisha janga hili limetoweka katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 119 kamati inashauri kurekebishwa kwa kufuta neno "mitano" na kuweka neno "kumi" mwishoni mwa kifungu hiki. Kamati inatoa ushauri huu wa kuongeza adhabu katika kifungu hichi kutokana na kushamiri kwa vitendo vya kuwanajisi watoto wa kiume kunakosababishwa na jamii kutozingatia thamani ya mtoto katika maendeleo ya ulimwengu na nchi yetu kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, aidha adhabu hii inapaswa pia kuongezwa na kufikia miaka kumi katika mtu aliyetenda kosa kwa kifungu cha 120 kamati inapendekeza kurekebishwa kwa kufuta neno "mitano" na badala yake kuweka neno "kumi" mwishoni mwa kifungu hichi.

Vile vile kamati inashauri jamii kutounga mkono juhudi za watu wenye kuendeleza vitendo vya udhalilishaji kwa kuwatafutuia dhamana au kuficha ushahidi wakati wanapotenda makosa hayo.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 133 (b) Kamati inapendekeza kurekebishwa kwa kufutwa na kuandikwa upya kifungu hichi kama ifuatavyo:-

"(b) Anamuingilia mnyama au anaingiliwa na mnyama au".

Mhe. Naibu Spika, kutokana na jamii kuendelea sana katika masuala ya teknolojia ya habari na mawasiliano, pamoja na kushamiri muingiliano wa watu mbali mbali katika jamii

kumekuwa kwa baadhi ya wanawake wenye kufanya vitendo vya kinyama ambapo wapo hapo awali ikidhaniwa vitendo hivyo ni kwa wavulana tu, lakini sasa mambo yamekuwa tofauti, kwani na wanawake nao hushiriki kufanya kitendo hiki na wanyama, kama inavyosikika kufanyika kwa mambo haya katika nchi zilizoendelea.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 216 (2)(c), Kamati inashauri kurekebishwa kwa kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

(c) "Anamchochea, anamuamrisha, anamsaidia au anamshauri mtu mwengine kujiunga na kundi la kihalifu**,"**

Aidha, mapendekezo hayo yametokana na kuongezeka kwa vikundi viovu na vya kihalifu katika jamii kwa madai kuwa hutokana na ugumu wa maisha. Kamati inashauri kuchukuliwa kwa hatua wale wote walioainishwa katika kifungu hiki ili iwe fundisho kwa vijana na watu wengine wenye kuendeleza makundi haya maovu, yenye kuhatarisha maisha ya wakaazi na wegeni katika nchi yetu yenye fahari ya amani na utulivu.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 221 Kamati inapendekeza kurekebishwa katika maneno ya pembeni, kwa kufuta neno **"**mafindofindo" na badala yake kuweka neno **"**matonsisi". Aidha, kamati inashauri kufuta neno **"**mafindofindo" na badala yake kuweka neno "matonsisi**"** kila lilipojitokeza katika kifungu hiki. Marekebisho hayo ni kutokana na mazoea na namna linavyotumika neno hili ndani ya jamii yetu. Hivyo, katika kulitumuia neno "matonsisi" linatoa maana sahihi na kila mmoja anaelewa maana ya neno hilo katika mazingira tofauti.

Mhe. Naibu Spika, katika mapendekezo ya jumla, kamati inashauri katika Mswada huu kila yalipotumika maneno **"**mtu

yoyote**”** yasomeke **“**mtu yeyote” na lilipotumika neno **“**yeyote**”** kwa kumaanisha kitu, basi litumike neno **“**yoyote**”.** Hii itasaidia kuleta mtiririko mzuri wa matumizi ya sarufi katika lugha yetu ya Kiswahili.

HITIMISHO

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu inaimani kwamba kukamilika kwa Mswada huu na kuweza kupita kwa kuwa Sheria, kutapunguza muendelezo wa makosa mengi na makubwa katika jamii hususan makosa ya udhalilishaji na makosa mengine ya kijinai. Hivyo, wataalamu wa Sheria na wahusika wengine katika utekelezaji wa Sheria hii, wanahitaji umakini na ukomavu wa hali ya juu katika kusimamia na kutoa haki kwa kila mmoja ili kutoa fursa kwa jamii wasielewe kuwa Sheria hii inatekelezwa kwa watu wa hali fulani na wengine haiwahusu.

Mhe. Naibu Spika, ni imani yangu kuwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu wamepata fursa ya kuupitia kwa kina Mswada huu, na kubaini maeneo kadhaa ya kuishauri serikali kuhusu utekelezaji bora wa Sheria inayotarajiwa kutungwa, amabayo itatoa fursa kwa kila mmoja miongoni mwetu kupunguza ongezeko la makosa ya jinai katika mazingira ya nchi yetu, lakini pia na kuwadhibiti watoto wetu kutokana na matendo maovu.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, ni matumaini ya kamati kwamba, Wajumbe wa Baraza hili tukufu, watauchangia, wataujadili ipasavyo na hatimae kuupitisha mswada huu na kuwa sheria ikiwa ni sehemu ya jukumu la Baraza, na hatimae kuipa fursa serikali kutekeleza sehemu ya jukumu lake la utekelezaji.

Mhe. Naibu Spika, Aidha, nachukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa wajumbe wote wa Baraza lako tukufu, kwa umakini wao na usikivu wa hali ya juu waliouonesha wakati wa

uwasilishaji wa hotuba hii. Kamati inawaomba waujadili kwa kina na hatimae kuupitisha kwa ajili ya kuwekewa misingi iliyo bora, katika utekelezaji wake ndani ya jamii ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum tunakushukuru sana. Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuendelea ninachukua fursa hii kuwakaribisha wageni wetu waliohudhuria hapa leo katika Baraza letu, nao naanza na Ndugu Godfrey Kinju. Huyu anatoka Temeke na ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Temeke na ni mgeni wa Naibu Spika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe wageni wetu wengine ambao ni wageni wa Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto Mhe. Maudline Castico, ni vijana wake watano ambao wamefanya vizuri katika mitihani yao ya Kidato cha Pili pamoja na Kidato cha Nne, wapo hapa leo pamoja na mlezi wao ambaye amefuatana nao anaitwa Bi. Saida pamoja na msaidizi wake Mhe. Waziri ambaye anaitwa Maria Obeli. Naomba nyote kwa pamoja msimame. *(Makofi)*

Vile vile nina taarifa ya mgeni mwengine hapa ambaye ni mgeni wa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, lakini naona bado hajafika. Hivyo, atakapofika nitatoa taarifa hiyo. Nawashukuru Waheshimiwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe muda wa majadiliano umefika ninao wachangiaji watano mbele yangu, naamini kwamba na wengine watajitokeza baadae. Lakini sasa nitaanza na Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata). Dakika zetu ni 20 waheshimiwa kwa hiyo nafikiri tutaendelea na dakika hizo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuipata nafasi hii muhimu juu ya kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Adhabu na Kutunga Sheria Mpya ya Adhabu, Kuweka Masharti Bora zaidi pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Waziri yeye na watendaji wake wote kwa kuona kwamba umefika wakati kunusuru vizazi vyetu na hata mambo mengine yanayohusiana na adhabu mbali mbali yanayotokea katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, pia niishukuru Afisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na *DPP* kwa mashirikiano mazuri waliyotupatia katika kuhakikisha kwamba, tunapata tafsiri nzuri juu ya kuchangia mambo mbali mbali yanayohusiana na sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza nitakuwa na mambo ambayo yatahusiana na adhabu. Mhe. Naibu Spika, tunaamini kwamba serikali yetu naipongeza kwa dhati kabisa kwa kuona kwamba umefika wakati wa kutunga sheria ambayo itakwenda na wakati tuliokuwanao. Pia niseme kuwa sheria hii hakutungiwa Shihata wala hakutungiwa fulani kwa kukomolewa, lakini sheria ni sheria sote inatugusa pindi unapokwenda kinyume na utaratibu uliowekwa. Kwa hivyo, nawaomba wananchi wote wa Zanzibar na wageni wanaoingia katika nchi yetu wafuate maadili mema na wajue tu kwamba sheria ikimgusa atakwenda kama ilivyopangwa. Hilo naipongeza sana serikali yetu kwa kuona hili linafaa kwa wakati tuliokwenda nalo.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 308, kifungu cha 109 "Adhabu ya Kubaka". Mhe. Naibu Spika, mimi nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi, tumetembea sehemu kadhaa katika nchi yetu na

bado tulisema tukimaliza Baraza hili tutaendelea na ziara juu ya kadhia hii iliyotokea ya kuharibu watoto wetu katika mitaa mbali mbali na sehemu mbali mbali. Kwa hivyo, tumeyaona mengi na nakuthibitishia Mhe. Naibu Spika, ilifika wakati kila tunapoingia baada ya kupata taarifa na vile vitendo tunavyohakikishiwa kuviona, Wajumbe wangu walikuwa wanalia hata la kuchangia hawana. Kwa hivyo, hii inaonesha dhahiri kwamba hili suala lina kero na kero kubwa na mimi kwa kuwa wizara hii nimeigusa Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto nitagusia sehemu hii zaidi kuliko pengine.

Mhe. Naibu Spika, kifungu hiki cha 109 kinasema "Adhabu ya Kubaka", naomba ninukuu kama ilivyo.

Kifungu cha 109 kinasema kwamba:

"Mtu yeyote ambaye anabaka isipokuwa katika mazingira yanayoelezwa katika kifungu kidogo cha (2) atapewa adhabu ya kifungo cha maisha na katika hali nyengine yoyote atapewa kifungo kisichopungua miaka 30 na faini, zaidi ya adhabu hizo ataamriwa alipe fidia kwa kiwango kinachoamuliwa na Mahakama, kwa mtu ambaye aliyetendewa kosa hilo, kwa madhara ya kimwili au kisaikolojia aliyosababishiwa mtu huyo".

Mhe. Naibu Spika, mimi napongeza kwa dhati kabisa hii adhabu haitoshi ya miaka 30, lakini adhabu ya maisha naipongeza, kwa sababu lazima tukubali kwamba binadamu tumeubwa na akili. Kuna wanyama wakali mbali mbali kama simba, nyati, ndovu. Namwita ndovu kwa maana yake jina jengine tusimwite tunalificha hilo. Kwa hivyo, tuseme huyu ndovu ni mnyama mkubwa wa ajabu, lakini unaweza kumfanya wewe akakufuata unavyotaka kwa kuwa binadamu kaumbwa na akili. Kwa hivyo, ajuwe anapofanya kitendo kiovu chochote anakifanya kwa akili zake.

Kwa hivyo, naomba adhabu hizi ziende na zitekelezwe, namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie tuipitishe kwa uwezo wetu sheria hii na Mhe. Rais kwa uwezo wake na busara zake hatochukua muda. Nampongeza sana Mhe. Rais kwa sababu kilio hiki kila wakati na kila pahala ninapokwenda udhalilishaji, hata sisi viongozi wake wa chini tunapokwenda kufanya mikutano yoyote basi tendo la udhalilishaji lazima tuliseme na kulikemea katika nchi yetu, kwa hivyo hii mimi naipongeza. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 2(a) kimesema kama ifuatavyo:

Kifungu cha 2(a)

"Ikiwa mkosaji kwa mara ya kwanza, ataadhibiwa kwa kupelekwa kwa mwaka mmoja kwenye nyumba ya watoto zilizoidhinishwa au kutumikia jamii,

(b) Ikiwa mkosaji wa mara ya pili atapewa adhabu ya kifungo cha kipindi cha miezi 12,

(c) Ikiwa mkosaji kwa mara ya tatu ni sugu atapewa adhabu kwa mujibu wa kifungu kidogo cha kwanza"

Yaani hapa inaelekeza kwa mtoto aliyekuwa chini ya miaka 18.

Adhabu ya kubaka kwa kundi, Kifungu cha 110.

Kifungu cha 110(1)

"Endapo kosa la kubaka limetendwa na mtu mmoja au zaidi kwa kundi, kila mtu katika kundi hilo aliyesaidia kutenda kosa hilo, basi atachukuliwa kwamba ametenda kosa la kubaka kwa kundi.

Kifungu cha 110(2)

"Mtu ambaye ametiwa hatiani kubaka kwa kundi, atapewa adhabu ya kifungo cha maisha".

Mimi sina haja ya kuongeza jengine, Mheshimiwa naunga mkono na naiomba serikali hili wala tusichelewe, kwa sababu wakati umefika hali imekuwa mbaya na watoto wetu wa kiume na wakike wanaharibiwa bila ya sababu. Kwa hivyo, hii itamgusa mwanamke vile vile na mwengine anayedhalilishwa kutokana na mambo hayo.

Kifungu cha 111(1) "kujaribu kubaka".

"Mtu yeyote ambaye anajaribu kubaka atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka 20".

Kajaribu hakufanikiwa, lakini kajaribu huyo atafungwa miaka 20. Kwa hivyo, nafikiri Mhe. Naibu Spikia, hili halina mjadala pia niipongeze serikali kwa kuliona hili. Mhe. Naibu Spika, ombi langu tu ni kwamba haya yote ili tulikomeshe kabisa katika nchi yetu lisitokee, yatekelezwe mara baada ya kupitishwa sheria hii na kutiwa saini na Mhe. Rais isichelewe, tumechoka katika nchi yetu.

Kifungu cha 111(2)

"Mtu anajaribu kubaka iwapo, kwa nia ya kuwezesha kufanyika kwa ngono haramu na mtoto wa kike au mwanamke anaonesha nia yake kwa:

(a) Kumtishia mtoto wa kike huyo au mwanamke kwa nia ya kufanya ngono;

(b) Akiwa ni mtu mwenye dhamana au ushawishi kwa mtoto wa kike au mwanamke, anatumia kitendo chochote cha kitisho dhidi yake kwa nia ya kufanya ngono;

(c) Anafanya udanganyifu kwa nia ya kupata idhini yake; na

(d) Endapo mtoto wa kike au mwanamke ameolewa, anajifanya kuwa yeye ni mume wa mtoto wa kike au mwanamke, na mtoto wa kike au mwanamke huyo anawekwa katika mazingira ambayo, isipokuwa kwa kutokea kitu kisichotegemea utashi wa mtu huyo, mtoto wa kike au mwanamke bila ridhaa yake angeingiliwa.

Mhe. Naibu Spika, nafikiri hii yote ni hatia na ikifikia kipindi hicho hakuna sababu ya kungojea huyo tena achukuliwe hatua zinazofaa, ili hili liondoke katika nchi yetu.

Kifungu cha 111(3)

"Endapo kosa limefanywa na mtoto wa kiume mwenye umri chini ya miaka 18, atapewa adhabu ya miezi 6 kwa kupelekwa kwenye nyumba ya watoto, skuli zilizoidhinishwa au kuitumikia jamii".

Mhe. Naibu Spika, hii yote ni vyema tukaelezea jamii ili jamii ikatusikia kifungu kwa kifungu itatusaidia. Kila mwenye mtoto wake, Shihata una watoto wako na mwengine ana watoto wake tuwaelimishe watoto wetu, kwa sababu tumepata *rumours* nyingi Mhe. Naibu Spika. Kuna wengine wanatupigia simu wanasema aah! basi Mheshimiwa tukiendelea hivyo hao watoto watamalizika kufungwa, sisi tumelelewa mpaka kufika hapa hatukubaka. Kwa hivyo, hili ni tendo pengine ni la makusudi au limetumwa kama ni kundi maalum la kuhatarisha watoto wetu.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 112 "kutorosha mwanamke"

Kifungu cha 112

"Mtu yeyote mwenye nia ya kumuoa au kumuingilia mwanamke wa umri wowote, au kuwezesha mwanamke kuolewa na kuingiliwa na mtu mwengine yeyote, anamchukua mwanamke huyo au anamzuwia bila ya ridhaa yake atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi miaka saba".

Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiri na hili liangaliwe, lakini pia adhabu hii ni miaka kidogo naomba iongezwe, kutoka miaka saba hadi miaka 10 atajifunza zaidi, kwa sababu huyu atakuwa mzoefu.

Mhe. Naibu Spika, jengine katika kifungu cha 113 "kutorosha watoto wa kike na kiume"

Kifungu cha 113(1)

"Mtu yeyote ambaye, bila ya halali anamchukua;

(a) Mtoto wa kike ambaye hajaolewa kutoka nje ya uangalizi au ulinzi wa baba yake au mama yake au mtu mwengine mwenye dhamana kisheria ya kumtunza au kumhifadhi, na bila ya raidhaa ya baba huyo, mama au mtu mwengine;

(b) Mtoto wa kiume kutoka nje ya uangalizi au ulinzi wa baba yake au mama yake au mtu mwengine mwenye dhamana kisheria ya kumtunza au kumuhifadhi, na bila ya ridhaa ya baba huyo, maa au mtu mwengine, atakuwa ni mkosa, na takapotiwa hatiani atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka 10.

Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiri huyu katorosha, lakini adhabu yake ya miaka 10 sio ndogo lakini kama itaongezwa pia sikatai.

Jengine Mhe. Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba shambulio la aibu katika kifungo cha 114.

Kifungo cha 114(1)

"Mtu yeyote ambaye, bila ya halali na bila ya heshima anamshambulia mwanamke au mtoto wa kike atakuwa ni mkosa, na akitiwa hatiani atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka 18 na atatozwa fidia inayoamuliwa na Mahakama.

Mhe. Naibu Spika, shambulio lolote lile ni baya na shambulio hufanywa kwa makusudi. Kwa hivyo, mimi niseme tu kwamba mheshimiwa na hili naunga mkono liendelee kama lilivyo. Mhe. Naibu Spika, vitendo vingi vinatokea sasa hivi, utasikia katika mawio au taarifa mbali mbali kwamba katika eneo fulani kuna mwanamke kapigwa kwa kukosa kumtilia mumewe kitoweo, wakati mwanamme katoka pale kenda kutafuta maji yake kanywa glasi zake karudi, anauliza kwa nini hakuna kitoweo anampiga tena wengine wajawazito.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, suala hili naomba lifikiriwe sana, kama pataongezwa kidogo pia sio mbaya, lakini naunga mkono kwa asilimia mia moja hili.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 115 "kunajisi mtoto wa kiume"….

Naomba kunukuu “Mtoto yeyote anamuingilia mtoto yeyote wa kiume atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha”.

Mhe. Naibu Spika, hili naliunga mkono na nimefurahi sana kwa sababu watoto wetu wengi wanadhalilishwa na waharibiwa kwa makusudi ndio niliotangulia mwanzo kusema labda kuna mtandao maalum ulioandaaliwa kuharibu watoto wetu. Kwa hivyo ni kwamba kifungo cha maisha itakuwa ni suluhisho la kuondoa kadhia hii.

Halafu jengine Mhe. Naibu Spika, kunajisi watu wenye ulemavu vile vile imewekwa adhabu ya miaka ishirini na hili naliunga mkono.

Mhe. Spika tukiri kwamba wakati wetu huu imani imekwisha kwa sababu watu na akili zao hufanya vitendo kama vya kinyama juu ya kuhatarisha maisha ya watu wetu. Kwa hivyo niseme Mhe. Spika sheria hii ni nzuri na sheria hii inafaa imekuja kwa wakati. Mimi ningewaomba Waheshimiwa Wajumbe ndio tunaokaa vijana wetu mitaani tunapata manun'guniko mengi sana kwa wazee, akinamama na wengineyo juu ya hatari hii iliyokuwepo katika nchini yetu. Kwa hivyo tuiunge mkono serikali kwa kuangalia kwamba panahaja ya kuweka sheria kali ambayo tunapiga kelele siku hadi siku. Mimi naseme tena Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake habari na utalii tumekumbana na mambo mengi, tumekwenda kila mmoja anapofika katika adha inayotokea vilio vinaanguka. Kwa hivyo tuseme haya yote dawa yake sheria hii ikishawekwa na ikifanya kazi, Mwenyezi Mungu atujaalia itaondoka.

Lakini la mwisho niseme Mhe. Naibu Spika, Zanzibar walipoanza vitangi huko nyuma kabisa kulikuwa na taarifa kwenye televisheni anawekwa na bango lake, kitangi yule anaoneshwa hivi na *TV* inamjua kwa sababu akijulikana mmoja au wawili itakuwa ni kama tokeo ambalo litatupa stara sana na usalama sana katika jamii yetu, mwengine ataogopa, lakini ukiambiwa tu fulani kakamatiwa au kambaka mtoto lakini haonyeshi wengine

hawamtambui. Mhe. Naibu Spika, hili tendo tunaambiwa la kuvunja haki za binadamu. Je, yule aliyetenda kosa lile naye sikavunja haki za binadamu. Mimi naomba lirudishwe kwa wahalifu wote hawa kama wanavyooneshwa hawa hawahujumu uchumi, wanaonyeshwa wanaoleta uhalifu mwengine wowote basi na hili litafutiwe rai mhalifu yule akifanya kosa kaonekana na limethibitika, vyombo vya habari vimtoe hadharani ili liwe kama ni fundisho kwa yeye na wengine lisitokee tena katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa vifungu vingi vipo na maeneo mbali mbali mimi ilinikosha sana Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa sababu tunaamini kwamba kadhia tunayoipata ni sehemu tosha ya kuhakikisha kwamba tunaipongeza serikali, tunaipongeza kwa dhati kabisa, tumpongeza Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein, Makamu wa pili wa Rais, Baraza la Mawaziri na wote kwa kuhakikisha umefika wakati kulikomesha tatizo hii lisitokee katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja na nawashauri wenzangu tuuchangie tusiogope, tutoe makali yaliyokuwepo lakini nasema sheria hii ikimalizika tu Mwenyezi Mungu amjaalie Rais wetu akae atulie aipitie, aitie saini ili itumike na kuleta stara kwa jamii yetu na Wazanzibari na watoto wetu.

Naunga mkono hoja. Ahsante. Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali. Sasa Waheshimiwa Wajumbe hapo awali nilitoa taarifa ya ugeni wa Mhe. Waziri wa Wizara ya Utalii nchini Kenya, sasa hivi namona Mheshimiwa yupo hapo. Kwa hivyo nichukue fursa hii kwanza kabisa kumkaribisha sana Mhe. Waziri wa Utalii wa Kenya katika

Baraza letu Tukufu na naomba sasa ukae ili kidogo niweze kutoa taarifa yako. Ahsante karibu sana.(*Makofi*).

Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri Najib Balala leo ni mgeni wa Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo, Mhe. Rashid Ali Juma. Mhe. Najib Balala atakuwa Zanzibar kwa mwaliko wa Sauti ya Busara kushiriki rasmi katika tamasha la busara.

Mhe. Waziri Najib Balala ni Mbunge kutoka katika jimbo la Mvita kwa vipindi viwili sasa. Waziri Najib Balala aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mwambao wa Utalii Mombasa, mwaka 2000–2003 alikuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanya Biashara yaani *Chamber of Commerce*. Mwaka 2003–2004 Waziri wa Michezo Utamaduni na shughuli za kijamii na wizara ya kazi, mwaka 2005 – Waziri anaeshughulikia urithi wa Kitaifa, nafikiri mnafahamu nini urithi wa Kitaifa na sisi tunao Mji Mkongwe na mambo mengi mengi tunayo hapa Zanzibar, katika 2011 -2012 Mwenyekiti wa umoja wa mataifa wa kamati tendaji ya kusimamia utalii.

Mhe. Waziri Najib Balala tunakukaribisha sana na tuna furaha na tunafaraja kuwa nawe leo hapa na tunatarajia sana utakuwa mtulivu kabisa katika kutembelea maeneo yetu hapa ya Zanzibar na utafurahi sana. Karibu sana Mhe. Najib Balala.(*Makofi*).

Waheshimiwe Wajumbe naomba nirekebishe ile kauli yangu ya muda wa kuchangia kwa kuwa Kanuni zetu zinatwambia kwamba kwa mikutano ya kawaida Kanuni ya 58(6) mikutano ya kawaida tutuaifanya, uchangiaji utakuwa ni dakika 15 tu.

Kwa hivyo naomba sana Waheshimiwa Wajumbe wajipange katika hizo dakika 15. Lakini jengine ni kwamba wachangiaji wameshaanza kuongezeka, kwa hivyo ningeomba sana watu wajali muda. Sasa baada ya kusema hayo naomba sasa

nimkaribishe Mhe. Zulfa Mmaka Omar, baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Shehe Hamad Mattar na Mhe. Asha Abdalla Mussa.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika Mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako kwanza naomba nianze kutoa pongezi za dhati kwa Kamanda wa Mkoa wa Kusini Pemba kwa mujibu wa kazi zake ambazo anazozifanya kupinga udhalilishaji pamoja na kusimamia masuala mazima ya madawa ya kulevya.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Kamanda wetu wa Mkoa wa Kusini Pemba sasa hivi kasimamia kinaga ubaga juu ya masuala ya madawa ya kulevya na tuona jitihada zake zimetoa matunda katika Mkoa wetu, niseme tu tokea nizaliwe sijasikia kesi za madawa zinafuatiliwa na watu ambao wanauza madawa kulevya wanakamatwa majumbani kwao au katika vigenge vyao na kesi zile kuzifuatilia kwa muda wa miezi sita na kutolewa adhabu, Lakini ni mezi sita tu Mhe. Naibu Spika, nimeona kwamba kuna kesi sita Mahakamani zimeweza kufuatiliwa akijumuika yeye na kikosi chake wamekamata watu ambao wanahusika na madawa ya kulevya ambao ni *chronic* na kufikishwa Mahakamani na kupewa adhabu.

Napenda kumshukuru sana na nimuombe aendelee hivyo hivyo Mwenyezi Mungu yuko pamoja na yeye. Ninaamini kwamba kwa ujira wake huu Mwenyezi Mungu atamlipa yale mema kwa kitendo hiki kibaya ambacho anachokipiga vita.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze katika kifungu cha 108. Mhe. Naibu Spika, hapa pametajwa makosa ambayo hayatopatiwa adhabu. Lakini nilikuwa naomba tu katika kifungu hiki cha 109(2)

adhabu yake kimeonesha umri wa miaka 18 au miaka 17 ambaye amebaka tumeona adhabu yake haiko mbaya kwa sababu akili zake bado hazijatengamaa, zipo kwamba mwaka mmoja, miaka miwili na miaka mitatu. Ila ningeomba hapa kiongezwe kitu kimoja kwa sababu wale wa miaka 17 au 18 ambao wanafanya makosa haya kama mwanamme ana miaka 17, mwanamke ana miaka 16 basi ni vyema ilikuwa izingatiwe umri wao.

Ni vyema tuangalie suala zima la kupewa dhamana kwa sababu huyu kijana ambaye wa miaka 17 kama atafanya kitendo hichi na wa miaka 16 mara nyingi inakuwa ni makubaliano yao wenyewe. Nilikuwa naomba sana kama kuna uwezekano kijana huyu apatiwe dhamana kwa sababu kijana huyu inakuwa bado yumo katika masomo na pia yuko katika umri mdogo. Kuna wale ambao wanafanya matendo haya wa miaka 35 kwa kuwafanyia wa miaka mitano, hawa hawastahiki hasa kupewa hii dhamana na mimi nilikuwa naomba kwamba adhabu yako iwe ni maisha sio miaka 30.

Mhe. Naibu Spika, miaka 30 kama tunawafanyia masihara watu hawa. Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana katika suala hili liangaliwe huu umri kwa sababu tunajua kwamba miaka 17 ni mwanafunzi ambaye yuko skuli na mara nyingi sana anakuwa bado anachokitenda hakifahamu kwa miaka 17. Lakini akitenda kwa mitatu basi adhabu hii anatakiwa na yeye basi aitumie.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende katika kifungu 151. Mhe. Naibu Spika, hapa tumeona kwamba Jaji Mkuu kapewa ruhusa ya kutoa dhamana pale ambapo inastahiki. Mhe. Naibu Spika, hapa mimi sina pingamizi napo ila nilikuwa namuomba Jaji Mkuu, hii dhamana ni nzito, hii dhamana ina lawama, na sisi tumemuamini sana na tunamjali sana na tunajali heshima yake. Tulikuwa tunamuomba sana asikubali kishawishi chochote wala asikubali rushwa yoyote juu ya dhamana hizi ambazo sisi tumempa

dhamana ya kutoa dhamana hii. Kwa hivyo, tunamuomba sana Mhe. Jaji Mkuu na tunamuamini asije kufanya makosa juu ya uaminifu wake ambao tunamuamini sisi sote Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, niende sehemu ya 35 kifungu cha 365(a), (b), (c) na (d) "mamlaka ya Mahakama katika kusimamia makosa ya mitandao. Mhe. Naibu Spika, hapa tunaona kwamba kuna kosa la usambazaji wa picha za ngono kupitia kompyuta. Mhe. Naibu Spika, hili suala athari zake ni kubwa tunaona kwamba sasa hivi watoto wetu wengi sana wamejiingiza katika hii mitandao kwa ajili ya kuangalia picha hizi ambazo hazina maana na zinawaletea athari kiupande wake.

Pia hapo hapo tunakuta kwamba kuna masuala mazima ya ku-*edit* picha katika kompyuta. Mhe. Naibu Spika, kesi hizi ni nyingi sana lakini hatma yake tunaiona kwamba hazifuatiliwi au haziendi moja kwa moja na zile adhabu ambazo wanapewa haziridhishi. Nikiangalia katika Mswada huu Mhe. Naibu Spika, suala sikuliona. Kwa hivyo, nilikuwa naomba kwamba kuna watoto pia ambao wanabakwa, unakuta kwamba mtu anambaka mtoto baadae anamchukua *video*, *video* zile zinasambazwa katika kompyuta. Lakini sasa tukiangalia katika Mswada ndani suala hili halikushughulikiwa, kosa hili halipo.

Kwa hivyo nilikuwa naomba sana kosa hili kwa imani yako ilikuwa nalo lizungumziwe ili kuwekwa adhabu yake ambayo itastahiki. Kwa sababu tukiangalia kwamba sasa hivi tunaona kwamba kompyuta nyingi utamkuta mtu kwamba kafanyiwa *editing k*atika picha, pengine mtu maskini kavaa vizuri tu, lakini unaweza kumu–*edit* yuko vibaya na kosa lake linaweza kuleta athari kwa yule ambaye kafanyiwa *editing*. Lakini makosa yakienda Polisi au Mahakamani Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hayaridhishi hukumu zake, hivyo katika sura hii yanahusiana na kompyuta ni vyema kuorodheshwa.

Mhe. Naibu Spika, pia nizungumzie suala la simu. Mheshimiwa sasa hivi tunakuta kwamba makosa mengi sana yanatendeka katika simu kuna *message* za matusi, kuna *video* zisizofaa sasa hivi watu wanatuma. Lakini katika Mswada huu Mhe. Naibu Spika, sikuona suala ambalo linahusiana na mtandao wa simu. Kwa hivyo nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri mfanye masuala kidogo na hili suala hili nalo ni vyema kuingizwa katika Mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka nizungumzie juu ya jamii. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli masuala ya udhalilishaji sasa hivi yamezidi. Lakini sasa na sisi jamii nilikuwa naomba sana tubadilike kwa sababu hata kama zitawekwa hizi adhabu za miaka 30 au mwaka mmoja kama jamii hatutotaka kubadilika hili suala halitoweza kumalizika. Sasa hivi jamii yetu tumekuwa hatuna imani, tumekuwa hatuna umoja, unamkuta mtoto wa mwenzako anafanya makosa unamuangalia tu unasema mwache afanye. Suala hili wengine tunalishirikisha kwenye siasa unaweza kusema aah! yule si mtoto wa fulani, fulani si ana chama fulani.

Mhe. Naibu Spika, hii haifai, sisi jamii tunatakiwa tubadilike mtoto wa mwenzako ni wako ukimuona kwamba mtoto leo amefanya kosa unatakiwa umkemee, sio leo kafanya kosa wewe unamuona unanyamaza kimya. Unamuona kwamba fulani anamtendea kosa mtoto wa fulani unaridhika unasema basi tu afanye, itakuwa si vizuri hata kwa Mwenyezi Mungu naamini hayupo radhi juu ya suala hili ambalo tunalifanya.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, tunaona kwamba zamani watu wanashirikiana katika malezi kesi hizi zilikuwa hamna nyingi sana, lakini sasa hivi sijui niseme kwamba utandawazi au ni kitu gani, au niseme kwamba imani zetu zimekwisha katika nafsi zetu. Masuala haya unamkuta hasa yule pale mtoto anaingia katika nyumba ya mtu

fulani na yule hana uhusiano nae wowote na unajua kwamba ana uhusiano nae wa kimapenzi, kwa nini usipige vita, kwa nini usiende kusema, lakini mwisho wake unasema aah! Namuacha bwana mama yake si yuko pahala fulani, mama yake hivi. Mhe. Naibu Spika, hapo malezi hayaendi na hapo imani haitokwenda hata tuseme kwamba watu wafungwe miaka mia mtu tuseme atafungwa maisha.

Mhe. Naibu Spika, nahisi kwamba kufungwa hii adhabu tushaibadilisha lakini hii haitasaidia kumalizika masuala ya udhalilishaji. Tunachotakiwa sisi jamii tubadilike tuwe na imani, wewe mmoja useme kwamba mimi simlei mtoto wa fulalni kwa sababu za kisiasa au kwa sababu nyengine zozote, yeye mama yake tajiri, yeye mama yake hivi, unapomlea mtoto wa mwenzako naamini kwamba na wewe wako pia atalelewa. Kwa hivyo, niiombe sana jamii tuwe na imani tushirikiane katika malezi lakini tukisema kwamba aah! mtoto tu tunamuacha mimi naamini kwamba haitoleta picha nzuri.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba nizungumzie kifungu hicho hicho cha 151(4) kiwango cha madawa ya kulevya. Mhe. Naibu Spika, hapa pametajwa kiwango cha madawa ya kulevya ambacho watu wanapewa adhabu. Hapa kasema kwamba ni kiwango kidogo lakini niseme kwa Mhe. Waziri hichi kiwango kidogo hatukifahamu ni kipi hasa kwamba hofu yetu isije kusema kwamba hichi kidogo watu wakaja kuchanganya hapa ikiwa mtu akaja kukamatwa na madawa tukasikia nje kakamatwa kaachiwa kwa sababu kiwango ni kidogo. Kwa hivyo, tulikuwa tunakuomba sana Mhe. Waziri utakapokuja katika majumuisho utueleze hichi kwango kidogo ni kiwango gani. Isije ikawa kwamba ni bangi kilo kumi tukaambiwa kwamba ni kidogo ni bora kwamba utueleze ni kiwango gani tukikubali ama tukikatae.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende katika ufafanuzi wa maneno, kuna neno pale limetajwa “kilema”. Mhe. Naibu Spika, zamani suala hili lilikuwa likitumika lakini sasa hivi nahisi kwamba kutaja neno kilema ni makosa kidogo. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hili neno lifutwe na badala yake iandikwe “ulemavu”, nahisi kwamba italeta sura nzuri.

Mhe. Naibu Spika, nikimaliza hapo naiomba sana serikali na tunaona jitihada zinazochukuliwa ni kubwa sana katika Mahakama zetu, lakini kuna baadhi ya makosa ambayo hata sisi jamii tunayafanya pia nilikuwa naomba nayo tutoe elimu juu ya jamii. Tunakuta kwamba kuna makosa ambayo wanafunzi wamebebeshana mimba, kesi zile zinakwenda mpaka polisi mwisho wa siku wazee wale wanakataa kesi zile na kuamua kuzimaliza nyumbani.

Mhe. Naibu Spika, hii si haki, kwa hivyo nilikuwa naomba sana serikali izidi kutoa elimu juu ya suala hili kwa sababu mtoto yule unapoamua kumalizana nae nyumbani kusema kwamba aolewe unamnyima haki zake za kimsingi. Lakini sasa suala ambalo sasa hivi hasa ikipita sheria hii naamini kwamba kuna kesi nyingi sana zitatolewa hukumu majumbani ya kuozeshana na hili ni kosa kwa sababu kama tungelikuwa hatuogopi kuingia katika Dini, ningelisema kwamba tutunge sheria kwamba si ruhusa mtoto wa miaka kumi na nane kuolewa, lakini tukiangalia kwenye Dini anatakiwa kwamba mtoto akifika umri wa miaka kumi na moja anaruhusiwa kuolewa. Kwa hivyo, mimi nilikuwa naomba tu hili sawa, lakini sasa tuweke ile sheria kwamba kumuoa mwanafunzi ni kosa, tukiweka kwamba kumuoa mwanafunzi ni kosa naamini kwamba hatutoingia katika Dini lakini tutakwenda kijamii.

Mhe. Naibu Spika, wale ambao wanaoa wanafunzi wanatakiwa kupewa adhabu kali na pia wanatakiwa kunyimwa dhamana na pia hiyo miaka thelathini kuhusiana na wao, kutokana na hayo

Mhe. Naibu Spika, mimi naomuomba sana Mhe. Rais, atie saini ili sheria hii ianze kutumika, pia kama kuna uwezekano namuomba siku ile ya utiaji wa saini basi Mhe. Waziri awaalike wana UWAWAZA nao wende wakashughudie ijapokuwa kidogo ule utiaji wa saini ili tuweze kufurahi na sisi kutokana na maombi ambao tuliyokuwa tunayataka kila siku Mhe. Rais atuletee katika Baraza hili na leo katuletea.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Zulfa Mmaka Omar. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Shehe Hamad Mattar na ajitayarishe Mhe. Asha Abdalla Mussa na baadae atafuata Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Shehe Hamad Matar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nami kunipa fursa hii kuweza kutoa mchango wangu katika Mswada ulioko mbele yetu. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu namuomba aniwezeshe niweze kuwasilisha mchango wangu kwa ufasaha kabisa.

Mhe. Naibu Spika, kwanza katika mchango wangu niipongeze serikali kwa kupitia Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria,Utumishi wa Umma, na Utawala Bora na Idara Maalum pamoja na taasisi zote ambazo zilishiriki na wahusika wengine kwa jina jingine wanaitwa wadau ambao walikaa pamoja na kuona kwamba kuna haja sheria zetu hizi za Zanzibar kuzifanyia marekebisho. Kwa yale ambayo tumeona hayakuwepo na kuanza kuwepo katika serikali yetu na nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa kawaida mwanadamu yeyote ni mwenye mapungufu, na ndio maana tukawa tunakosoana, lakini niseme katika Miswada mingi inayokuja hapa tunafanya makosa ambayo

ukitizama yanaweza kuepukika. Kwa hivyo, katika Mswada huu na ukizingatia marekebisho ya wenzetu wa Kamati waliopitia Mswada huu marekebisho yamekuwa ni mengi madogo madogo ambayo tungeweza kuyaepuka bila kurudia tena masuala kama hayo tukaangalia mambo mengine. Kwa hivyo, ushauri wangu kwanza kabla ya haujawasilishwa Mswada huu mbele yetu, baada ya kuuandaa wahusika basi waupitie vyema, kama wanaona ni mkubwa kama huu basi wagawane hata kwa vikundi kila mtu apewe sehemu yake aweze kuupitia sarufi iliyotumika, maneno yaliyotumika ni sahihi na pahali ndipo ili ukifika hapa tuangalie kubadilisha vifungu au kurekebisha vifungu na siyo maneno "wa, ke, nyengine, vyengine, kama hayo na mengineyo".

Mhe. Naibu Spika, sasa niende moja kwa moja katika mchango wangu katika kifungu sehemu ya 16 ya Mswada huu kifungu 137, naomba niruhusu niinukuu.

Kifungu namba 137 kinasema kwamba:

> "Endapo mwanamke au mtoto wa kike kwa kitendo chochote kwa makusudi au kwa kuacha kutenda kwa makusudi akasababisha kifo cha mtoto wake akiwa chini ya umri wa miezi kumi na mbili lakini wakati wa kitendo hicho, au kuacha kutenda huko mezania ya akili yake ilikuwa inasumbuliwa kwa sababu hakuwa amepona sawa sawa kutokana na athari ya kumzaa mtoto huyo au kwa sababu ya athari ya kunyonyesha baada ya baada ya kumzaa mtoto huyo, pia bila ya kujali kwamba mazingira yalikuwa kwamba isipokuwa kwa kifungu hiki kosa hilo lingehesabika kuwa kuua kwa kukusudia, atakuwa ni mkosa kwa kosa linaloitwa kuua mtoto mchanga na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi miaka saba".

Hapa ndio kwenye mchango wangu unapoanzia.

Mhe. Naibu Spika, adhabu hii kwa kuua mtoto mchanga mimi naona ni ndogo iongezwe, na hasa pale anapozaliwa mtoto mchanga nje ya ndoa maana ndiyo matokeo mengi sana yanayotokezea hapa, watoto wanapotea katika hali hiyo, kifungo kama hiki kiongezwe angalau miaka 2 na isizidi miaka 10 kwa sababu, hii itaonesha kwamba wale wengine wenye kuona kitendo kama hiki ni kibaya wataanza kujirekebisha. Wataacha kufanya tendo ambalo linasababisha kupata mtoto, itakuwa ni adhabu kila mmoja anafikiria kwanza mimi nikifanya hivi matokeo yake ni nini.

Kwa hivyo adhabu kama hii huenda ikapunguza kuweza kufanya mimba ambazo haziko katika desturi nzuri. Lakini Mhe. Naibu Spika, mtoto huyu kama atazaliwa mimi nashauri kwamba ikitokezea hivyo, yule mama ambaye amezaa mtoto huyo ni vyema ampeleke kwenye taasisi ambazo zinahusika na usalama wa mtoto huyo kama hospitali au polisi, kwani kuna watu ambao hivi sasa wamehangaika katika maisha yao kutafuta mtoto. Mtoto yule ataweza kulelewa na mtoto yule anaweza kuwa ni mtoto mwenye manufaa zaidi kuliko yule ambaye amezaliwa ndani ya ndoa.

Mhe, Naibu Spika, naomba sana wananchi katika jambo hili, wale ambao hawajafanya basi ikitokezea kama hilo wasifanye hivyo. Naomba sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika, jengine niende katika sehemu ya 25 ya Mswada huu kifungu namba 267 naomba ninukuu.

Kifungu namba 267 kinasema:

"Ikiwa karafuu ni mali ya serikali au mashirika yake zimeibiwa mkosaji atapewa adhabu zifuatazo:"

Mhe. Naibu Spika, kwanza hapa kabla ya adhabu naomba katika kutaja hizi mali zisitajwe serikali na mashirika tu, kwa sababu asilimia kubwa hii mali ya karafuu ni ya wananchi. Kwa hivyo, kifungu hiki hapa kisiwekwe hivi bali kiongezwe kama mali hiyo ni ya mwananchi yeyote nayo itahusika na adhabu hiyo. Ikiwa kitaingizwa hapo sasa ndipo katika hizo adhabu.

Adhabu inasema:

a)"kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka kumi".

Sawa mimi sina matatizo lakini

(b) "akiwa katika Chuo cha Mafunzo atapanda na atailea mikarafuu mia moja".

Sasa Mhe. Naibu Spika, tujiulize tayari serikali imeshajiandaa maeneo ya kupanda mikarafuu hiyo. Kwa sababu hili ni tendo ambalo kila mwaka linafanyika, zinapozaliwa karafuu lazima wezi wa karafuu watatokea. Tumejipanga vipi kuhakikisha kwamba adhabu hii itatekelezwa mtu akiwepo katika Chuo cha Mafunzo. Lakini atailea vipi mikarafuu hiyo mia moja, hapa tuangalie tena upya kweli hili tunalolitunga hapa linaweza kutekelezeka au tunaliweka tu kwenye maandishi. Hapa miye ndio penye wasi wasi wangu kwamba naona hata tukiweza kuweka adhabu hii haitoweza kufanya kazi. Kwa sababu maeneo ambayo yamewekwa siyaoni, wala sijui kama yametayarishwa kiasi gani. Kwa hivyo, itakapoonekana kwamba tayari tumeshaweka maeneo mwenye kosa kama hili tunajua tunampeleka moja kwa moja na anaweza kutekeleza ile adhabu.

Mhe. Naibu Spika, lakini jengine niwapongeze walioandaa Mswada huu kuona kwamba vile vifungu kwa ujumla wake ambavyo katika sheria iliyopita havikuwemo na leo wamevileta ndani ya Baraza hili na ndani ya Mswada huu tutaona tunavipitisha. Kwa mfano yalipozungumzwa masuala ya uhaini yalikuwa hayazungumzwi katika sheria iliyopita lakini sasa katika sheria zetu tunaona yameanza kuzungumzwa.

Mhe. Naibu Spika, ni imani yangu kwamba sheria hizi tulizozipita hapa ni kweli tunazitunga leo, tunazitunga kwa nia safi kabisa na bila ya kumtungia mtu yeyote lakini tutakapoona kwamba sheria ambayo tumeitunga hapa na kwa utekelezaji wake ni vigumu basi tusisite kurudi hapa kuifanyia tena marekebisho, kwani huu siyo Msahafu tunaweza kuona kifungu hiki hakiendani na hali yetu ilivyo nchini basi naomba sana tusione kuiacha kwenye vitabu ikawa imekaa tu naomba sana tuirudishe hapa tuifanyie marekebisho.

Mhe. Naibu Spika, nawaomba sana Waheshimiwa wenzangu nao wajitahidi kupekua Mswada huu na wao wauchangie kama vile ambavyo mwenyewe mtu ataona.

Baada ya hayo naunga mkono mswada huu mia juu ya mia pamoja na marekebisho yake. Ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Shehe Hamad Mattar. Sasa nimkaribishe Mhe. Asha Abdalla Mussa atafuatie Mhe. Rashid Makame Shamsi na pia ajitayarishe Mhe. Said Omar Said.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii ili kuweza kuchangia Mswada wa sheria mpya ya adhabu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niwapongeze sana waandaaji wa Mswada huu, lakini pili niwapongeze Kamati ya Katiba na Sheria kwa kuweza kutuwasilishia na kupendekeza mapendekezo mengi ambayo wameyaona kupitia katika kamati yao.

Mhe. Naibu Spika, sote tunafahamu kwamba Baraza lako hili tukufu kupitia mimi Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa, nikiwa ni mwana Uwawaza niliwahi kuleta hoja binafsi inayohusiana na masuala mazima ya udhalilishaji wa wanawake na watoto, lakini pia hoja ile ilizungumzia hasa jinsi ya mfumo mzima wa uendeshaji wa kesi hizi za udhalilishaji wa wanawake na watoto.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kati ya maazimio ambayo tuliyapitisha hapa likiwemo azimio la adhabu ya kubaka na masuala mazima ya udhalilishaji. Kwa kweli niishukuru sana na niipongeze sana Serikali ya Zanzibar pamoja na watendaji wake wote kwa kuamua kwa makusudi kwa kuandaa sheria hizi za adhabu na hivi leo kuleta hapa Barazani kwa ajili ya kupitisha sheria hizi na baadae ziweze kufanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, suala la udhalilishaji jamii nzima inafahamu na inaona lakini pia tumeona katika Sheria ya Adhabu ya Namba 6 ya mwaka 2004 kuna mapungufu ambayo yalikuwepo na mapungufu hayo ikiwemo adhabu ya kubaka. Hapo mwanzo mtu akigundulika ana kosa la kubaka mshitakiwa huyo sheria hapo mwanzo ilikuwa inazungumzia kwamba mwisho wa adhabu yake ni miaka saba, lakini sasa tunaipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa makusudi ya kuamua kwamba kwa sasa katika kifungu cha 109 kinasema kwamba " Mtu yeyote ambaye anabaka isipokuwa katika mazingira yanayoelezewa katika kifungu cha 2 atapewa adhabu ya kifungu cha maisha na katika hali nyingine yoyote atapewa kifungo kisichopungua miaka thelathini".

Mhe Naibu Spika, kwa kweli tupongeze sana, hili litafanya kwamba mtu ambaye anataka kujaribu na kutaka kubaka basi ataiheshimu hii sheria. Ninachokiomba kwamba kwa jamii husika ibadilike na ione kwamba sasa hivi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeamua na ipo tayari kuwashughulikia wale wote ambao wanatenda vitendo hivi vya ubakaji.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia katika sheria hii katika kifungu namba 110 pia imemzungumzia mtu ambaye anabaka yaani kwa mtu mmoja au kwa makundi, pia katika sheria hii imezungumzia kwamba endapo kosa la kubaka limetendwa na mtu mmoja au zaidi ya kundi, kila mtu katika kundi hilo aliyetenda au aliyesaidia kutenda kosa hilo atachukuliwa kwamba ametenda kosa la kubaka kwa makundi, lakini pia imesema kwamba mtu ambaye atajaribu kubaka atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka ishirini, pia suala hili mimi nalipongeza sana na nakubaliana na kifungu hiki.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala zima la utoroshwaji wa watoto wa kike na wa kiume, sote ni mashahidi na tumeona hivi karibuni tu Wizara ya Elimu ilipokuwa inatangaza matokeo ya kidato cha pili pamoja na mengineyo tumeona kwamba wanafunzi wengi wameshindwa kufanya mtihani wengine walitoroshwa, wameolewa lakini pia tumeona kwamba watoto ambao walitakiwa waendelee na masomo yao wameshindwa kurudi maskuli kwa sababu walitoroshwa na baadae wakakamatiwa wakaolewa.
Mhe. Naibu Spika, kwa kweli suala hili mimi nafurahika nalo kwa sababu litakomesha wale wote wanaopenda kutorosha watoto wa kike au wa kiume kwa nia ya kutaka kuwakomoa. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli masuala ya udhalilishaji tunayafahamu sote na kila siku yanajitokeza japokuwa kila siku serikali inapiga vita pamoja na viongozi wote kwa jumla, lakini bado yanajitokeza. Hivi karibuni tulisikia kwamba kuna mtoto wa kike amebakwa lakini kesi hizi zinashindwa kuendelezwa na kutolewa hukumu,

na ushahidi wote unaonekana lakini hatujui ni tatizo gani, lakini inafika pahala mshitakiwa anapewa dhamana pia baadae mshitakiwa huyu anatoroka anakimbia. Kwa hivyo ushahidi tena unakosekana kupatikana.

Mhe. Naibu Spika, natumai kwamba sheria hizi zikitekelezwa ipasavyo na wale wasimamizi wa sheria hizi naamini kwamba suala zima la udhalilishaji litapungua hapa Zanzibar. Natoa mapendekezo yangu au ushauri katika kifungu cha 114 ambacho hiki kinasema shambulio la aibu, lakini kifungu hiki cha 114 kimetofautiana na kifungu cha 135, kifungu cha 114 kinasema kwamba:-

"mtu yeyote ambaye bila ya halali na bila heshima anamshambulia mwanamke au mtoto wa kike atakuwa ni mkosa na akitiwa hatiani atapewa adhabu ya kifungo cha kipindi kisichozidi miaka kumi na nne na atatozwa fidia itakayoamuliwa na Mahakama".

Mhe. Naibu Spika, ukikiangalia kifungu cha 135 kinazungumzia shambulio la aibu kwa mtoto wa kiume na shambulio hili la aibu kwa mtoto wa kiume yeye kapewa pale miaka ishirini na tano. Mimi napendekeza kwamba kifungu hiki cha 114 kimtizame mwanamke ndiye anayeshambuliwa siku zote mashambulio ya aibu na wanaotudhalilisha sana ni wanaume, hao wanaume mliowaweka huku kwenye kifungu namba 135 kwamba mwanamme yeye akishambuliwa kwa shambulio la aibu yeye atapewa miaka ishirini na tano, lakini kwa mwanamke miaka isiyozidi miaka kumi na nne. Naomba sana watutizame sana tunaoathirika sana ni wanawake. Tunaomba kifungu hiki basi kiendane na kifungu cha 135 ambacho kisomeke kwamba:

"shambulio la aibu kwa mtoto wa kiume au wa kike wapewe adhabu yote sawa".

Mwisho Mhe. Naibu Spika, naomba sana wanaosimamia sheria hizi, watekeleze ipasavyo ili haki zitendeke na tuone kwamba suala la ubakaji, kutorosha na mashambulio ya aibu yaweze kuondoka hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa haya machache niungane na wenzangu napitisha mswada huu kwa asilimia mia moja, Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante san Mhe. Asha Abdalla Mussa. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Rashid Makame Shamsi baada ya hapo atafuata Mhe. Said Omar Said, ajitayarishe Mhe. Nadir Abdul-latif.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe.Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Mswada huu unaohusiana na sheria za adhabu. Awali nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na watendaji wake kwa kuweza kuuleta Mswada huu muhimu ambao ni dira ya amani katika nchi yetu.

Mheshimiwa vile vile nichukue fursa hii kuipongeza sana Kamati inayoshughulikia Katiba na nimpongeze kwa dhati sana muwasilishaji wa ripoti, Makamo Mwenyekiti, Mhe. Mwantatu. Vile vile nichukue fursa hii kuwapongeza wale wote walionitangulia katika michango yao katika Mswada huu muhimu sana. Niwaombe na wengine wajitokeze ili tuuchangie kwa nguvu ili hatimae tuweze kuupitisha Mswada huu muhimu.

Mhe. Naibu Spika, Mswada huu ni muhimu sana na wenzangu wametangulia kusema kwa sababu kelele nyingi tulikuwa tunapiga Barazani lakini hata katika jamii juu ya makosa ambayo yanapaswa kutochukuliwa dhamana ambayo kwa wakati ule yalikuwa yanachukuliwa dhamana. Mswada huu umeongeza

makosa kutoka matano (5) hadi kumi na moja (11) ambayo sasa yatakuwa hayana dhamana. Kwa hivyo moja kati ya vilio vyetu vile hivi sasa nafikiri vimenyamazika, ikiwemo hususan lile kosa la udhalilisha ambalo limetawala zaidi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile tulikuwa tunapiga kelele sana juu ya adhabu ambazo tulikuwa tunahisi haziendani na uzito wa makosa. Kwa hivyo tushukuru sana katika Mswada huu wa Sheria adhabu nyingi zimeongezwa ili kuona kwamba zinaendana sasa na wakati na zinaendana na uzito wa makosa. Hili linaleta faraja na tuipongeze sana serikali yetu sikivu kwa kuweza kuliona hili na hivi sasa nina imani kwamba sisi Wajumbe wa Baraza, lakini vile vile na jamii inayotuzunguuka tutakuwa tumepata ahuweni kidogo kulingana na vile vilio vyetu.

Mhe. Naibu Spika, suala la kuongeza uzito wa adhabu ni suala moja lakini suala la kutenda makosa ni jambo la pili. Tumeongeza kiwango cha adhabu katika makosa hususan ya udhalilishaji. Tujiulize tu kwamba kuongezeka kwa adhabu kunaweza kuwa muwarubaini wa kuweza kuondosha tatizo, nafikiri hauwezi ukawa ni muarubaini wa moja kwa moja inaweza likawapunguza ongezeko la makosa. Mimi niiombe sana jamii pamoja na marekebisho haya suala la msingi ni suala la maadili. Tukubali kwamba jamii yetu maadili yameporomoka tumeongeza adhabu lakini kama maadili yatakuwa hayapo basi tatizo linaweza kuendelea kubaki. Kwa hivyo niiombe sana jamii kuweza kubadilika kuweza kuendana na maadili yale ambayo tulikuwa tunayafuata hapo nyuma.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, ukiacha suala hili suala jengine lipo katika ushahidi, sheria hii imeongeza adhabu lakini kama wananchi wetu hawajabadilika kuweza kukubali kukaa ushahidi juu ya makosa haya hususan ya udhalilishaji, basi bado tutawapa mwanya wale wahalifu kuendelea kufanya makosa. Kwa

hivyo niiombe sana jamii kubadilika na kuwa tayari kuweza kuchukua nafasi ya ushahidi wa dhati kabisa katika kusimamia kesi hizi ili wahalifu hawa waweze kutiwa hatiani na hatimae waweze kutumikia vifungo.

Mhe. Naibu Spika, nikija katika waraka wa Mswada huu katika ukurasa wa 274 kifungu cha pili katika maneno ya ufafanuzi neno la tano kutoka juu limesemwa neno kilema, nilikuwa natoa mapendekezo tu kwamba msamiati huu kwanza ni msamiati ambao katika waraka huu haukujitokeza, neno ambalo limejitokeza ni neno walemavu, lakini vile vile katika muktadha wa wenzetu wa jamii ya walemavu neno hili kwao hivi sasa sio rafiki sana kilema. Kwa hivyo ningependa hilo neno tulirekebishe na likae walemavu.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije ukurasa wa 326 kuna suala zima la kifungu hichi cha 163 kinachozungumzia watu wavivu na wenye tabia mbaya, pamoja na kutaja watu mbali mbali hapa wenye tabia mbaya lakini kutokana na wakati unavyokwenda nilikuwa napendekeza, kifungu cha kuongeza juu ya wale watu ambao wanatembea wakiwa wamevaa nguo za karaha au nusu uchi. Hivi sasa tabia hii inashamiri na wenzetu kule Tanzania Bara wameshaanza kupingana nayo. Sasa hilo wimbi la watu wa aina hii sasa wanaelekea Zanzibar. Kwa hivyo kungekuwa na kifungu cha kuweza kuwaadhibu watu hawa ambao wanatembea wamevaa nguo za karaha au nusu uchi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, sasa nije katika ukurasa wa 332 katika kifungu cha 187 katika kifungu hichi imezungumzia juu ya kuuwa mtoto mchanga. Hivi sasa kuna wimbi kubwa sana la akinamama kuweza kusababisha vifo kwa watoto wao waliowazaa, lakini Mhe. Naibu Spika, ukweli ni kwamba adhabu iliyowekwa hapa kifungo cha kipindi kisichopungua miezi sita au kisichozidi miaka saba, hichi kifungo ni kidogo mno. Kwa sababu wimbi hili sasa

hivi limekuwa kubwa na sababu ambayo imesemwa hapa kutenda huko mezania ya akili ilikuwa inasumbuliwa, mezania ya akili tutaipima vipi kwa huyu mtu ambaye ameweza kutenda kosa, kwamba mezania yake ya akili ilikuwa inasumbuliwa lakini mtoto huyo anayetajwa hapa ni mtoto chini ya umri wa miezi kumi na mbili na inawezekana na miezi kumi na moja, ina maana huyu mtu aliyejifungua mpaka miezi kumi na moja mezania yake ya akili haijakaa sawa.

Mhe. Naibu Spika, hili lazima litizamwe upya vyenginevyo watu watajifungua na wale wenye dhamira mbaya ya kuwauwa watoto wao au kwenda kuwatupa na watoto wale ikawa ni sababu ya vifo vyao. Lakini katika kifungu hichi hichi kimeeleza endapo mwanamke au mtoto wa kike kwa kitendo chochote inaendelea. Mhe. Naibu Spika, mtoto wa kike hajifungui. Hichi kifungu lazima kifanyiwe marekebisho, anayejifungua ni mwanamke, ukisema mtoto wa kike kujifungua mimi sikubaliani nalo, *otherwise* itolewe ufafanuzi katika tafsiri kulw, mtoto wa kike ni kuanzia umri gani ambaye anaweza kujifungua.*(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nielekee katika ukurasa wa 364 katika kifungu cha 319 kinachohusu uchomaji wa mali kwa makusudi. Katika kifugu kidogo cha (c) napenda nikisome kinasema, samahani kifungu cha (b) "chombo chochote kile kiwe kimekamilika au bado hakijakamilika", yaani mtu kama atachoma chombo chochote kile kiwe kimekamilika au hakijakamilika ina maana atakuwa ameweza kufanya kosa hilo. Lakini Mhe. Naibu Spika, kosa hilo adhabu yake ni kifungo cha maisha. Sasa mtu amechoma chombo ambacho kimekamilika au hakijakamilika adhabu yake iwe kifungo cha maisha, hilo mimi nalipinga.

Lakini vile vile tukitazama tafsiri ya hicho chombo katika ukurasa wa 277, chombo kinasema nini ni Jumuiya inayojumuisha meli, boti na kila aina ya chombo kinachotumika kusafiria majini, aina

ya chochote kinachotumika kusafiria majini. Sasa majini kuna vyombo vingi vya kuafiria na vyengine ni vidogo ukilinganisha na meli au boti. Sasa kuna mitumbwi inatumika kusafiria, sasa mtu atakuja kuchoma mtumbwi wa mwenziwe, kifungo chake kiwe ni maisha. Hii mimi ningependa kipengele hichi kiweze kurekebishwa au tafsiri ya chombo iweze kurekebishwa.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha (b) katika kifungu cha (c) imejumuisha vile vile mrundikano wowote wa mazao ya mboga mboga au wa madini au wa mafuta ya matunda, yaani utakapochoma mrundikano wa mazao adhabu yake ni hiyo kifungo cha maisha. Mheshimiwa hapa hatujatenda haki lazima kifungu hichi kifanyiwe marekebisho mtu anaweza kuja kuchoma rundo la mboga za watu akaja akafungwa maisha hapa. Aidha vile vile kifungu kinachohusiana na mazao Mhe. Naibu Spika, kimetajwa katika 321, kwa hivyo kingeelekea huko yale masuala yote ya uchomaji wa mazao basi yangekuwa yanaelekea huko.

Mhe. Naibu Spika, niweke msisitizo tu kwamba sheria hii ni nzuri imejaribu ku-*cover* mambo mengi ambayo tulikuwa tunayalilia na msisitizo zaidi uwe katika maadili lakini vile vile katika mashahidi kuweza kuchukua nafasi yao katika kutoa ushahidi katika kesi mbali mbali na hiyo ndio itakayosababisha wale wanaotuhumiwa na makosa kuweza kuingia hatiani, bila ya hivyo basi tutakuwa yale matatizo ambayo tunataka yaondoke basi yanaweza kubaki au kuendelea kubaki.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu wachangiaji ni wengi na mada hii ni muhimu sana basi nishukuru na niwaombe wenzangu waendelee kuchangia mada hii ili hatimae tupitishe kwa pamoja Mswada huu, na mimi naunga mkono Mswada huu asilimia mia kwa mia Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Rashid Makame Shamsi, sasa nimpishe Mhe. Said Omar Said na baada ya hapo naomba ajitayarishe Mhe. Suleiman Sarahani.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu Jaala Subhanahu Wataala kwa kuniwezesha kwa mara nyengine kuhudhurika katika kikao cha leo Ijumaa. Pili nikushukuru na wewe kwa kunipa na mimi nafasi hii ya kuchangia angalau dakika mbili tatu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Adhabu, kutunga Sheria mpya ya Adhabu kuweka masharti bora zaidi pamoja na mambo mengine yanayohuiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri mhusika pamoja na watendaji wake wote wanaohusiana na Mswada huu, lakini pia niipongeze Kamati ya Katiba na Sheria kwa kuweza kupitia Mswada huu na kuweka marekebisho tunayoyaona hapo mbele. Lakini vile vile nichukue nafasi ya kumpongeza mpaka muwasilishaji wa ripoti hii ya Kamati.

Mhe. Naibu Spika, nipongeze Mswada huu kwamba umemaliza mambo yote na mahitaji yote ya watu wa Zanzibar. Mswada huu wanaupenda wanaadamu wote, mwizi anaupenda Mswada huu mwizi hapendi aibiwe eti, mzinifu pia anaupenda Mswada huu, mzinifu hapendi aziniwe. Kwa hivyo Mswada huu umemaliza mahitaji ya Wazanzibari.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mimi kidogo nataka nianze na ukurasa wa 282 sura ya tano adhabu mimi nipongeze tu mtiririko wa adhabu zilizobainishwa hapa, lakini katika adhabu zilizobainishwa hapa nataka nibakie kwenye herufi (h) kuweka dhamana kwa ajili ya kutunza amani na kuwa na tabia njema ni miongoni mwa adhabu zinazopendekezwa kutolewa katika Mahakama. Lengo la

Mahakama si kuadhibu, lengo ni kuondosha uovu, kama lengo ni hilo basi ni vyema kwa baadhi ya makosa yawekwe hukumu hii namba (h) kuna makosa ambayo hayahitaji dhamana ya papo kwa papo kisa mkasa. Lakini kuna makosa mengine inafaa adhabu hii kwa mfano.

Mtu kuwashawishi watu wasitende halali kwa mfano watu kuwashawishi watu kufanya vurugu, kufanya fujo kuondoa amani, sasa mtu kama huyu akigundulikana akafungwa miezi sita au miaka minne mfano, aah! mimi naona apewe hii (h) aweke dhamana achukue dhamana kwa ajili ya kutunza amani na kuona tabia njema kwa kipindi cha miaka kumi apewe dhamana hiyo ya kutunza amani kulikoni kufungwa miezi sita. Nataka tuamini kwamba kujizuia na uovu ni kazi zaidi kuliko kufanya ibada, nataka tukubali hapo mtu anaweza akaamka saa 10.00 akenda akaadhini halafu akenda akaiba, ni kosa hilo, anaweza akaswali halafu huku akaazini. Kwa hivyo tujue kwamba kujizuia ni ngumu zaidi kuliko kutenda yale makosa, sasa tunapompa mtu dhamana hii ni kazi ngumu, hii ni ni adhabu kubwa kulikoni kumfunga miezi sita.

Nikitoka hapo nataka niende ukurasa wa 317 katika kifungu 142, kinasema nanukuu.

> "Mtu mwanamme yeyote ambaye anamuingilia kingono mwanamke ambaye anajua au ana sababu ya kuamini kuwa ni mke wa mtu mwengine bila ya ridhaa au ruhusa ya mume wake ambapo kumuingilia huko hakuhesabiki kuwa ni kosa la kubaka atakuwa ni mkosa"

Mhe. Naibu Spika, mimi napendekeza neno moja liondoshwe, lifutwe

> "…bila ya ridhaa au ruhusa ya mume wake"

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu zinaa ni kitendo cha mwanamme kumuingilia mwanamke ambaye siyo wake, ndiyo zinaa. Hata ikawa

mtu hajaolewa yupo kwa wazazi wake, wazazi wake wakaruhusu mtoto yule aziniwe, basi bado ni kosa hilo. Hakuna ruhusa ya mume kutoa ruhusa ya kuziniwa mke wake, pia hilo ni kosa. Kwa hivyo naomba sehemu hii ifutwe iwe haimo ili isomeke hivi:

> "Mtu mwanamme yeyote ambaye anamuingilia kingono mwanamke ambaye anajua au ana sababu ya kuamini kuwa ni mke wa mtu mwengine hilo litakuwa ni kosa".

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye ukurasa wa 318 katika kifungu cha 143(2) kimeeleza hivi naomba kunukuu.

> "143(2)Iwapo mkosaji ni mtu mwanamme mkosaji huyo atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka 25.
>
> (3) Iwapo mkosaji ni mtu mwanamke mkosaji huyo atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka 5."

Kwa nini? Namuomba Mhe. Waziri aje atupe sababu kwa nini huyu akapewa miaka mingi mwanamme 25 na mwanamke akapewa miaka mitano (5) au ni kutokana na udhaifu wao au ni kwamba Mahakama inawaonea huruma na kama ni hivyo kama inawaonea huruma tuje Nam. 5.

> "(5) Iwapo itadaiwa kwenye taarifa au shitaka na ikadhibitika kwamba mtu mwanamme ana umri chini ya miaka 12 mkosaji mwanamke atapewa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka 20. "

Kwa hivyo ina maana hapa hakuna huruma, sasa kwa nini kule kukawa na huruma, namuomba Mhe. Waziri atufafanulie.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 305 makosa yanayohusiana na Dini. Serikali haina Dini lakini Wazanzibari wana Dini yao, kila mtu ana Dini yake, watu wana Dini zao. Dini za watu ni sawa sawa na nyumba za watu, hakuna aliyetayari kuingiliwa nyumba yake bila ya idhini yake.

Hakuna aliyetayari kuchafuliwa nyumba yake na mtu mwengine na ikitokea hivyo ina maana hapo pashaanza kuvunjwa amani. Tuelewe kwamba mtu anapotukana Dini nyengine ambayo siyo yake, ni sawa na mtu aliyemtukana baba wa mwenzake ambaye si wake, maana yake anataka na yule baba yake atukanwe. Kwa hivyo yeyote anayemtukana mtu maana yake amemtukana mtu wake. Kwa hivyo na huyu yeyote ambaye atathibitika kutukana Dini nyengine, kwa mfano huyo mtu ni Muislamu ametukana Dini nyengine basi ahesabike huyo ameutukana Uislamu kwa sababu ni lazima na Uislamu utashambuliwa.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na hayo adhabu yake imeeleza kwamba mtu ambaye anakashifu Dini atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi miaka saba. Hiyo ni ndogo mno adhabu hiyo. Kukashifu Dini za watu yeyote akayekashifu Dini ya mwenzake Dini yeyote lazima huyu apewe adhabu zaidi ya hii. Naomba sana kwamba adhabu hii ni ndogo mno kwa masuala ya Kidini, kwa sababu Dini ndiyo sheria yenyewe. Sasa atakayeitukana sheria vipi, mtu huyo ni, lazima apate adhabu kuliko adhabu zozote. Naomba sana hapa izingatiwe zaidi, adhabu hii ni ndogo mno kwa ajili ya Dini.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja nakushukuru sana.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Said Omar Said, mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu atakuwa ni Mhe. Suleiman Sarahan Said, karibu Mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii na muda uliobakia nafikiri utanitosha kwa sababu wengi wapo watakaochangia na wengine wameshachangia mengi na mimi nichangie kidogo.
Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nawashukuru kuaanzia Waziri na watendaji wote walioshughulika katika kuandaa mabadiliko haya ya adhabu hizi ambazo labda tuseme zimeshapitwa na wakati au nyengine ndio zimetanguliwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kwa kutunga kitabu hichi kwa ajili ya marekebisho ambayo ni mazito ni sawa sawa kwa duniani kutengeneza

silaha nzito kwa ajili ya wanaadamu baada ya kuona kwa silaha ndogo ndogo hawazuiliki. Kwa hivyo na sisi Zanzibar tukaona yale mambo ya zamani wenzetu wanatoka mbali au sisi wenyewe tunaiga kwa kujakujifundishia tena kwa upande wa Zanzibar kwa sababu sheria zetu zilikuwa ndogo za kibinadamu tulizokuwa tunazifuata kwa mujibu wa sheria yetu.

Mhe. Naibu Spika, kitabu hichi kina Sehemu 40, kina vifungu 397 ni kikubwa sana kwa kukichambua kimoja kimoja tunaweza tukafika wiki. Kwa hivyo kila mmoja anadokoa sehemu yake ambayo inaweza ikawa inagusa sehemu fulani ya kama kuboresha zaidi.

Mhe. Naibu Spika, ilikuwa tunafikia wakati katika miaka iliyopita mwanamke tunalikuwa tunamuona na kama Dini yetu ya Kiislamu wengine wanavyoona kwamba mwanamke ni mtu mdogo sana katika maumbile yake ya kinguvu, na pia ni mtu ambaye hajumuiki sana katika mambo mengi ya makosa ya jinai au makosa mengine ambayo yalikuwa ni makosa ya kiume kiume ambayo wanaume ndiyo walipaswa kuyafanya au kufanyiwa vitendo vyengine ambavyo vinafanywa kwamba adhabu zake ziwe hivyo.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi wanawake wamejiingiza katika makundi na katika sehemu ambazo hazikuwa kama ndiyo jinsia yao wala haikuwa katika nasaba zao za Kidini au kihulka zao. Lakini sijui kama ni wakati au mafundisho, lakini wanawake na wao au sijui yale maneno na sheria iliyosema kwamba wanawake na wao wana nguvu sawa labda wanataka kuingia kwenye *zone* za kiume.

Mhe. Naibu Spika, kitabu hiki ukitaka kukisoma na kukichambua kinaingia katika mambo mengi yakiwemo Dini, lakini pia unaweza ukasema kama unatukana. Maana kuna mambo humu yanayozungumzwa mengi ukiseme sio mambo ya kuyazungumza katika mambo ya haya, lakini ni lazima uyazungumze kutokana na kadhia iliyokwishakutufika. Ukisema neno ngono ilikuwa ni neno la maajabu sana lakini sasa inabidi tuliseme wazi wazi hata kwa watoto wako inabidi ufahamishe kutokana na hali halisi ilivyo na ndio kitabu hiki kikatungwa.

Mhe. Naibu Spika, niwausie sana wanawake adhabu zilizotungwa humu pamoja na wanaume ni kubwa na nzito. Lakini na wanawake na wao wamo katika jitihada za kuwafukuza wanaume katika nguvu za kujiingiza katika masuala kama haya.

Kwa hivyo na watungaji waliotunga katika maeneo haya….

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa sio wanawake ni baadhi ya wanawake. Siyo wanawake wote ambao wanafanya hivyo, kuna baadhi ya wanawake, sawa sawa na baadhi ya wanaume. Rekebisha kauli yako.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, nafuta kauli yangu baadhi ya wanawake lakini pia nafuta kauli yangu na kwa baadhi ya wanaume. Nashukuru Mhe. Naibu Spika, kwa maelekezo hayo uliyonielekeza.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze na Sehemu ya Tatu sioni kama ina marekebisho, lakini sehemu ambayo katika Sehemu ya Sita kutokujua sheria hakuwezi kuwa ni sababu ya kusamehe kwa kutenda kosa au kutokutenda kosa ambalo linaweza kuwa ni kosa, isipokuwa kama kujua sheria kwa mkosaji inaelezwa wazi kuwa ni kiini cha makosa.

Mhe. Naibu Spika, mimi si mtu jaji, wala si mtu Polisi lakini kwenye vyombo vya Sheria mara nyingi sisi tunapofanya makosa tunasema nilikuwa sijui na naona kama naonewa. Ningeiomba hii Wizara nao wakaweka *slogan* katika maeneo kwamba kutokujua sheria hakuwezi kuwa ni sababu ya kusamehewa. Angalau binadamu akajua kwa sababu hili neno dogo lakini linaonesha kama mimi nilikuwa sijui kwa hivyo mtu anaweza akajipima. Hili nilikuwa nalitolea mawazo kama litawekwa kama *slogan* katika maeneo kwamba kutokujua sheria sio kutenda kosa au kutokutenda kosa. Hapa nilikuwa nasemea hii ili liweze kuangalia hapa.

Lakini kuna sehemu nyengine katika hiyo hiyo katika kifungu cha 10, kutokuwa na akili timamu. Hili suala nano linakuwa na utata ambalo suala hili linakwenda sambamba na kuwajibika kwa watu kwenye kitu cha kutenda haki. Binaadamu hata kama ni mgonjwa wa akili lakini ugonjwa ule unakuja kuthibitika baada ya kuja kutenda kosa. Sasa

jamaa zake au kutokujua jamaa zake hawawezi kusema mgonjwa huyu ni wa akili mpaka akishakufanya madhambi yake. Hapa nilikuwa nasema kwamba kwa mtu ambaye atafanya kosa kwa wale jamaa zake baadae ndiyo watakuja ku- *claim* kama huyu ni mwendawazimu na hawakutoa taarifa mapema basi na hawa na wao sheria ichukue mkondo wake. Angalau na wao wapeleke taarifa kwamba mtu huyu ili tuweze kujua baadhi ya wendawazimu katika maeneo. Mtu mnamuona anafanya vituko hamsemi na ukimwita mwendawazimu anakuja mwilini. Ningeomba watu wanaohusika na hapo wakachukua suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine hapo hapo katika kifungu cha 13, umri mdogo wa miaka 12 unachukuliwa kuwa hauwajibiki kuwa ni kosa la jinai. Sasa hivi kama nilivyosema kwenye baadhi ya wanawake na baadhi ya watoto, wengine akili zimekuwa nyingi, mtoto wa miaka mitatu sasa hivi anatumia *compute*, mtoto wa miaka saba anaweza kukufanyia mambo huwezi kuamini. Maeneo haya ya kumuhusisha mtoto moja kwa moja kwamba hahusiki watatumika vibaya sana watoto. Hii sehemu tungeitizama vizuri tukajua hasa sio wale watoto wa zamani kwa watoto wa sasa wataalamu wakaitizame vizuri inakaaje, kwa sababu watoto ndio watakaotumiwa katika hizo *section* nyengine.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kidogo kidogo kwa haraka sana ukurasa wa 26 unaozungumzia suala la adhabu. Kwenye kitabu hiki bado kwenye sheria hii hakuna adhabu iliyotamkwa kwa kosa lolote, kosa hilo litaadhibiwa kwa adhabu ya kifungo kisichozidi miaka miwili au kupigwa faini shilingi milioni moja au vyote viwili kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningeweza kushauri kwamba tunakwenda sambamba na mwaka kwa milioni, kwa hivyo kama miaka miwili basi na milioni ziwe mbili, kama miaka mitatu basi na milioni ziwe tatu, inategemea kifungu na hiyo pesa yenyewe. Kwa hivyo hapa bado kulikuwa kunamarekebisho kama itawezekana yarekebishwe.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda kwenye Sura ya Sita Kifungu cha 33 ni kwamba tulizungumza hapa kwamba askari na vyombo vyetu vyote ni vyombo tunavyoviamini sana. Lakini nakubali maneno yako ni baadhi ya askari na wetu wengine wanaweza wakavitumia vibaya au wanaweza wakawa wanajitumikia kwa maslahi yao. Hichi nafurahi kwa niaba ya

hawa waliotunga sheria wataona hili kwamba na wao hawakuaminika kupita kiasi na badhi wapo wanaotumika haya. Kwa hivyo kifungu hichi nakipongeza lakini pia nimefurahi na kuona kwamba kuna watu ambao.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia muda umekwisha, maliza.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mheshimiwa namaliza kabisa au mpaka jioni, basi. Basi mimi nilikuwa natoa wazo kidogo kwa upande wetu wa Zanzibar tunapofanya matatizo au linapotokea tatizo katika kesi ya jinai, watu wengi ambao wanafika pale wanaweza wakawa wanavamia, wanapoteza ushahidi na wanamalizia kila kitu. Kwa hivyo ningeomba maeneo kama hayo tukaweza kubadilisha staili.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, Mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Namalizia Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Hapana muda wako umeshapita, nitakupa dakika 5 jioni ya kumalizia ukija mapema. Waheshimiwa Wajumbe muda wetu wa kumaliza kikao umeshafika kwa hivyo nisitishe Kikao hichi hadi jioni saa 11:00. Ahsante.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirejea)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea na majadiliano yanaendelea, asubuhi tulikuwa tumembakishia Mhe. Suleiman Said Sarahani dakika zake tano. Kwahiyo, Mhe. Suleiman naomba uzimalizie dakika zako tano na baada hapo mchangiaji atakayefuata ni Mhe. Mwanaasha Khamis na ajitayarishe Mhe. Tatu Ussi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika kwa msaada wako wa kuniona tena, ili dakika nyengine za nyongeza nipate kwa kumalizia kwanza hii niendelee tu kwasababu ya muda, ilikuwa nilizungumzia zaidi katika kifungu kile ambacho kimetaja vikosi vyetu kwamba kuna baadhi ya wengine wanakuwa uwaminifu wao kidogo wanateleza. Kwahivyo, nikasema tu kwamba pamoja na hayo pia baada ya kupata *training* zote zile za kijeshi ambazo wanafanya.

Lakini, wapate taaluma za kuweza kisheria ambapo kama mtu anaongoza kikundi kile basi moja katika wanaokuwa wana sheria kidogo waweze kwasababu baadhi ya wakati mengine wanaweza wakawa wanatumia nguvu zaidi kuliko zile sheria ambazo tumezitunga wenyewe.

Kwahivyo, hilo nilikuwa nalikazia kwamba walivyo elekeza humu ni vizuri sana lakini pia kuna haja ya kuongeza wanajeshi wetu sasa hivi ni wasomi na wana uwezo lakini labda ya mafunzo au taaluma nyengine zinakuwa kidogo zinakuwa mbali nao.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nazungumzia kuhusu habari ya maeneo mengi ambayo yanatokea uhalifu hasa Zanzibar mara nyingi tunakosa ushahidi kutokana na kupoteza ushahidi kwa watu ambao wanawahi kuingia kwenye eneo lile kabla ya vikosi vinavyohusika kuweza kulizingira lile eneo na kupata ushahidi, utakuta kama pamefanya uhalifu basi utamkuta mtu kaokota kisu, kaokota kitu gani bila ya kujua kwamba athari zake zile zinaweza zikamrudia yeye baada ya kuja kuangalia *finger print* na vitu vyengine.

Kwahivyo, ningeshauri sana wananchi baada ya kutokea uhalifu wakaweza kuliachia eneo lile watu au vikosi vinavyohusika na maeneo yale, ili waweze kupata ushahidi wa kusaidia katika kutatua tatizo hilo, wa hivyo Mhe. Spika nilikuwa nakazia na hilo.

Lakini pia najaribu kuzungumza kwamba nchi hii kila mmoja ni askari, kwa hivyo utaratibu wa kumkamata mhalifu kuzuwiya kosa au kufanya kosa kila mmoja linamuhusu ukiachia kwamba kuna utaratibu wa vikosi maalumu vinafanya kazi yao, lakini kila mmoja ni askari wa mwezake anapomuona kama anafanya uhalifu au anataka kufanya uhalifu anayo sheria ya kuweza kumzuwia au kumkamata akitaka kufanya uhalifu huo.

Mhe. Naibu Spika, pia mimi naunga mkono baadhi ya katika mahkama zetu tunao *ma-assessor* ambao wanatusaidia katika kesi zetu ambao wanamsaidia Mhe. Jaji au Mhe. Hakimu katika kusikiliza kesi na kuweza kumpa maelekezo ya kwamba nini ambacho kilitendeka zaidi na ufahamu wao. Lakini kwa utaratibu wa marekebisho ni kwamba sasa hivi *ma-assessor* wote watakuwa hawamo isipokuwa katika Mahkama Kuu, mimi naunga mkono hili kwasababu kwa upande wa Mahkama Kuu wasiondoshwe katika kesi hasa zile ambazo zinahusu na adhabu ya kifo wawepo ili kusaidia utaratibu ule, hilo naunga mkoni kutoka na tatizo hilo kwa hivyo hapo naunga mkono.

Lakini katika ukurasa wa 136 Mhe. Naibu Spika, naomba kunukuu.

Ukurasa wa 136 unasema hivi:-

" Mwanamke au mtoto wa kike ambaye anatenda tendo la usagaji na mwanamke mwengine au mtoto wa kike mwengine ama mfanyaji au mfanywaji atakuwa mkosa na atatiwa hatiani atapewa adhabu ya kifungu kwa kipindi kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka kumi ".

Mhe. Naibu Spika, hii ni *style* mpya imeingia katika nchi yetu ilikuwa haipo, ikiwa miaka mitano inatosha kulikomesha jambo hili sawa, lakini kama haitoshi basi iongezwe muda au miaka

kwasababu ya jambo hili liweze kuondoka, lakini tatizo linalonipa shida hasa ushahidi wa huyu msagaji na mswagajwi nini maana yake sijui kuna kitu gani ambacho kitakamatwa kitakuwa kitakuwa ni ushahidi wa jambo hili walikuwa wakifanya.

Sasa hili ndio namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapo kuja kufanya majumuisho ataweza kunifafanulia pale panakamatwa nini, ili kionekane kwasababu wanawake wakikaa kwenye chumba ni ruhusa, wanawake kulala pamoja ni ruhusa, wanawake kupelekana chooni ni ruhusa ni wajibu wetu lakini utakuta tukamate nini hiki? Kwahiyo, Mhe. Naibu Spika, hapa naomba Mhe. Waziri atakapokuja katika ushahidi huu kama ameliona lipo, basi atupe na ushahidi ukimkamata hivi kavua nguo, kafanya hivi atajulikana huyu alikuwa akifanya hivi. Kwa maana hiyo, namuomba Mhe. Waziri hili aliangalie kidogo ili tuweze kujua huyu mtu atakuwa ushahidi gani wa kukamata.

Lakini niendelee katika kifungu ambacho Mhe. Waziri alitoa katika mahkama zetu kwamba uwezo wa mahkama zetu uwezo wa majaji wetu ulikukwa kama Mahkama za Mkoa ilikuwa mwisho kusikiliza kesi ambayo ina uwezo kama wa milioni saba (7,000,000/=) na sasa hivi wameongezea kama milioni kumi na nne (14,000,000/=).

Mhe. Naibu Spika, mimi hapa kutokana dhana nzima ya pesa zetu kwa sasa hivi na pesa zenyewe zilivyo katika nchi yetu, pesa zimepanda chati sana kwamba Mahkama za Mkoa zina nguvu na zina maeneo makubwa na zina mambo mengi badi *amount* ya milioni kumi na nne (14,000,000/=) ni ndogo ningesema kwamba ikiwa baada ya milioni kumi na nne (14,000,000/=) mtu anaendea Mahkama Kuu kesi nyingi zitaweza kurundikana Mahkama Kuu kwasababu *amount* ya pesa sasa hivi katika kisiwa chetu pesa ni nyingi.

Kwahivyo, kitu cha milioni kumi na nne (14,000,000/=) ni kitu kidogo kwa hivyo mambo mengi yanakuwa kwenye milioni thelathini (30,000,000/=). Hivyo, ninashauri Mhe. Naibu Spika, kwasababu hakuna madhara zaidi sijui kama kutakuwa na nyengine tukaongezea milioni thelathini (30,000,000/=) kutokana na uwezo wao Mahkama ya Mkoa na wengine wale wakapandishwa kutokana na nafasi zao ili kuweza kujua kwamba tathmini halisi itakuwa ni kiasi gani.

Lakini mimi nilikuwa nazungumza pamoja na yote haya Mhe. Naibu Spika tumeshatunda sheria, tumeshatunga adhabu, tumeshafanya kila kitu kwa kweli kila mmoja anataka awajibike kwa namna ambavyo ametakiwa kuwajibika kama hatutokuwa na umoja tukaweza kusaidia...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Suleiman Said Sarahan, nimekupa dakika tano tu na zimeisha.

Mhe. Suleiman Said Sarahan: Naomba sana Mhe. Naibu Spika, katika jadweli hili makosa mengi ya kijinai, makosa mengi ya udhalilishaji tunapiga kelele lakini kama hakuna ushirikiano wa daktari, askari, mahkama, raia basi sheria hizi tutazitunga kila siku tukizibadilisha bila ya kuwa na uweledi wa uhakika ambao kila binadamu anatakiwa ajuwe kama mwezake amefanyiwa kosa basi haki itendeke itakuwa hatujafanya kitu chochote.

Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii naunga mkono hoja asilimia mia ahsante *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Suleiman mchangiaji anayefuata ni Mhe. Mwanaasha Khamis atafuata Mhe. Tatu Ussi na ajitayarishe Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Asante sana Mhe. Naibu Spika na mimi kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika mswada uliokuwepo hapa mbele yetu kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Rais na watendaji wote wa serikali ambao wameona suala hili lina umuhimu kutuletea hapa juu ya Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Adhabu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi kilichopita natumai na wewe uliwahi kuleta hoja ya udhalilishaji lakini pia katika madhimisho yako pia ulipendekeza maazimio ulipendekeza kuwa Sheria ya Adhabu ibadilishwe na kwasababu ilikuwa haikizi vigezo, lakini vile vile na kipindi kilichopita Mhe. Asha Abdalla Mussa wa Jimbo la Kiwengwa na yeye alileta hoja binafsi humu Barazani naye pia katika maazimio yake na yeye alitaka pia kufuta Sheria ya Adhabu na niwapongeze serikali na waziri wameliona hilo na wametuletea.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije moja kwa moja katika mswada huu sehemu ya 13 Makosa Dhidi ya Maadili kifungu 113.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 109 kuna adhabu ya kubaka na 110 kuna adhabu ya kubaka kwa kundi, 111 kuna kujaribu kubaka.

Mhe. Naibu Spika, napongeze sana kwa marekebisho haya lakini nije katika kifungu cha 113 ambacho *marginal note* yake iko kutoshosha watoto wa kike na wakiume.

Mhe. Naibu Spika, hapa tumeona kuwa kuna kifungu (a) na (b) lakini nilikuwa napendekeza kama kilivyokuwepo katika 109 Adhabu ya Kubaka lakini 110 kuna Adhabu ya Kubaka kwa Kundi na 111 kuna Kujaribu Kubaka. Kwahiyo, Mhe. Naibu Spika napendekeza sana kwa Mhe. Waziri waongeze kifungu chengine katika 113 baada ya (a) (b) iwe na (c) na *marginal note*

isomeke Kujaribu Kutorosha kwa Mtoto wa Kiume na Wakike na kisomeke:

"Mtu yoyote ambaye anajaribu kutorosha mtoto wa kike au wakiume atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungu kwa kipindi kisichopungua miaka ishirini kama kilivyo katika Kujaribu Kubaka".

Mhe. Naibu Spika, kwa nini nasema hivi, kwa sababu nataka kiengezwe hivi kionekane kabisa japokuwa katika mswada huu kuna adhabu za jumla ambazo zimo, lakini ilipendekeza kiwepo hiki kifungu kama kilivyokuwepo katoka jaribio la kubaka na hapa kifungu hiki kiwepo kionekane dhahiri shahiri.

Mhe. Naibu Spika, matokeo ni mengi ambayo watoto wanajaribiwa kutoroshwa na tunaona pengine hata hospitali watu wanaingia wanatorosha watoto lakini pia hata maeneo ya bandarini na *airport* kesi tofauti tofauti zipo. Kwa maana hiyo, kifungu hiki kikiwepo hapa kitakuwa tayari kinaonesha wazi wazi hata kama huko kwengine kipo lakini hiki kitakuwa kinaonesha na adhabu yake iwepo ya hili jaribio la kutosha watoto. Mhe. Naibu Spika nadhani Mhe. Waziri na watendaji wake wote na wanasheria wataona inafaa kukiweka hiki kifungu, ili hii sheria iweze kufanya kazi kwa umakini.

Mhe. Naibu Spika, twenda katika kifungu cha 222 naomba nipate ufafanuzi kwasababu kifungu hiki kuhusu uondoshaji wa viungo vya binadamu, Mhe. Naibu Spika naomba kunukuu.

Kifungu cha 222 (a) na (b) vinaeleza hivi:-

a) Anaondosha kiungo cha binadamu katika mwili wa mtu ikiwa mtu huyu yupo hai au amekufa bila ya idhini ya mtu huyu au idhini ya mtu wa karibu wa mtu aliyekufa.

b) Anaondosha kiungo cha binadamu katika mwili wa mtoto au bila ya idhini ya mzee, mlezi au mtu wa karibu wa mtoto huyo atakuwa ametenda kosa na atapewa adhabu ya kifungu kwa kipindi cha miaka ishirini.

Mhe. Naibu Spika, wasiwasi wangu uko hapa namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho anipe ufafanuzi, ili nielewe kwa sababu inawezekana huyo mlezi au mzazi anaweza akatenda hilo kosa anaweza akatoa idhini lakini ana makusudio ya kutenda kosa labda jee, ikitokea kama hivi itakuwaje na sheria hii itamkamata wapi yule mzazi atakayetoa idhini kwa vile hii sheria tayari imempa mamlaka ya kutoa idhini, lakini anatowa idhini ya kutenda kosa pengine anataka atowe kiungo cha mwanawe kwasababu tofauti lakini sheria inampa idhini. Kwahiyo, Mhe. Naibu Spika naomba Mhe. Waziri atakapokuja anielekeza au aniambie labda ikitokezea sheria hii huyu mzazi au mlezi itamkamata wapi.

Mhe. Naibu Spika, tuje katika kifungu cha 309 kinachohusu kupokea mali iliyoibiwa na iliyopatikana isivyo halali. Mhe. Naibu Spika, kifungu hiki cha 309 kimeeleza na kifungu kidogo cha 2 kimeeleza mtu na kifungu cha 3 pia kimeeleza hayo makosa ya kupokea mali iliyoibiwa na iliyopatikana.

Mhe. Naibu Spika, hapa naomba nipendekeze kwamba sheria hii haikumuonesha yule mtu anayeuziwa ile mali ya wizi. Kwahiyo, Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri tuongeze kifungu chengine cha nne kuwa:

"Mtu yeyote anayenunua mali ya wizi atakuwa ametenda kosa na atapewa adhabu ya kifungu kwa kipindi kisichozidi miaka miwili".

Napendeza hivyo Mhe. Naibu Spika, kwa sababu bila ya kuwepo mnunuzi wa vile vitu vilivyoibiwa nadhani itakuwa hao wanaoiba hawana pale pa kupeleka vile vitu wanavyoviiba, lakini kama tutamuachia hii sheria imguse tu yule aliyeiba yule mnunuzi wa vitu vya wizi haonekani hapa basi sifikiri kama tutakuwa tumetenda haki. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nchi yetu Zanzibar na sote tunajua kuwa kuna mawimbi makubwa tu ya vitu vya wizi na wanaopelekewa ni watu na wanavinunua. Vilevile, isitoshe katika suala hilo hilo la wizi kuna watoto wetu ambao wameathirika na madawa ya kulevya na adhari hiyo inawapelekea mpaka kuingia katika vitendo vya wizi na wakiingia katika vitendo vya wizi wanaipa aidha ndani majumbani kwao na wana uhakika kile kitu wanakiiba anakiuza na anakiuza kwa mtu, kwa maana hiyo anajua nikienda kuvunja sehemu au nikiipa pahala fulani kuna eneo ambalo nikipeleka kitu changu kitanunuliwa hata kama cha wizi. Kutokana na hali hiyo, naomba sana Mhe. Naibu Spika nimuombe sana Mhe. Waziri na hili walizingatie ili hiki kifungu cha kumshika huyu anayenunua vitu vya wizi.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa sina mengi ya kuchangia ila nichukuwe nafasi hii pia kuwapongeza sana Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kwa sababu mambo yote wameyaona na wameyafanyia kazi na bahati nzuri wizara au serikali imeyakubali mapendekezo yake, ili kwa kurekebisha sheria hii na ifanye kazi kwa ufanisi.

Vilevile, Mhe. Naibu Spika, naomba sana serikali yetu na nawaomba watendaji wakuu wa Mahkama na sehemu zote zinazohusika watakazotumia hizi sheria, basi wawe makini kwa kufuata sheria ili kila mtu apate haki yake kwa mujibu wa sheria hii tutakayoipitisha siku hizi chache hapa ndani ya Baraza la Wawakilishi. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, mchangiaji anayefuata ni Mhe. Tatu Mohamed Ussi, na baadaye atafuatia Mhe. Omar Seif Abeid na ajitayarishe Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini.

Mhe. Tatu Mohammed Ussi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ili nichangie Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Adhabu.

Mhe. Naibu Spika, nianze kuungana na wenzangu kwa kumuunga mkono Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuona kuna haja ya kutuletea mswada huu, ili tuujadili kwa maslahi ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, moja kwa moja nakwenda kwenye mchango wangu ambao utakuwa katika ukurasa wa 311, kifungu Nam.119, naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

Ukurasa wa 311 kifungu cha 119 kinachozungumzia kuhusu "mwenye nyumba kuruhusu mtoto wa kiume kunajisiwa".

Mhe. Naibu Spika, kwanza niungane na maoni ya kamati jinsi walivyoeleza kwamba adhabu iliyowekwa hapa inaonekana kuwa ni ndogo. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu kitendo hiki cha mtu kumuweka mtoto wa kiume ndani ya nyumba, ni kitendo kibaya na kumdhalilisha mtoto. Kitendo hiki kimekuwa sawa sawa na kile cha kumdhalilisha mtoto wa kike. Sasa kumuweka mtoto wa kiume akanajisiwa ndani ya nyumba kwa hivyo ni kitendo cha udhalilishaji. Hivyo, kutokana na adhabu iliyokuwa hapa ya miaka mitano naona kuna haja adhabu hii iongezewe kwa sababu nahisi ni ndogo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile mchango wangu mwengine unakwenda kwenye sehemu ya kumi na nne, ukurasa wa 320, kifungu Nam.151, kupuuza kutoa chakula kwa mtoto au mtu mwenye ulemavu atakuwa ni mkosa.

Mhe. Naibu Spika, kifungu hiki kwanza nilipokiangalia sijaona ni adhabu gani kwa mtu ambaye atafanya kosa hili na adhabu gani atapewa. Kwa hivyo, nilikuwa naomba baadae nijuilishwe ni adhabu gani ambayo atapewa kwasababu Mhe. Naibu Spika kupuuza kumlea mtoto na ikiwa mtu ana uwezo ni tatizo kubwa na ambalo linatuathiri hasa sisi akinamama.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu kuna baadhi ya wazee akina baba, sio wote lakini kuna baadhi ya akinababa suala hili wanakuwa wanalipuuza makusudi wanaacha watoto wanazubaa mitaani, pengine mtoto kamuachia kwa mama yake lakini yeye hashughuliki kuhusu mambo ya chakula, mambo ya mavazi wala mambo ya elimu. Hili linatuathiri sana sisi akina mama kwa sababu sisi ndio tunaokaa na watoto zaidi. Kwahiyo, Mhe. Naibu Spika, kutokana na kifungu hiki naomba nacho mtu akipuuza aekewe adhabu na yeye kama wanavyowekewa adhabu wengine. Kuna akinababa wengine wanapuuza kuwapa chakula watoto wao na kuwashughulikia na hatimae ndio tukakuta watoto wengi mitaani wanazubaa kutokana na kukosa huduma za wazee wao ambao wengine wana uwezo.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nakuja kwenye sura ya kumi na sita, ukurasa wa 334, kifungu Nam.197 kinazungumzia kuhusu kwa yule mtu ambaye wale ambao wanaoshawishi au wanaosaidia mtu kujiua. Mhe. Naibu Spika, kifungu hiki kimempa adhabu huyu anayeshawishi au anayemfanya mtu kumtia maneno ili ajiue pengine kwa sababu zilizokuwa na msingi.

Mhe. Naibu Spika, lakini nikiteremka katika kifungu cha 394 ukurasa huo huo, huyu mtu anayejaribu kujiua naona sikuona adhabu aliyowekewa. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu wengine wanajaribu kujiua pengine kwa makosa, wengine wanajaribu kujiua lakini hawawahi kujiua pengine akabahatika asijue. Sasa hapa kama anajaribu kujiua kwa nini asiwekewe adhabu na yeye ikiwa hakuwahi kujiua ambayo ikamfanya aache kuidhulumu ile nafsi.

Mhe. Naibu Spika, hapa nilikuwa naomba napo huyo anayejaribu kujiua na ikawa hakuwahi kujiua, basi na yeye apewe adhabu kwa sababu naona wale wanaoshawishi wamepewa kifungo cha maisha. Sasa yeye je huyu anayetaka kuidhulumu nafsi? Kwahivyo, naomba hapa Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja anipatie ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye ukurasa wa 334 kuhusu kuharibu au kumficha mtoto au kumuua mtoto. Kwa kweli, Mhe. Naibu Spika, tumekuwa tukishuhudia matokeo mengi ya watu wanaojifungua kuwatupa watoto au wengine kuwaua au kuwaficha na mara nyingi watoto wanaokotwa kotwa hasa katika kipindi hiki. Sasa nilikuwa najiuliza hii sheria ya kumtupa mtoto au ni wangapi ambao wamewahi kuwatupa watoto au kuwaua na wakapewa hatia hii ya kifungo, kwasababu siku zote tunasikia ndani ya redio leo mtoto kaokotwa, leo mtoto kafanyaje lakini bado sheria hii inaonekana haifanyi kazi vizuri, kama ipo basi haifanyi kazi vizuri. Kwahivyo, Mhe. Naibu Spika, tunaomba sheria hii nayo iangaliwe vizuri kwasababu wimbi la utupaji wa watoto umekuwa mkubwa hususan siku hizi.

Mhe. Naibu Spika, sina mengi isipokuwa naomba tu hapa tunakuwa tunatunga sheria na hii sheria tunayoitunga ni sheria ya adhabu, na tuliomba kama alivyozungumza Mhe. Mwanaasha Khamis Juma kwamba alileta Hoja kuhuusu masuala ya

Udhalilishaji, lakini tukaona sheria zile pengine hazifanyi kazi. Kutokana na hali hiyo, sasa tunaomba kutunga ni jambo moja na sheria kufuatwa ni jambo jengine.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo machache naunga mkono hoja asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Tatu Mohamed Ussi, mchangiaji anayefuata ni Mhe. Omar Seif Abeid na baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini na atafuata Mhe. Mussa Foum Mussa.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi jioni ya leo kuchangia mswada huu muhimu ambao ni mswada wenye kuhitaji kuufanyia kazi sana. Lakini kabla ya kuendelea kama hakutakuwa na mambo ambayo yataniridhisha nitatamka wazi kwamba sitauunga mkono mswada huu. Kwakweli, kuna mambo kadhaa ambayo nimeyaona ambayo yanahitaji marekebisho mengi. Kwahiyo, katika mswada huu naomba tupate ufafanuzi wa kina na marekebisho ambayo ni mambo yanayogusa maisha ya wanadamu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tunatunga mswada leo, mswada ambao ni mgumu unagusa maisha ya watu wote ya kizazi cha muda mrefu. Kwahiyo, natoa nasaha kwa wenzangu katika kuupitia mswada huu wakati wa kuchangia kwetu ni vyema tukachukua muda na Mhe. Naibu Spika nakuomba kwa wale wenye uwezo wa kuchangia waongezwe muda ili wapate kuchangia kwa kina. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naanza katika kifungu cha 3, tafsiri ya neno “mwanamme” halafu nakwenda kwenye ukurasa wa 277 mambo ya uzembe.

Mhe. Naibu Spika, tumeona kuna baadhi ya mambo ambayo yapo yanayosababishwa na uzembe, kwenye kifungu cha 8(1). Mhe. Naibu Spika, tumeshuhudia ajali nyingi zikitokea ambazo zinasababishwa na uzembe wa barabarani unaofanywa kwa makusudi na madereva, lakini hapa inaonekana kwamba sheria hii haijaiangalia kwa kina suala la uzembe. Sasa bila ya kuathiri masharti yaliyotajwa na sheria hii kuhusiana na vitendo vitakavyofanywa na kuacha kufanywa kwa uzembe. Naomba kusema kwamba:

"Mtu hatowajibika kwa kosa la jinai kwa kufanya au kuacha kufanya kitendo ambacho kimetokea bila ya idhini yake, au tukio lilotokea kwa bahati mbaya".

Mhe. Naibu Spika, leo madereva wamekuwa wakiendesha gari kwa *speed* kubwa wanawaua watu ikisha mtu huyo anashtakiwa kwa kosa la kuua bila ya kukusudia au hapa limeingia neno la uzembe, yule uliyemua hatima yake tumeiweka wapi? Kwahiyo, naona suala la uzembe hapa liondolewe hasa, suala la uzembe akisababisha ajali itakayo-*cost* maisha ya watu ahesabiwe na yeye kwenye kosa la uuaji, kwasababu tusiangalie upande mmoja tu, tumuangalie yule mtu tumeshamuua maisha yake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikienda katika kifungu cha 10 kuchukuliwa kwa akili timamu. Hili neno linajirejea rejea hivyo naomba pawekwe sawa.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 12 kutenda kosa ikiwa umeelewa, kinasema.

"Isipokuwa kama ilivyoelezwa katika kifungu hiki kulewa hakutachukuliwa kuwa ni utetezi katika kosa lolote la jinai".

Kifungu kidogo kinasema.

"Kulewa kutakubaliwa kuwa ni utetezi kwa shtaka lolote la jinai, iwapo tu kwa sababu ya kulewa huko, mtu anayeshtakiwa wakati wa kutenda au kuacha kutenda kosa analoshtakiwa alikuwa hatambui kutenda huko au kuacha kutenda ni kosa au alikuwa hatambui alitendalo".

Mhe. Naibu Spika, ulevi ni starehe wewe si unakwenda kulewa kwa starehe, wengine wanalewa kwa kunuia kufanya makosa. Kwa hiyo, ikiwa umetenda kosa, ikiwa umelewa ihesabiwe kama umetenda kosa, umelewa au umetenda kosa, hukulewa yote ni sawa kwa sababu wewe yule uliyemfanyia makosa umeshamuathari. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, suala la kuwa umelewa lisichukuliwe kwa njia yoyote, yote iwe ni kosa tu kama umetenda kosa ukiwa umelewa au hujalewa.

Mhe. Naibu Spika, tukienda katika kifungu cha 17 tukitizame, naomba kukinakili tena.

"Katika kutumia haki ya kujilinda mwenyewe au kulinda mtu".

Mhe. Naibu Spika, hapa kuna uwezo wa kutumia matumizi ya nguvu katika kujilinda. Kwa maana hiyo, lazima tukubali kwamba mtu anapokusudia kufanya kitendo kama cha ujambazi pale tayari yeye damu yake imeshamcheka lolote anaweza akalifanya kwa mtu. Sasa kama tukisema kutumia nguvu ya kujilinda kutumia nguvu kupindukia tukawazuia tutakuja watia hatiani au tutakuja waweka makosa askari wetu wanapopambana na majambazi. Jambo hili naomba parekebishwe hapa, ili askari wakati wa kutekeleza kazi zao kifungu hiki kiweze kuwalinda, kwamba itakapobidi askari kutumia nguvu katika kujilinda kwao waweze kutumia silaha kwa kujinusuru wao au mali wanazozilinda. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tukienda katika kifungu cha 24 hapa nasikitika na matumizi ya lugha zilizotumika katika miswada hii. Kuna maneno yameandikwa haijalishi. Kweli Mhe. Naibu Spika, nikuulize sisi Waswahili tuliomo humu ndani sote tumeshindwa kuandika neno mpaka tulete mswada uliondikwa neno haijalishi, hakuna tafsiri ya neno jengine bila ya kuandika neno haijalishi. Kwakweli, naona hili si neno, neno hili kusema kwamba haijalishi si neno la kulitumia lirekebishwe neno hili au liondolewe kabisa. Yamo maneno pale yanayotaja bila ya kujali, basi lile neno bila ya kujali litumike na neno haijalishi ambayo ime-*appear* sehemu nyingi napendekeza yaondolewe.

Mhe. Naibu Spika, sasa naingia katika kifungu cha 108. Kifungu hiki kimezungumzwa kwa mapana na watu wengi, lakini na mimi napendelea kuongeza msisitizo katika suala hili. Mhe. Naibu Spika, kubaka ni tatizo sote tunakubaliana kama kubaka ni tatizo na ni jambo ambalo halipendezi kwa sisi tu hata kwa Mwenyezi Mungu wetu aliyetuumba analichukia. Lakini, jambo moja ambalo napenda niliombe, kwamba adhabu za kubaka zipangwe kwa mujibu wa umri wa wahusika.

Kama ilivyopangwa umri wa miaka kumi na mbili kwamba hatahesabiwa kufanyiwa kosa na haya ya kubaka kwa vijana wale ambao wako kwenye *hot age*, mimi napendekeza kwamba yapangiwe adhabu tofauti. Sisemi kwamba wasiadhibiwe, waadhibiwe lakini adhabu zao zisiwe sawa na watu wenye umri wa kuanzia miaka 25, 30 kwa sababu hapa umri wa miaka 18 kambaka mtoto wa miaka 17, hawa ni watu ambao tayari wanalingana umri na vijana wetu wa leo. Hawa hata kama itakavyokuwa tukimfunga huyu miaka 30 kwa sababu ameshafika miaka 18 tumtizame maisha yake yote tumeyamaliza, tumemmalizia maisha anatoka gerezani akiwa na miaka 48 atalisaidia nini taifa hili, hana kitu cha kukisaidia tena taifa.

Kwahiyo, adhabu za kubaka kwa vijana mimi napendekeza zilingane na umri.

Mhe. Naibu Spika, twende katika kifungu cha 109 adhabu za kubaka. Hii kama nilivyosema kwamba itumike kwa watu ambao umri wao ni mahsusi. Mhe. Naibu Spika, lakini pia nilikuwa nimeiona nguvu katika mswada huu ambao wamepewa Mahakimu. Napenda nirudi tena kidogo kwenye 14 pale ambapo inasema kwamba afisa wa Mahkama hatoajibika kijinai. Suala la kusema kwamba Afisa wa Mahkama kwamba hatawajibika kijinai, hapa sisi si kwamba tunampenda, hapa tunamuumiza kwasababu kuna watu wakijua kwamba mimi siwezi kushtakiwa kwa jinai wala sitafanya jambo lolote kijinai anaweza akatenda makosa anavyotaka yeye.

Hapa itakuwa sheria hii haijatenda haki, ili haki itendeke kama wanavyosema wenyewe na ionekane kama imetendeka kila mtu awajibike kwa kosa atakalolifanya, awe ni hakimu, awe ni karani, awe ni mwakilishi awe ni waziri, awe ni nani. Hapa kusiwekwe kipengele cha hakimu kumlinda au Afisa wa Mahkama kumlinda watu wote wawajibike kijinai atakapotenda kosa la jinai. Haya ndio mapendekezo ambayo mimi nilikuwa nataka niyaingize katika mswada huu.

Pia kuna neno katika kifungu cha 24 nimerudi tena, maana yake niliogopa lile kuja kuambiwa muda umekwisha ndio nikaenda kule. Kuna neno limeandikwa 'almuradi'. Almuradi hili neno la Kiarabu, hivi sisi jamani nauliza tena, sisi Waswahili hatuna maneno ya kutafsiri? Pale neno 'almuradi' sio pahala pake, hawa watunga sheria ambao wana maneno tele ya kuyatumia mimi napendekeza maneno kama haya yasiingizwe humu, yasiingizwe kwenye sheria zetu yawekwe maneno ya Kiswahili kwa Kiswahili, kwasababu tunayekwenda kumpa sheria hii ni Mswahili.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Omar Seif Abeid muda wako umekwisha, malizia.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, basi la mwisho nilikuwa napenda kuzungumzia suala la usafirishaji wa binadamu ambalo limezungumzwa katika kifungu cha 153. Pia katika kifungu kile tuingize kifungu ambacho kitawalinda watu wanaowasafirisha watoto wao hasa wanaume. Kuna baadhi ya kesi tumezikuta wanaume wanawatorosha watoto wao baada ya kuachana na mwanamke. Mwanamke anakuwa anapata tabu ya kulea baadae mwanamme anamchukua anamuhamisha.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Omar Seif Abeid, kaa chini.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, mimi nitaunga mkono pale nitakapopewa majibu ya masuala yangu. Ahasante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Omar Seif Abeid. Sasa mchangiaji anayefuata ni Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini na baadaye atafuata Mhe. Mussa Foum Mussa na baada ya hapo atafuata Mhe. Hidaya Ali Makame.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na mimi kunipatia nafasi kuchangia machache katika hotuba hii au katika mswada huu muhimu wa Mhe. Waziri wa (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Maalim Haroun Ali Suleiman). Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Adhabu, Kutunga Sheria Mpya ya Adhabu, Kuweka Masharti Bora zaidi pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwakweli, hii

sheria ni muhimu sana Mhe. Waziri, katika suala zima la utawala bora kwenye nchi yetu. Tunapozungumza misingi ya utawala bora tunazungumza suala la uajibikaji, suala la uwazi, suala la ushirikishwaji na suala la utawala wa sheria. Sasa Mhe. Naibu Spika, naomba nitilie mkazo sana hili suala la utawala wa sheria (*the rule of law*).

Mhe. Naibu Spika, nchi yoyote ikiwa hakuna utawala wa sheria na kutoa adhabu kwa kweli taifa lake litakuwa haliendi ipasavyo na matokeo yake kila mmoja anafanya anavyotaka yeye, anavyoona inampitikia na daima maendeleo ya nchi hayatapatikana. Lakini naomba nimshukuru sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kutilia mkazo suala zima la utawala bora. Misingi yote ya utawala bora hasa suala hili la utawala wa sheria ni muhimu sana.

Mhe. Naibu Spika, hivi majuzi Mhe. Rais alifungua Mahakama pale Mwanakwerekwe, alipofungua jengo lile la Mahakama alitoa hotuba nzito sana yenye maadili na sheria hii. Naomba ninukuu kidogo baadhi ya vipengele na nawashukuru sana Zanziabr Leo wamem-*quote* kama alivyozungumza, wanasema "Dkt. Ali Mohamed Shein, "Mahakimu, Majaji, fanyeni kazi kwa weledi". Wakaendelea kusema, "Dkt. Shein akemea rushwa, akerwa na ucheleweshaji wa kesi".

Mhe. Naibu Spika, alihimiza watendaji hao kutekeleza wajibu wa kusimamia utawala wa sheria, kwani ndio msingi imara wa kutenda haki. Huyu ni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi yeye ndiye kiongozi wetu na anaesimamia muhimili mmoja wa sheria, lakini pia anausimamia muhimili mwengine huo wa Mahakama ambao haidhuru kuna mtu mwengine kwa mujibu wa katiba yetu.

Mhe. Naibu Spika, haitoshi, nam-*quote* Mrajis Mkuu tena. Juzi tu Ndugu Issaya Kayange, yeye naye katika harakati zile za wiki ya sheria naomba nim-*quote* Mheshimiwa naomba radhi, alisema: "Nawaomba wadau wa sheria wakiwemo Polisi, Mahakama, *DPP* na Chuo cha Mafunzo kuhakikisha kila mmoja anafanya kazi kwa mujibu wa sheria".

Mhe. Naibu Spika, haya yametokea juzi tu, sasa inaonesha nini? Mheshimiwa inaonesha kweli kuna mmong'onyoko wa maadili na ukosefu wa kufuata sheria katika vyombo vyetu vya Mahakama. Kiongozi wa nchi amezungumza haya na Mrajis mwenyewe mwenye Mahakama amezungumza haya. Sasa lazima tujitathmini, ningemuomba sana Mhe. Jaji Mkuu, ningemuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu tujitathmini hii hali sio nzuri tungoje mpaka *head of state* azungumze, angurume tena kwenye siku ya sheria kidogo haipendezi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kinachogomba zaidi mimi najiuliza, hivi wahasibu wao wanafuatiliwa na kutizamwa utendaji wao na *CAG*, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Yeye wale anawapitia wanatizama *surprise check*. Kuna taasisi nyengine nao wana utaratibu kama huo, hivi kwenye Mahakama kuna chombo gani cha kuwasimamia Majaji utendaji wao? Nani anafuatilia hili suala alilolizungumza Mhe. Rais ucheleweshaji wa kesi, rushwa, kuna chombo gani ambacho kinawafuatilia hawa Majaji kuona kwamba kweli wanayofanya si halali?

Mhe. Naibu Spika, sisemi wote, wako wengi wazuri tu wanatusaidia na wanatenda vyema, lakini kuna wachache ambao hee, nitumie neno la kizungu *very a notorious* wanajulikana, ndio nchi yetu ndogo tu wanajulikana. Tena watoto wa mjini wanakwambia Ah! Wewe unapelekwa kwa jaji gani aa! Huko utakwama twende huku bwana, huku utapenya halafu siku ya pili

yuko mjini anadunda tu anakucheka wewe. Hayo ndio mambo ya mitaani Mhe. Naibu Spika, ninayokupa.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi naomba sana, namuomba sana Mhe. Waziri tunapozingatia utawala bora lazima tutafute *better mechanism* kuhakikisha na Majaji nao wanafuatiliwa, wanasimamiwa, wanakosolewa. Hili ni suala la msingi sana.

Sheria hii Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana *DPP* kwa hili gazeti lake la Mkurugenzi wa Mashtaka Toleo la Kumi na Mbili ametoa *article* nzuri sana inayohusu hii sheria ya adhabu ilikoanzia chimbuko lake. Tunaambiwa toka mwaka 2017 tena imetokea India huko tukaitafsiri na sisi tuka-*quote* halafu tukabadilisha tunaambiwa tokea *Cap. 22 Revise Laws of Zanzibar 1922* baadaye.

Mhe. Naibu Spika, sasa inaonesha vipi ilivyokwenda mpaka tumefikia hapa leo. Kwahivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba nitilie mkazo sana hili suala la Majaji nao kusimamiwa, kukosolewa na wao pia kuwa na utaratibu wa kuwaadhibu wale ambao wanakosea na wana-*tarnish good image* ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba niende kwenye ukurasa wa 282 kifungu cha 25. Kifungu hiki wanasema aina mbali mbali za adhabu, zimetajwa (a) mpaka (m). Naomba kuzungumzia kifungu cha k, "kuifuta au kusitisha leseni ya udereva chini ya Sheria ya Usalama Barabarani". Wamezungumza Waheshimiwa mbali mbali hapa, mtu anauwa tena unaona hasa uzembe haidhuru kakusudia, lakini alichofanya ni uzembe wake.

Juzi Maungani pale imetokea ajali mbaya sana, dereva anatoka ndani *corner* anaingia *main road* hakusimama. Sasa yule dereva yuko *main road* akamkwepa kenda kagonga *Hiace* watu wanne wamekufa masikini. Sasa dereva yule *innocent,* kakimbia lakini

hawa ndio wamekuwa *victimized*. Sasa Mhe. Naibu Spika, kitu kama hicho dereva anakamatwa ananyang'anywa leseni, kweli kauwa, kasababisha vifo vya watu wanne ananyang'anywa leseni! Haiingii akilini. *(Makofi)*

Sasa naomba kushauri Mhe. Naibu Spika, hizi adhabu zimetajwa hapa, adhabu zifuatazo zinaweza kutolewa na Mahakama, kifo, kifungo zimetajwa mpaka (m) kwenye ukurasa wa 282. Lakini nataka kumuomba Mhe. Waziri hebu tuangalie uzito wa kosa na ile adhabu inayotolewa kweli yana-*match*? Kwakweli, kuna adhabu nyengine zinatolewa haihalisi lile kosa, kosa analiona kubwa lakini adhabu ndogo.

Kutokana na hali hiyo, naomba *Judiciary* yetu i-*review* kidogo hizi adhabu zinazotolewa nyengine kweli zinauma, siku ya pili unamuona mtu analipa faini unaambiwa kauwa au mtu kasababisha ajali mtu kakatika mguu yeye anaambiwa faini shilingi laki tano au milioni mbili, shilingi milioni mbili mwenzako keshautupa mguu kidogo inauma. Kwahiyo, ningeomba sana hili tulipitie tulitizame uzito wa kosa na adhabu inayotolewa, sikatai sisi wengine sio wanasheria hatujui lakini angalau ni *common sense* tu, tuangalie tu inahalisi?

Mhe. Naibu Spika, jengine nililonalo kwenye ukurasa wa 330, haraka haraka namaliza sina vingi kidogo tu, sasa hivi adhabu ya kuuwa kwa makusudi. Nimezungumza kidogo lakini nasema adhabu ya kuuwa kwa kukusudia, "Mtu yeyote ambaye ametiwa hatiani kwa kosa la kuua kwa kukusudia atapewa adhabu ya kifo". *Fine*, sasa adhabu ishatolewa kwamba yule auwawe na yeye anyongwe. Sasa Mhe. Rais ndio wa mwisho yeye kwa busara zake anaangalia kweli iko haja auliwe na yeye au isiwepo au abaki afungwe maisha? Lakini sasa sheria imesema atapewa adhabu ya kifo.

Mhe. Naibu Spika, ningemuomba sana Mhe. Waziri nilikuwa nahisi tu labda iwe *open* zaidi isiwe kama hivi *vague*, kwasababu kuna mtu hapa ambaye na yeye anawajibika kuidhinisha adhabu ya kifo. Sasa labda angei-*qualify* zaidi kwamba ah! *Subject to confirmation* kwa kiongozi wa nchi, nahisi kwa maoni yangu kwasababu hapa ishasema adhabu iweko. Sasa kama haikutekelezwa tumkamate nani, maana swali ndio hilo tu hapa ilivyo iko *open*, atapewa adhabu ya kifo sasa haikutekelezwa tumkamate nani? Sasa nilikuwa nataka busara zake tu Mhe. Waziri kui-*qualify* zaidi nahisi iwe *better qualified* hii sentensi, kidogo naona kama iko *vague*. Tunaamini kwamba kiongozi wa nchi ana busara zake, ana hatima yake, lakini hii sheria kuiacha hivi ilivyo kwa maoni yangu nahisi kidogo haiko *open*.

Mhe. Naibu Spika, sina mengi mswada ni mzuri sana, tukijitahidi kuusimamia sote kwa pamoja naamini utatuweka pazuri. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono pamoja na marekebisho yake kwa asilimia moja mswada huu. Nakushukuru sana ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame, mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Mussa Foum Mussa na baadae atafuata Mhe. Hidaya Ali Makame na ajitayarishe Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa ruhusa ya kuchangia mswada huu tulionao.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niupongeze huu mswada, kwasababu mswada huu una mambo mengi ambayo yametuzunguuka katika maisha yetu ya kila siku. Kwahivyo, nawaomba Waheshimiwa wote huu mswada tuunge mkono, tuchangie na baadaye tuupitishe, ili uendelee kufanya kazi.

Mhe. Naibu Spika, huu mswada kuna mambo mengine lazima atuwekee waziwazi, ili utakapoanza kutumika utumike katika hali iliyokuwa nzuri.

Mhe. Naibu Spika, na mimi vile vile nataka kuchangia na kwanza nitaanza ukurasa wa 280 kifungu cha 17(1) yaani, kinaeleza matumizi ya nguvu katika kujilinda. Mhe. Naibu Spika, naomba nikinukuu hiki kifungu ili nipate kuelezea vizuri.

Kifungu 17(1) kinasema kwamba:

"Katika kutumia haki ya kujilinda mwenyewe au kumlinda mtu mwengine au kulinda mali, mtu atatakiwa tu kutumia nguvu za kiasi zinazohitajika katika ulinzi huo".

Kifungu 17(2) inasema:

"Mtu atawajibika kijinai kwa kosa lolote linalotokana na matumizi ya nguvu kupita kiasi katika kujilinda au katika kumlinda mtu mwengine au katika kulinda mali".

Mhe. Naibu Spika, kwanza nipongeze huu mswada kwa kukileta kifungu hiki cha mtu kujilina. Lakini nataka niseme kwamba, kwa mfano mtu anapokuja kukuibia mali yako au anapoingia katika nyumba yako na wakati huo huo anaingia na panga pale anakusudia kwamba chochote kinaweza kikatokea kwa yule mwenye nyumba au mwenye kulinda. Sasa mimi naambiwa nisitumie nguvu za ziada ili kujilinda, sasa je, mimi nitakapokuwa sikutumia nguvu akaniwahi yeye kuniuwa hapo sitakuwa mimi nimefanya uzembe?

Sasa kifungu cha 17(3) kinasema:

"Mtu yeyote atakayesababisha kifo cha mtu mwengine kutokana na matumizi ya nguvu kupita kiasi katika kujilinda, atakuwa ametenda kosa na kuua bila kukusudia".

Mhe. Naibu Spika, mimi hapa kidogo nina matatizo na nataka Mhe. Waziri atakapokuja aniweke wazi ili tufahamike vizuri. Kwa mfano, tumesikia watu wengi wanaolinda kwenye vituo vya mafuta walikwenda waibaji wakawauwa. Sasa, kwa mfano mimi nipo pale nishaona yule mwinzi anayekuja kwa hali yoyote ikiwa sikumuwahi kumuuwa ataniuwa mimi je mimi nitakapofanya iwe nimefanya kosa ambalo la kuuwa bila ya kukusudia? Ata, kwahivyo nadhani hiki kifungu kirekebishwe kwamba mtu atakuwa na haki ya kujilinda wakati atakapoona mwinzi au mtu yeyote atamuwahi yeye kumuuwa basi yeye ndio awahi kuuwa. Hata Sheria yetu ya Kiisilamu inazungumza hivyo.

Kwa mfano, mtu ukimuona yule ikiwa sikumuwahi kumuua yeye ataniua mimi basi sheria inakuruhusu ya Kiisilamu uanze wewe kumuua ndio kujilinda, lakini hapa imewekwa hii haki lakini haikuwekwa vizuri kwa hisia zangu mimi. Kwahivyo, lazima mtu kwa vile kapewa haki ya kujilinda basi aangalie mtu amekuja vipi. Tumeona watu wamepigwa, wamefungwa, wamekwenda kulazwa hospitali kwa kuumizwa na wezi. Sasa yeye anaambiwa asijetumia nguvu za ziada, aa hapa Mhe. Naibu Spika, hiki kifungu kidogo utoe uwazi kwa vile kimetoa ruhusa mtu apewe ruhusa ya kujilinda kwa hali yoyote atakayotumia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo vile vile niende katika ukurasa wa 282 unaozungumza Sura ya Tano "Adhabu", yaani kifungu cha 25. Hapa pamezungumzwa adhabu nyingi, adhabu zitakazoweza kutolewa na Mahakama, zimezungumzwa nyingi hapa, adhabu ya kifo, kifungo, kutumikia jamii, faini nyingi tu zimezungumzwa. Lakini nataka ku-*deal* kidogo na hii adhabu ya kifo yaani mtu kunyongwa.

Mhe. Naibu Spika, hii adhabu imewekwa hapa lakini kwa mawazo yangu mimi hii adhabu inawekwa lakini hatuwezi kuitumia, sasa tunakiweka kitu ambacho hatuwezi kukitumia kina maana gani kukiweka. Sasa mimi nawazo yangu hapa baada ya kifo kiwe kifungo cha maisha. Kwasababu hii adhabu inawekwa na toka tupate uhuru mwaka 1964 mpaka hii leo hatujasikia mtu kunyongwa na adhabu za vifo vinatolewa. Sasa nadhani tuangalie kwamba hivi sasa nchi nyingi adhabu hii ya kifo imeondolewa. Kwahivyo, na sisi hatuna sababu kuendelea nao na kwa vile hatuwezi kuitumia. *(Makofi)*

Halafu vile vile tumeweza kuiondoa adhabu ya mikwaju eeh! Bakora tumeiondoa kwasababu ya kwamba dunia nzima imeondolewa. Sasa leo tu bado tunaendelea na adhabu ambayo kuwa hatuwezi kuitekeleza. Nadhani hii hakuna haja na vile vile mtu anaweza kuhukumiwa kifo akanyongwa lakini wakati huo huo atakapokata rufaa ya Mahakama ya Rufaa mtu yule inawezekana sababu ile aliyohukumiwa pale ikathibitisha kwamba ile kosa hakufanya na huku keshanyongwa. Sasa hiyo nadhani hiki kipengele iko haja kwa wakati tulionao hivi sasa hukumu hii ya kifo kuondolewa imepitwa na wakati kwa sababu twende na wakati na dunia inavyoenda. Tumeweza kuondoa bakora tusije weza kuondoa kifo ambacho kuwa hatuwezi hata tukikiweka hatuwezi tukakihukumu.

Kwakweli, kwanza nawapongeza maraisi wote waliokaa Zanzibar kwamba hukumu hiyo bado hawajaweza kuitekeleza wanai-*revue* kwamba mtu aendelee kufungwa kifungo cha maisha. Sasa nadhani ni vyema kuiondoa na sisi tukahesabika katika ulimwengu kwamba Zanzibaar hukumu ya kifo na wao wameiondoa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo vile vile niende ukurasa wa 217 kifungu cha 136 kinachozungumzia matendo ya usagaji. Mhe.

Naibu Spika, kwanza naomba nikisome hichi kifungu cha 136 kinasema:

"Mwanamke au mtoto wa kike ambaye atatenda tendo la usagaji na mwanamke mwengine au mtoto wa kike mwengine ama mfanyaji au mfanywaji atakuwa ni mkosa na akatiwa atiani atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka kumi."

Mhe. Naibu Spika, nadhani sote tunaelewa kwamba matendo haya ya usagaji katika nchi yetu yanaongezeka. Sasa kwanza nataka niseme hii adhabu iliyowekwa kwa hisia zangu ni ndogo sana kwasababu hili jambo Mwenyezi Mungu akutuwekea njia iliyokuwa nzuri tunatafuta njia nyengine. Sasa hii adhabu ndogo lakini napata wasi wasi kwamba hawa watu wanaofanya kitendo hichi cha mambo haya watapatikana vipi? Kwasababu mwanamme anapoenda hospitali daktari anathibitisha lile jambo. Lakini hapa daktari atathibitisha nini? (*Makofi*)

Halafu vile vile kiukweli Mhe. Naibu Spika, hili jambo zito na pia naomba kwamba hii miaka isiwe mitano ianzie miaka kumi halafu mpaka ishirini kwa sababu hili jambo likomeshwe. Siku moja nilimsikia hapa Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf alitaja mambo haya akasema niwataje? Sasa inawezekana na sisi humo tumo. Kwahivyo, hili jambo tujitahidini kulipangia sheria iliyo nzito kwa sababu leo tunapanga sheria sisi lakini kesho sisi hatumo humu watakuja wenzetu sheria msumeno.

Mhe. Naibu Spika, lakini nasema kwamba hapa ametajwa mtoto wa kike lakini katika hii adhabu na yeye ameingizwa. Lakini katika kutafsiri mtoto wa kike ni mtu mwanamke aliyechini wa umri wa miaka 18. Sasa hapa niliingia kiwewe kidogo kwamba je, mtoto aliyechini wa umri wa miaka 18 hii adhabu atapewa au vipi hapa?

Kwahivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho naomba atufafanulie kwasababu alitajwa mtoto wa kike na kwenye ufafanuzi kule mtoto wa kike ni mwanamke aliyechini wa umri wa miaka 18 na hapa pana adhabu atakapokamatwa. Je, mtoto yule adhabu hii atastahiki kupata kwasababu bado umri wake ni mdogo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo vile vile niende ukurasa wa 217 ingawaje mwenzangu Mhe. Said alikwisha lizungumza hili jambo katika kifungu cha 142. Lakini nataka niendelee kukisoma pia kifungu 242 (ii). Yeye alisoma (i) lakini mimi nasoma (ii) mtu mwanamke yoyote ambaye anaruhusu kuingiliwa kingono na mtu mwanamme yoyote ambaye anajua au ana sababu za kuamini kuwa ni mume wa mtu mwengine bila ya ridhaa au ruhusa ya mke wake atakuwa ni mkosa na vile vile kifungu hichi vle vile hapa bila ya ridhaa au ruhusa ya mke wake. Haya mambo hayapo katika malezi yetu hayapo kwa hivyo, sehemu hii ifutwe. Kwasababu mwanamke huyo atakuwa mjinga sana ataeruhusu mambo hayo. Kwahivyo, hili jambo haliko kwenye tabia zetu mila zetu, kwa mwanamme au mwanamke kutoa ruhusa hiyo. Kwa maana hiyo, nadhani haiko haja kuingiza katika sheria hii bora hiyo sehemu iondolewe kabisa iwe haipo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, vile vile niende katika ukurasa wa 318

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mussa Foum Mussa, malizia umebakiwa na dakika mbili.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mhe. Naibu Spika, namalizia kwenye kifungu cha 143 kinachozungumzia kufanya maangiliano ya kingono na maharimu zake mtu. Lakini naomba kunukuu kifungu cha 143 (6).

Kifungu cha 143 (6) na (7) vinasema hivi:-

(6) "Iwapo mtu mwanamme anajaribu kutenda kosa lolote kati ya yaliyotajwa atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka 10"

(7) "Iwapo mtu mwanamke atajaribu kutenda kosa lolote kati ya yaliyotajwa atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka 3".

Akaa! Kuna nini Mhe. Naibu Spika.

Sasa tendo la aina moja huyu mwanamme huyu mwanamke wamefanya kosa moja huyu apate miaka kumi huyu mitatu. Mhe. Naibu Spika, kwa vile hili jambo basi adhabu iwe sawa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mussa Foum Mussa, muda wako umekwisha.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja, kwasababu bado ninayo mengi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mussa Foum Mussa. Sasa mchangiaji anayefuata ni Mhe. Hidaya Ali Makame, baadaye nitampa nafasi Mhe. Dkt. Makame Ussi na atafuatiwa na Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuweza kuchangia juu ya Mswada huu wa Sheria ya Adhabu uliotujia sisi ndani ya Baraza hili ili kuweza kuyarejebisha yale ambayo tumeyapigia kelele siku nyingi, tumeyasemea siku nyingi na wenzetu waliopita pia wameyazungumzia.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nipongeze sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar kwa kuona haya mambo ndani ya nchi yetu, tayari kuna kadhia mbali mbali ambazo zinatukwanza na zinatusababishia kwenda kwenye muelekeo sio. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia niipongeze wizara kwa kusikia vilio vya wananchi lakini pia kuyaona mengi ambayo hivi sasa ni changamoto kubwa katika jamii yetu. Mswada huu umekuja wakati muafaka ijapokuwa umechelewa kidogo, lakini kwa hivi sasa pia hauko nyuma zaidi unaenda na wakati na niseme kwamba huu mswada umeacha tu baadhi ya mambo kidogo ambayo ndiyo tunayafanyia marekebisho. Lakini kwakweli mswada huu wizara inayohusika yakisimamiwa maswala haya yaliokuwemo ndani ya mswada huu unaorekebishwa hapa leo, kwakweli nchi yetu sidhani kama kutakuwa na non'gono'ngo nyengine kuhusu masuala ya udhalilishaji lakini pia na sheria za adhabu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze moja kwa moja kwenye kifungu cha 136 ukurasa wa 315. Mhe. Naibu Spika, katika mswada huu kuna sheria hii ya matendo ya usagaji. Mhe. Naibu Spika, wenzangu wameshakizungumzia kifungu hichi lakini na mimi kwa muono wangu na kutokana na hali jinsi ilivyo pia nitakizungumzia kifungu hichi kutokana na hali ilivyo Mheshimiwa kuna adhabu hapa iliyowekwa na adhabu hii si ndogo. Lakini ningeiomba sana serikali adhabu hii ikaongezwa, sababu ya kusema hivyo miaka mitano lakini isiyozidi miaka kumi, miaka mitano tunasema hapana kitu ni sawa sawa na kufumba macho na kufumbua kwa ulimwengu wa sasa hivi. Kwasababu umo ndani ya nyumba wewe unaumwa siku tatu au mwezi lakini ukitoka nje ni sawa sawa na ulieumwa siku mbili.

Sasa na huyu mtuhumiwa unemuweka ndani miaka mitano ni sawa sawa na umemuweka miaka miwili au ni mmoja na nusu. Kwahiyo, akitoka kule ana hasira zake zaidi atakuja kuyaanzisha

tena. Kwahiyo, mimi ningeiomba hapa sana serikali juu ya adhabu hii mimi nasema labda ikaekewa kiwango kwa umri wa watu tukaangalia kuanzisha umri wa miaka 18 mpaka miaka labda 35 tukawaekea adhabu hiyo ya miaka 10 mpaka 40. Lakini kuanzia miaka 50 au 38 au 40 kuendelea na huko jambo maisha wakae huko wanakuja huku kufanya nini? Kwasababu Mhe. Naibu Spika, tuangalie sheria ambayo inatugusa kisayansi lakini na sheria ambayo inatugusa kidini pia kuna dini gani inayoruhusu matendo haya? Ni sawa serikali yetu haina dini sawa lakini sisi wananchi tunazo dini.

Je, tujiulize ndani ya nafsi zetu kuna sheria gani ya dini ipi inayoruhusu masuala haya. Tukiangalia tunakuta kwamba hizi sheria hakuna kwenye dini na dini zote zinapiga vita. Lakini kwa hapa tunasimamia dini yetu ya kiislamu ndiyo mpaka Mwenyezi Mungu wetu kasema tena katuwasa hasa juu ya masuala haya.

Kwahiyo, kama mtu huyu tayari keshaonekana *live* na suala hili keshajulikana, keshabainika unamuweka ndani ya gereza au ndani ya kifungo miaka mitano huyu unamchonga makali. Mhe. Naibu Spika, naomba sana hapa hii adhabu ikaangaliwa ikafanyiwa marekebisho na ikaengezewa muda adhabu ya miaka mitano haitoshelezi kwa watu hawa.

Mhe. Naibu Spika, hili suala sasa hivi limekuwa yaani limepamba moto mpaka maskulini mpaka wanafunzi wetu tayari wameshakuwa wanachipuka na tabia hizi na tabia hizi zinachipuka kutoka na kwamba sheria ilikuwa haipo labda. Sasa hivi ishakuwepo mtu anasikia ni miaka mitano Waheshimiwa wameshaipitisha ndani ya Baraza la Wawakilishi kwakweli wataogopa lakini si dhani kama mtu ataingia ile ghofu kwa kusikia miaka mitano atakuuliza hasa miaka mitano ni nini? Kwahiyo, naomba sana Mhe. Naibu Spika, ili vitendo hivi

vikatishe visiwepo kabisa basi hii sheria iongezwe ya adhabu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nakuja kwenye kifungu cha 144 ni idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Mhe. Naibu Spika, kifungu hichi pia kinanitia wasi wasi kutokana na jinsi tulivyoelezewa. Tunafahamu kwamba ndani ya dini yetu suala la zinaa pia limepigwa vita au limekwatazwa haswa, lakini hapa tunaambiwa kwamba mashtaka kwa kosa lolote chini ya kifungu cha 142 au cha kifungu cha 143 hayatafunguliwa bila ya idhini ya maandishi ya Mkurgenzi wa Mashtaka. Kwa nini hayo mengine yafanyike bila ya kuwepo yeye hili lisifanyike mpaka idhini ya maandishi, idhini ya maandishi insaidia nini pale?. Mzinifu mwanamme au mzinifu mwanamke atakapoonekana tu ambaye tayari yumo ndani ya ndoa hukumu yake ni kuuliwa dini inavyosema sawa, hatuwezi kufanya hivyo kutokana na hali zetu zilivyo.

Lakini kwa nini hii adhabu isifanywe mpaka idhini itoke kwa Mkurugenzi tena ya maandishi ya maandishi kivipi inasaidia nini yaani? huyu Mkurugenzi kama hayupo kwa hiyo mfano hayupo miezi, miaka kwahiyo lisifanyike mpaka awepo yeye na idhini ya maandishi. Mimi sijafahamu hapa kivipi maandishi hayo yataandikwa kinamna gani huo wino utakaotumika wino upi.

Kwahiyo, hapa naomba sana na hii idhini ikaangaliwa kwasababu hili kosa lililotendeka hapa hawa watu ni watu wazima wenye akili zao na wanajua kila kitu katika dini lakini katika sheria, halafu leo unakuja kuwaandikia hapa kwa idhini ya Mkurugenzi na idhini yenyewe ya maandishi. Mhe. Naibu Spika, hapa ningehitaji ufafanuzi zaidi juu ya suala hili la idhini ya Mkurugenzi.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nije kifungu cha 86 kinazungumzia matangazo ya mali iliyoibiwa. Mtu yeyote ambaye

anatangaza hadharani kutoa zawadi kwa kurejeshewa mali yeyote ambayo imeibiwa au imepotea, mtangazaji keshatangaza kwamba yeye amepotelewa na mali yake kwa hiyo kamtangazia yule ambaye ameiokota ile mali amrejeshee. Sasa kama kaiokota mali ile halafu keshairejesha baadaye unakuja kumuwekea adhabu ya miaka miwili. Kwa maana hiyo siku hizi tukiokota tujifanyie wenyewe tu, tusipeleke, maana tena ukishapeleka kule kuna adhabu ya miaka miwili hapa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hapa sijafahamu hii sheria inasemaje kiukweli. Lakini tukiiangalia mtu ambaye kaokota mali ya mtu, keshatangaziwa ndani ya redio mtu mwenyewe yuko sehemu fulani, anakaa sehemu fulani kwa hivyo wewe unatakiwa upeleke pahali fulani. Umeiba au umeokota, umeokota na kama kuokota sio kuiba umerejesha kwa imani yako, basi uiangalie ile imani yako lakini tena kusiwe kuna adhabu ya miaka miwili huku kama mtu aliyeiba. Hapa hii adhabu iangaliwe kwa huyu mtu ambaye ameokota hakuiba. Pia kama kaiba keshatangaziwa redioni kairejesha, huyu hafai kupewa adhabu ya miaka miwili, kwa sababu hakuwa na nia nzuri.

Hata kama kairejesha, ilikuwaje mwanzo akaiba. Keshatangaziwa kasikia kuna zawadi fulani itatolewa ndio akaona aa! na mimi niende nikapeleke ili nionekane kama niliokota au sijui nilifanyaje, kwa hivyo nakwenda kuirejesha ili nionekane na mimi nina moyo. Kwa hivyo, adhabu hii mimi ningeomba sana Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri aiangalie nayo na kama kuna uwezekano wa marekebisho basi irekebishwe. Lakini kwa huyu mtu ambaye ameokota na yeye aangaliwe kwa jicho la huruma, kwa sababu hakuwa na nia mbaya, hakuwa na nia ya kuiba wala hakuwa na nia ya kutumia vibaya hii mali.

Mhe. Naibu Spika, sikuwa na mengi ya kuchangia juu ya mswada huu, lakini mengi yameshazungumzwa. Sheria iko vizuri na

adhabu zipo nyingi zitendewe haki. Tutakapozitendea haki adhabu hizi zilizokuwemo na hizo nyengine ambazo tumeshazirekebisha, nadhani kuna mengi yatakayorekebishika na mengi ambayo yatafanyiwa kazi kwa kutendewa haki wananchi wetu, lakini pia kuitendea haki nchi yetu na kuwa ya salama zaidi na amani katika kuishi na jamii zetu.

Mhe. Naibu Spika, nikimalizia hapo niseme naunga mkono hoja hii au mswada huu kwa asilimia mia moja, hapo mengine yatakapojibiwa zaidi tutazidi kuupa nguvu zaidi mswada huu kwa kushirikiana na wizara na serikali yetu kwa ujumla ili tuone nchi yetu ni jinsi gani inavyokwenda kwa hali ya usalama na amani, ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Hidaya Khamis. Mchangiaji wetu anayefuata atakuwa ni Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi, baada ya hapo ajitayarishe Mhe. Miraji Khamis Mussa. Kwa upande wa wajumbe nafikiri wachangiaji wetu wa mwisho watakuwa ni wawili, Mhe. Mussa Ali Mussa na Mhe. Hamza Hassan Juma. Mheshimiwa karibu.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi niwe mmoja kati ya wachangiaji kwenye mada hii adhimu ya marekebisho ya sheria. Kwanza kabisa Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda niipongeze serikali nzima kwa mabadiliko inayoyafanya kwa lengo la kuleta maendeleo. Moja katika mabadiliko hayo inafanya serikali ni hii hapa leo, kufanya mabadiliko ya sheria.

Mhe. Naibu Spika, mwenzangu hapa aliyetangulia alisema sheria ni msumeno, ni kweli kwamba ukifanya kosa mfano kwenda mbele basi utahukumiwa. Lakini ukirudi nyuma fanya mazuri basi itakulinda. Kwahivyo, ndio maana watu wanasema kwamba sheria ni msumeno. Jukumu kubwa la serikali pamoja na sheria,

Wizara hii ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kuweka *security and order*, ambayo yakipatikana mambo haya hususa kwenye *order, security* ni usalama ambao pia utasaidia nchi iende kwa vile ambavyo inatakiwa iende. *Order* itatusaidia kuweka mshikamano, kuweka ushirikiano na kuweka umoja, utulivu, amani, upende na kadhalika.

Kwahivyo, nathubutu kusema kwamba sheria ni muhimu sana katika kila kitu. Kwa mfano, uwe rais au waziri na hata raia wa kawaida basi pia kuna sheria zinakulinda.

Mhe. Naibu Spika, sasa kabla sijaingia kwenye michango yangu ya kwenye kitabu hiki, napenda kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

Sasa naingia kwenye hoja. Kwanza kabisa ili twende vizuri na kesi na twende vizuri na wakati, tuwa-*convict* watu ambao wamefanya makosa kweli, basi vile vyombo vya kuchunguzi kisayansi au kitaalamu lazima viweko, yaani ushahidi wa kweli lazima vile vyombo vinavyoweza kuleta ushahidi wa kweli lazima tuwenavyo. Kwahivyo, nashauri wizara husika ifanye utaratibu ambao utatuwezesha tupate vyombo hivyo, hata kwa kuanzia kwanza na pia tupate wataalamu wanaoweza kuvitumia vyombo hivyo.

Kwa mfano, mambo ya *DNA* na mambo mengine mengi ambayo ushahidi wa kweli itasaidia kuthibitisha kwamba huyu hata kama kapata mashahidi wa uwongo wangapi wanamtetea, lakini huyu ndiye aliyefanya kosa.

Mhe. Naibu Spika, sasa naingia kwenye Sehemu ya Pili. Sehemu ya Kwanza sikuona tatizo imekwenda vizuri, Sehemu ya Pili kidogo nataka kutoa mchango wangu. Kinasema kwamba

Mamlaka, namba 4 hiyo inasema, Mamlaka ya Mahakama za Zanzibar kwa madhumuni ya sheria hii ni sehemu yoyote ndani ya Zanzibar na sehemu yake ya bahari, na makosa yatakayotendeka kwenye Bahari Kuu katika vyombo vilivyosajiliwa Zanzibar. Sasa hapa tunataka kujua kwanza kwenye bahari ni undani gani kwenye bahari, hiyo itaitwa ni habari ya Zanzibar ni eneo la Zanzibar.

Sehemu ya Tano, inasema kwamba endapo kitendo ambacho kimefanyika chote ndani ya mamlaka ya Mahakama, itakuwa ni kosa dhidi ya sheria hii na endapo sehemu ya kitendo hicho kimefanyika nje ya mipaka ya mamlaka ya Mahakama, mtu ambaye sehemu ya kitendo hicho ndani ya Mamlaka ya Mahakama, anaweza kushtakiwa na kuhukumiwa chini ya sheria hii kama vile amekifanya kitendo hicho chote ndani ya Mamlaka ya Mahakama.

Sasa hapa nasema sheria kidogo haijafafanua wazi kwa mtu ambaye amefanya kosa ndani ya Mamlaka ya Mahakama ya Zanzibar, lakini kwa bahati mbaya ameshatambulikana anatafutwa sasa akamatwe, lakini kwa bahati mbaya ameondoka kwa kukimbia. Akienda nchi nyengine au nje ya eneo hili na kule akafanya kosa kama lile na kwa bahati mbaya akakamatwa akafungwa. Sasa nini hatima yake atakaporudi hapa. Nilitaka hapa ieleze wazi, atasamehewa kwa sababu keshafungwa huko, au akirudi hapa ana kesi yale.

Pia Mhe. Naibu Spika, ningependa nijuwe *validity* ya kesi, kama mtu amekimbia kesi ni muda gani ambapo atarudi atakuwa bado atashtakiwa, na muda gani ambapo atakuwa pengine hana kosa, kama hakuna ningependa kujua hilo.

Halafu Sehemu ya Tatu, nikiingia katika sehemu hii misingi ya jumla kuhusu uwajibikaji wa kijinai. Hapa inasema kwamba

kutokujua sheria hakuwezi kuwa ni sababu ya kusamehewa kwa kutenda au kutokutenda kitendo ambacho kinaweza kuwa ni kosa. Isipokuwa kama kujua sheria kwa mkosaji kitaelezwa wazi kuwa ni kiini cha kosa. Sasa mtu ambaye hajui sheria anajijua mwenyewe, au labda akuambie aa! mimi sheria hii sijui, kwa hivyo shahidi yeye mwenyewe. Sasa nani atakuja kueleza, hapa imesemwa yapatikane maelezo kwamba huyo mtu hajui sheria, nani atakayekuja kueleza kitendo hicho mpaka aaminiwe kwamba kweli huyu mtu hajui sheria. Hapa pia ningependa nipate ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, halafu niende kwenye ukurasa wa 283, sura ya 6 uhaini na makosa mengine dhidi ya serikali. Hapa sheria namba 27 inasema, "mtu ambaye anapanga, anaanzisha, anazusha au anakusudia tendo lolote, jambo au dhana na kueleza kutamka na kutangaza mpango, kuanzisha, kuzusha au kusaidia huko kwa kuchapisha chapisho lolote au maandishi, au tendo lolote dhahiri au kwa kutenda tendo lolote ambalo linakusudia kuleta au kusababisha kuondosha au kuleta mabadiliko ya Serikali ya Zanzibar kinyume na utaratibu wa katiba, ambapo mabadiliko ya Serikali ya Zanzibar kinyume na utaratibu wa Katiba ya Zanzibar atakuwa ni mkosa wa kosa la uhaini na atapewa adhabu ya kifo". Kwanza napenda kusema kwamba mtu huyu kama atafanikiwa anaweza akasababisha vifo vya watu wengi sana.

Kwahivyo, nadhani hii sheri sasa ichukuwe mkondo wake kwamba ifanyike mtu akibainika na kosa basi adhabu yake iwe ni kifo kweli, isiwe ipo hapa imeandikwa tu lakini anafanya kosa inafanywa kama haijulikani, matokeo yake anaachiwa anakuwa huru. Hivyo, itakuwa anavunja kanuni moja, anajaribu ile inaitwa *conspiracy to pervert the course of justice* na anayemsaidia basi pia na yeye anaingia kwenye kosa kama hilo.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 28 kinasema;

"Mtu anayeingia Zanzibar kwa nia ya kupanga harakati za kupinga Mapinduzi dhidi ya serikali au kwa nia ya kuchochea wengine kupanga harakati hizo atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu".

Sasa mgeni anapofika hapa anakutana na watu bila shaka bila ya msaada wa watu hawezi kufanya haya yaliyoelezwa hapa. Kwahivyo, nasema na yule atakayesaidia vitendo vivyo na yeye pia awekewe hukumu yake.

Halafu nakwenda kifungu cha 30 hasa (b) inasema:

Kifungu cha 30(b)

"Kwa mtu yeyote ambaye anafahamu kuwa mtu yeyote ana nia ya kutenda kosa la uhaini au kufanya uhaini na hakutoa taarifa kwa njia yoyote kwa Rais wa Zanzibar, waziri wa Serikali ya Zanzibar au Ofisa Tawala, Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, Hakimu au Ofisa Dhamana wa Kituo, Polisi au hakufanya jitihada za kuzuwia kufanyika kwa kosa, atakuwa ni mkosa wa kosa la kupita uhaini".

Hapa mimi nasema kwanza Ofisa Tawala hayupo tena, kwa hivyo hapa pafanywe marekebisho kwamba siku hizi kuna Katibu Tawala, kama ndio huyo aliyekusudiwa, kama siye basi nawachia kama kilivyo. Lakini kama ni Ofisa Tawala wa Wilaya, wa Mkoa wana wajibika kihivi, basi iwe Katibu Tawala.

Mhe. Naibu Spika, sasa hapa mtu anafahamu kuwa, mtu yeyote ambaye anafahamu kuwa mtu yeyote ana nia ya kutenda uhaini. Sasa hapa kidogo mimi nasema, inawezekana mtu akafahamika visivyo na inawezekana akafahamika kweli visivyo. Kwahivyo, ielezwe hapa kwamba mtu kama kabainika anafanya hivi

ambavyo vimeelezwa hapa, lakini baadae akaja akabainika hana kosa hilo, basi pia ielezwe kuwa atafanywa nini.

Mhe. Naibu Spika, niingie kwenye ukurasa wa mwisho. Kwakweli hii karatasi imeandikika kweli. Kwa hivyo, naona tabu hata kusema mambo mengine, kwa sababu pengine nitajikosea mimi mwenyewe, kwa sabu wataalamu wamekaa hasa wakaiandika hii.

Mhe. Naibu Spika, Sehemu ya Kumi katika ukurasa wa 303, makosa mchanganyiko dhidi ya Mamlaka ya Umma. Vile vile hapa kuna maelezo, "mtu yeyote aliyeajiriwa katika utumishi wa umma, ambaye katika kutekeleza majukumu ya ofisi yake anafanya udanganyifu wowote au kuvunja uaminifu unaoathiri jamii ama udanganyifu huo au uvunjaji wa uaminifu ungekuwa ni jinai au sio jinai kama ungetendwa dhidi ya mtu binafsi atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichodhidi miaka miwili". Hapa mimi nasema kwanza kama kosa ni hilo, hili ni kosa kubwa na ni kosa la kihalifu kimaendeleo. Kwahivyo, miaka miwili hii kwanza ni kidogo sana, angalau ingeanzia miaka mitano. Lakini pia kuna mtu anayemsaidia, hakuelezwa hapa. Sasa kama kuna mtu atamsaidia kufanya hivyo, basi na yeye pia atumikie hii miaka miwili.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo narudia tena, naona nisiende mbali wenzangu wameshachangia sana. Narudia tena kupongeza wizara hii, hususan Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kutuletea mswada huu ambao una umuhimu sana katika maendeleo ya nchi hii. Nchi ikiwa tulivu na nchi ikiwa inadhibitiwa vizuri basi maendeleo tunayokusudia yale ya katika kundi la pili la uchumi wa dunia basi tunaweza tukayafikia haraka.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu na kunipa fursa hii. Napenda kurudia tena kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Dkt. Makame Ali, mchangiaji wetu anayefuata sasa hivi ni Mhe. Miraji Khamis Mussa, baadaye atafuata Mhe. Mussa Ali Mussa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi jioni ya leo ya kuchangia mswada huu wa sheria mpya ya adhabu. Kwanza na mimi niwapongeze wote walioleta mswada huu mbele yetu, ni mswada mzuri una mambo mazuri, kwa hivyo tunachangia na sisi vile vile vizuri ili ukae sawa zaidi.

Mhe. Naibu Spika, moja kwa moja niende kwenye Sura ya Pili, eneo la matumizi ya sheria namba 4. Katika kifungu namba 4 kuna maneno hapo nachangia tu kwa ufupi, lakini tafsiri yake wenzangu watakuja kunipa inahusisha kwenye Bahari Kuu katika vyombo vilivyosajiliwa Zanzibar. Naongea yale maudhui ya moja kwa moja. Hapa tunazungumzia zaidi maeneo ambayo sheria hii itafanya kazi. Sasa Bahari Kuu imetajwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano, ile mipaka yetu haikutaja maeneo ya Bahari Kuu. Sasa isijekuwa tunatunga sheria ambayo baadae itatoa mgongano. Wenzetu tu waje watuweke sawa kwenye eneo hili, napendekeza kama kutakuwa na tatizo hilo basi tuizungumze ile mipaka yetu kama ilivyotajwa na Katiba ya Zanzibar kwenye kifungu hicho. Sina tatizo lakini nilikuwa na mchango wangu huo.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende kwenye Sura ya 6, Uhaini na Makosa mengine dhidi ya serikali. Pia katika kifungu cha 27 kuna maneno katika kifungu hicho na nayaanza hapo hapo katika kwa sababu mswada ni mkubwa na maneno ni mengi;

Kifungu cha 27

"…au kwa tendo lolote la dhahiri"

Sasa maelezo kwa ujumla yanazungumzwa matendo yale ya uhaini, hapa kwa tendo lolote la dhahiri, lakini kuna matendo ya siri yanahusiana na huu uhaini na ndio maana kukawa kunawekwa idara mbali mbali za ulinzi na usalama wanayapeleleza na wakayapata katika kutengeneza kosa maana yake na pale tunaweza tukawashtaki. Sasa wenzetu watuambie hapa tendo lolote la dhahiri, haya matendo ya siri kwenye eneo hili la uhaini kwenye kifungu hiki tunayapa nafasi gani. Kwahivyo, wenzetu watusaidie na vyenginevyo waweke ya dhahiri na ya siri au siri na dhahiri kwenye eneo hili.

Mhe. Naibu Spika, sina tatizo. Lakini pia kwenye kifungu cha 28 ambacho pia hiki kinabeba mahudhui ya kifungu cha 27. Kuna mtu anayeingia Zanzibar kwa nia ya kupanga harakati za kupinga Mapinduzi dhidi ya Serikali, lakini na 29 pia kinasema mtu anayechochea mgeni sasa tafsiri ya maneno haya maana yake kama yanaondoa ule umoja wa kifungu namba 27.

Sasa nilikuwa napata shida tu je, kwa Wazanzibari ambao wamejiingiza na wamefanya vitendo hivi vya ushawishi maana hapa tumewazungumza hawa, ni vyema sasa tukatunga sheria tukawazungumza wote ikawa Zanzibari ikawa wageni malengo yangu yalikuwa hayo maana yake hapo tulizungumza kwa mtu anayeingia Zanzibar anayeingia Zanzibar yupi, maana anaweza kuingia Zanzibar mgeni anaweza kuingia Zanzibar Mzanzibari mwenyewe maana katoka Dar-es-Salaam kuja Zanzibar lakini mazingira yake ni yepi. Sasa naomba hili kosa maana yake liwahusishe watu wote ikiwa ni Mzanzibar ikiwa ni mgeni lakini na tafsiri yake iwekwe vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda kifungu namba 30 mtu yeyote ambae ataficha uhaini baada ya kutokea au atafanya (b) hiyo kwa kuwa mtu yoyote ana nia ya kutenda uhaini au kufanya uhaini kutoa tafsiri kutoa tarifa kwa njia yoyote kwa Rais wa Zanzibar, Waziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Afisa Tawala, Jaji wa Mahakama Kuu Zanzibar, Hakimu na Afisa dhamana au kituo chochote cha Polisi.

Tunapozungumza sheria hii maana yake ni sheria ya Zanzibar tuna vikosi vyetu vya Idara Maalum tunaanza na Comodoo, na Makamishna sasa unampa mamlaka tu kama Afisa Tawala lakini Idara Maalum nzima unaiwacha ambapo sehemu kubwa wale wakuu wake wa vikosi ni wakuu wa ile kamati ya Ulinzi na usalama ya Zanzibar maana unawatoaje. Sasa nilikuwa napendekeza zaidi ya hawa tuliowaweka basi na wale wa Idara Maalum waingizwe pale maana yake iingizwe na Idara Maalum, mimi sina tatizo na waliowekwa lakini ule msingi wa hapa maana yake lazima tukubaliane hawa wakuu wa vikosi basi wana umuhimu sana.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende katika kifungu namba 31 nacho 31(a) kinazungumza kumuondoa mtu kwa nguvu za kijeshi kutoka kwenye Ofisi ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, mtu huyu ni mtu gani maana unaweza kwenda kumuondoa mtu kwa nguvu katika hiyo hiyo Afisi ya Rais lakini kenda kuchukuliwa pengine mlinzi, sasa tupate tafisi ya mtu huyu ni mtu wa aina gani. Lakini vimezungumzwa vyombo vyengine kama Baraza la Wawakilishi, lakini tujue katika vitu vya uhaini kosa kubwa ni vyombo vyetu vya habari ambavyo katika makosa ya uhaini ukiviteka hivi, maana moja ya mbinu na mikakati ya watu wanaoataka kufanya uhaini hukimbilia huku kwa nini vyombo vya habari tumevitoa katika eneo hili. Mimi nije nipate majibu tu lakini dhamira yangu nasema zaidi ya hivi

tulivyoviweka basi na vyombo vya habari tuviingize ili kuweza kulinda ule uhaini katika maeneo hayo muhimu.

Lakini katika hiyo hiyo 31(i) kuanzisha vita dhidi ya Zanzibar au kuionyesha nia kwa kitendo cha dhahiri, narudia kule kule kitendo cha siri kinakuwaje maana katika uhaini hata ukiona watu wako dhahiri basi ujue hao walevi wanapita wakiongea, lakini katika uhaini hasa watu wanafanya siri. Sasa dhamira yangu ilikuwa ni hiyo hiyo dhahiri na siri iwepo.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende katika kifungu namba 32(1) ambacho mtu hataweza kushtakiwa kwa kosa la uhaini au kwa makosa yaliyoainishwa kwenye vifungu namba 30 na 31 isipokuwa shtaka lililoanzishwa ndani ya miaka miwili baada ya kosa kutendeka. Sasa hapa nilikuwa napata mashaka Mahakama ipi maana yake itakuwa ina uwezo wa kushtaki hivi vitendo vya uhaini, lakini Mahakama hapa kama tumeziweka lakini tukishamaliza maana sisi hapa Mahakama zetu tunamalizia katika *level* ya Mahakama Kuu. Je, kwa sheria yetu hii itatupeleka katika Mahakama ya Rufaa. Sasa sijui wenzetu wanasheria kwa sababu mimi sikupita katika sheria lakini tutaweka katika utaratibu gani wao wenyewe wanaweza wakatusaidia.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende kifungu chengine kipya namba 39 mtu yoyote ambae atasimamia au atakuwepo na atakubali kusimamia kiapo chochote, hapa tunazungumzia suala la viapo visivyokuwa halali sasa tafsiri ya viapo hivi visivyokuwa halali maana yake hayupo. Mtu anaweza kusema tu siku moja akaamka asubuhi mimi walahi bilahi mie Rais wa Zanzibar maana yake tunajua ndio kiapo hicho ambacho kakosea, sasa tafsiri ya viapo maana yake itakuwa vizuri nayo ikatolewa. Sasa bila ya kutoa maana yake hili linaweza likawa tatizo akasema mimi kweli nimeapa lakini tafsiri ya kiapo kisichohalali ni kipi.

Sasa naomba niende kifungu cha 43(1) ambacho hapa chini yake huko kuna adhabu huko imetolewa kifungu kwa kipindi kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi miaka miwili, adhabu hii kwa makosa tunayozungumza hapa ni adhabu nyepesi kweli kweli. Mhe. Naibu Spika, napendekeza adhabu hii tukaiangalia upya na tukaiongeza kwa mujibu wa makosa ambayo tunayazungumza hapa, sasa katika kupendekeza angalau tungeweka miaka mitatu.

Mhe. Naibu Spika, lakini eneo hilo hilo tumezungumza kesi za uvumi ripoti ambazo kawaida zitapelekea katika utaratibu wa kupotosha nchi, lakini kuna vyombo vya habari vitakavyotumika unajua nchi ya Rwanda kuna mwandishi wa habari mmoja alipotosha umma watu wakauwana bure tu na wengi tu. Lakini hapa hatukuiweka sasa vyombo vya habari mtu akitupotosha maana yake, adhabu yake ni nini ijapokuwa anasema sehemu kubwa ya vyombo vya habari inawezekana maana yake utaratibu wake usisimame hapa au kama sheria zile za mtandao zikakaa katika Jamhuri ya Muungano, lakini sheria yetu sisi italindaje utaratibu huu. Sasa ndio maana nikasema katika kifungu hichi kwanza adhabu ni ndogo na tuiongeze.

Lakini eneo la kifungu namba 44(2) mtu hatoshitakiwa kwa kosa chini ya kifungu hichi bila ya ruhusa ya maandishi ya Mkurugenzi wa Mashitaka, nilikuwa nasoma Katiba katika eneo lile la 56(a)(4) ukiisoma Mhe. Naibu Spika, utaikuta Mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka chini ya kifungu namba 3 yanaweza kutekelezwa na Mkurugenzi wa Mashitaka mwenyewe au mtu mwengine kwa maagizo au amri maalum kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashitaka.

Mhe. Naibu Spika, sasa sheria hii tumeipeleka moja kwa moja kwake yeye Mkurugenzi wa Mashtaka, lakini katiba pia imezungumza kwa upana zaidi sasa nasema tafsiri hii angalau ilingane na kifungu hichi cha katiba maana yake ile kuweka na

utaratibu wa kawaida, lakini jengine katika utaratibu wa kimahakama wana uwezo wa ku-*establish* ile *motion* ya kesi maana yake wakaitisha ile. Sasa katika kifungu kama hichi maana yake hawa wote wakawa shtaka hawajalipeleka Mahakama je ikasema hili shauri hili ni letu hawana haki ya kulisikiliza katika kifungu hichi kidogo Mwanasheria Mkuu uje utusaidie kunako eneo hili.

Lakini kwa dhamira ya maelezo yangu ya kifungu hicho pia basi maana yamejitokeza kwenye kifungu mwanzo cha 44(2), 47(2), 50(1), 70(3), 96(8) na kifungu cha 144 ambacho kime-*court* vifungu vya 142 na 143. Kwahivyo, yale ambayo nimeyasema hapa na ushauri wangu yasipingane na Katiba basi yaainishwe kwa vifungu vyote hivyo nilivyovitaja kama Katiba ya Zanzibar inavyoelekeza katika eneo alilopewa haki za msingi Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende kifungu cha namba 46(1) na 46(2) kwa pamoja maana huku yametwajwa makosa lakini huku imetajwa katika utaratibu wa kawaida kifungu 46(2) naomba na hichi nikisome. "Bila ya kujali masharti ya kufungu kidogo namba 1 mtu anayeunda au anayeweka vifaa katika chombo kwa namna moja wapo katika hizo zilizotajwa kwa kutimiza mkataba uliofanywa kabla ya kuanza kwa vita kama ilivyoelezwa hatapewa adhabu yoyote".

Sasa lakini kifungu cha (a) ukikifuatilia baada ya Mhe. Rais wa Zanzibar kutoa tangazo la kutokufungamana na upande wowote katika vita mtu huyo atatoa *notice* mara moja kwa Rais wa Zanzibar au Katibu Mkuu Kiongozi. Mhe. Naibu Spika, hoja yangu iliyo hapa na naomba hapa uje uniweke sawa vizuri Mhe. Mwanasheria Mkuu mmehusisha taasisi Maana yake ni Mhe. Rais wa Zanzibar katika kutoa ile *notice* lakini tumehusisha pia Afisi ya Katibu Mkuu Kiongozi katika jambo kubwa kama hili, maana

yake *notice* hii yawezekana ikaenda kwa Katibu Mkuu Kiongozi moja Katibu Mkuu kiongozi kama tulivyonae sasa hivi *alhamdullillah* maana yake mawasiliano na Rais yako karibu anaweza akatoka akasema *notice* nimepokea. Lakini tunaweza tukaja tukapata Makatibu Wakuu Kiongozi wengine pengine wenye dhamira kama hawa waliokuweko nyuma ya pazia kwenye jambo hili .

Sasa mimi hoja yangu maana yake taasisi ya Mhe. Rais kuiunganisha na watendaji …….

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Miraji Khamis Mussa, umebakisha dakika mbili.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mbili haya naomba nimalizie lakini hoja yangu hapa maana yake ni kumbakisha Mhe. Rais na kuondoa tafsiri ya Katibu Mkuu Kiongozi. Lakini kufungu namba 47(i) tumezungumzia mambo ya vyombo hivi ya baharini lakini kwenye anga vipi hapakuzungumziwa hapa tunaelekea wapi sasa makosa yakifanyika katika upande wa anga vipi, lakini anga ambayo inapita katika visiwa vyetu vya Zanzibar. Sasa kwa kuwa muda wangu umeisha yaliyobakia naomba nichangie kwa maandishi maana mengi kidogo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu. Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru kwa kunipa nafasi na kunishtua kuwa dakika zimekwisha nakushukuru sana ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Miraji Khamis Mussa. Mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Mussa Ali Mussa, na baada ya hapo atachangia Mhe. Hamza Hassan Juma na ajitayarishe mchangiaji wetu wa mwisho kwa upande wa wajumbe Mhe. Panya Ali Abdalla.

Mhe. Mussa Ali Mussa: *Bismillah Rahmani Rahim* ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi kuchangia Mswada wa Sheria ya Adhabu, Mswada ambao unatokana na makosa matona ya awali na sasa kufikia makosa 11, kwa kweli ……..

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mussa Ali Mussa, tunaomba sijui watu wa mitambo sijui kama mnasikia au ni mimi tu ninayesikia kelele nyingi sana ee haya tuendelee.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Huu mswada wa adhabu……

Mhe. Naibu Spika: Hebu tafuta sehemu nyengine ya kuzungumzia labda hapo pana matatizo kidogo.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Mheshimiwa kwenye mitambo.

Mhe. Naibu Spika: Lakini inawezekana hapo pana matatizo atafute sehemu nyengine azungumzie kidogo labda.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Kwanza Mhe. Naibu Spika, nataka nieleze historia ndogo ya Zanzibar. Zanzibar haikuwa na makosa mengi ya jinai Zanzibar ilikuwa ni nchi ya utulivu na amani na usalama, makosa haya yamekuja baada ya mitandao, mitando ndio iliyosababisha makosa mengi Zanzibar. Zanzibar leo ni ajabu Zanzibar iliyopita kusikia kuna mtoto wa miaka minne au saba amebakwa ilikuwa ni ajabu kubwa sana jambo hili halikuwepo. Au mtoto wa kike amepewa ujauzito jambo hili pia halikuwepo mambo haya yamejitokeza baada ya mitandao kuja hapa. *(Makofi)*

Lakini, ninachoataka kusema kwamba makosa haya ambayo leo tunayatungia vifungu vya adhabu kuna makosa mengine adhabu zake naziunga mkono ni sahihi, kuna makosa mengine nasema adhabu zake ni kubwa mno. Mhe. Naibu Spika, unaposimama kutunga sheria ujue sheria ni msumeno leo iko kwangu kesho iko

kwako na inakata kote kote, sasa tuangalie hii sheria tunayoitunga je itakata upande mmoja au itakata kote kote na ikikata kote kote je haina madhara. Sheria ambayo nataka kuizungumzia ni kifungu 114 kifungu hichi cha shambulio nasema kifungu cha shambulio la kuumiza mwili hichi kifungu kina kasoro, kwa sababu mimi ni mzazi nina watoto na watoto wa sasa kama tunavyowajua hawaeleweki, wewe baba wanakuona huna maana, huna akili na mwisho wanakubalidisha jina wanakuita dingi.

Jee, leo unarudi kazini unamkuta mtoto wako wa kike wa miaka 18 amesimama na mjane ukimshambulia Mhe. Naibu Spika, ufungwe miaka 14 hiyo ni sheria, na utakaposhambulia ujue unashambulia kwasababu umechukizwa hushambulii tu utashambulia kwasababu umechukizwa na unaposhambulia bakora haichagui utakwenda kupiga wapi, bakora inaweza kupigwa kwenye kichwa, kwenye bega au kwenye mgongo na bakora ikienda inakwenda na uvimbe au damu. Sasa hapo baba atapelekwa katika vyombo vya sheria na atahisabiwa ameshambulia na akipatikana na hatia na hatia itakuwepo kwa sababu PF3 itasema kwamba mtoto amepigwa. Jee baba akifungwa miaka 14 au 10 akirudi hawa watoto wengine waliobakia hapa nyumbani watabakia na nani, watabakia katika shauri lipi, katika huduma ipi.

Mhe. Naibu Spika, kwahivyo tunapotunga sheria tuangalie sheria na nia ya lile kosa ovu na matokeo yake na vitendo viovu. Tusiangalie tu kwa sababu huyu kashambulia basi madhali amepatikana na hatia afungwe kifungo cha miaka 14. Baba ana haki ya kumshambulia mtoto wake, baba ana haki ya kumshambulia mkewe, kwasababu kuna mambo ambayo itabidi tushambulie ndani.

Kwa mfano, nimekwenda kutaabika mchana wa kutwa nzima, nimekuja sasa nataka kupumzika, wewe hutaki, ile ni haki yangu

mimi, hata sheria inasema hivyo. Ingawa sheria inasema ushambulie kwa kutumia ncha ya kanga. Lakini hapa hapatakuwa na ncha ya kanga, maana yeke mimi na wewe tulikubaliana kuwa tutaowana. Sasa kama tumeowana basi mambo mengine yafuatie na yakifuatia kama hayataki kufuatwa kwa taratibu, itabidi yafuatwe kwa nguvu. Kwa maana hiyo kifungu hichi nacho kinatakiwa kifanyiwe marekebisho. Kwasababu wewe mwanamke utamnunulia pweza wa shilingi 8,000/= na mchuzi akanywa yeye mwanzo, usiku atakuletea rapsha ya kusema kwamba umembaka, hapa ubakaji haupo. Kwahivyo, hivi vifungu tuviangalie, lazima kila kitu tukiangaangalie na taratibu zake na mwendo wake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, twende kwenye kuvunja nyumba mchana au usiku. Hiki ni kifungu cha 290, nasema kwamba uvunjaji ni lazima uwe na nia ovu na kitendo kiovu, kwasababu utakapovunja nyumba ama kwa kutumia kuvunja mlango au kuondosha kanga utakuwa umevunja. Sasa jirani yako umepita mbele ya nyumba yale kuna joko limeingia wewe una bakora, ukaingia ndani ukalitoa kulipiga, sasa ushtakiwe na ukipatikana na hatia kwa kuwa umevunja ufungwe miaka 15. Ni lazima kwanza kuwe na nia ovu na vitendo viovu ndiyo ufungwe hii miaka 15. Au umeingia ndani umeiba embe mtoto wa miaka 17 anatoka shule au 18 kaingia ndani ya nyumba ya bibi Kizee kaiba embe anakuja kufungwa miaka 17 kwa sababu ya embe.

Mhe. Naibu Spika, haya makosa yaangaliwe na uzito wake sio tu kwamba mtu kavunja, kaingia ndani, nyumba za kwetu kule vijijini makuti ndio mlango, hazina kufuli wala vitasa, kuti, kanga, shuka, ni kuvunja nako kuondosha ukaingia ndani nako ni kuvunja. Lakini sasa tumfunge mtu kwa kuwa kaingia ndani kaiba yai moja tu, tumfunge miaka 15. Hili nalo naomba Waziri akija aje anipatie majibu.

Mhe. Naibu Spika, jengine kuhusu kughushi paspoti, hili kosa naona limeletwa hapa Zanzibar vipi na hili ni kosa la Muungano. Kama mtu anaghushi paspoti au ataghushi *document* nyengine yoyote ya Muungano hawezi hapa akahukumiwa, atapelekwa kwenye Serikali ya Muungano.

Vilevile kunahichi kifungu cha 69 kukutwa na silaha hili nalo ni kosa la jinai jamani. Mtu akipatikana amekutwa na silaha nyumbani kwa mtu anafungwa mwaka mmoja wakati aliyemshambulia mkewe anafungwa miaka 14. Nasema hapa napo panataka marekebisho. Kukutwa na silaha ni kosa kubwa tena la jinai tena kubwa sana kwahivyo mtu akikamatwa na silaha, hiyo silaha kwanza kaipata watu. Silaha inatakiwa iwe na askari wa polisi ambaye anakwenda kazini ndiyo anayetakiwe awe na silaha kisheria. Silaha inakuwepo Kambini kwa jeshi kwenye vikosi huko ndio kwenye silaha. Sasa unakamatwa na silaha unakwenda nayo nyumbani kwa mtu unakuja kufungwa mwaka mmoja huwo si utani. Kifungu hichi nacho angalau kiwe ni kifungu kisichopungua miaka mitano kwa sababu nalo ni kosa kubwa.

Mhe. Naibu Spika, kutamka tu kwamba mtu afungwe miaka 30, afungwe maisha, ujue kwamba iko siku atafanya kosa mtoto wako. Je, utakubali nayeye afungwe maisha. Sheria haichaguwi, tunapitisha tu mtu afungwe maisha. Sasa hivi tunafurahi kwamba mtu afungwe maisha unajua mtu ukimfunga maisha unamfunga mtu maisha ni sawa sawa na umemuhukumu kifo, uangalie nalo hilo kosa la kumfunga mtu maisha au miaka 30. Tuangalie na wakati maana wakati nao umebadilisha, makosa mengi yameingizwa kimitandao, makosa mengi yameingizwa kichuki, kisiasa ndiyo makosa yamekuja kujaa Zanzibar. Zanzibar haikuwa nchi ya makosa.

Kwakweli, Zanzibar haikuwa nchi ya makosa imeingiwa kwa makosa. Katika asilimia 15 wanasiasa tumechangia makosa,

maana mtu anafika tu analazimisha mimi lazima niwe fulani, ikiwa hukuwa fulani unasababisha fujo. Ikiwa hukuwa hivi itakuwa hivi, ikiwa hivi fanyene hivi. Sasa wewe hawa unaowaambia na wao ni binaadamu na wao wanatamania labda wewe ukiwa hivi yeye atapata hichi na yeye anakwenda kufanya fujo. Haya mambo yote tuyaangalie, sisi wanasiasa tunapokaa kwenye viriri tunakuwa tuna mambo yetu. Yale mambo yetu ya kutaka lazima mimi niwe kiongozi ndiyo yanayosababisha haya makosa ya jinai.

Mhe. Naibu Spika, hebu angalia wewe unasema mimi niapishwe niwe Rais, sasa uwapishwe uwe Rais vipi sasa, aah mimi lazima niwe Rais. Haya sasa na wengine huku wanasema wewe ndiyo utakaekuwa Rais, basi wanakuapisha. Ndio kwa majirani zetu mmeona yametokea. Mtu anakwenda kumtafuta mtu hata siyo wa nchi ile anakuja kumuapisha ili awe Rais. Mambo kama yale nayo yanatokezea hapa Zanzibar yamenusa, kwa hivyo hizi sheria tukizitunga tuziangalie vizuri sana ili zisije zikaleta madhara kwa watu wote. Isipokuwa kuna makosa ambayo haya nasema ni lazima tukiri kwamba tuyachukie na tuyakemee.

Mhe. Naibu Spika, hawa wenzetu wanaobaka watoto wa miaka 7, 8, 9, mpaka 16, hawa ndiyo wanaostahiki kufungwa miaka 30. Hawa ndiyo watu wabaya katika Zanzibar na kwa nchi nyengine yeyote kwa sababu hawa ni wauwaji. Huwezi kumbaka mtoto wa miaka 6, 7, unapata jambo gani, una raha gani. Hii ni laana, hii ni aibu kusikia nchi kama hii ya Zanzibar inafanya mambo kama haya au kuna mtu amefanya jambo kama hili na akawa bado yumo mitaani anatanua. Hichi si kitendo kizuri ni kitendo ambacho tunahitaji kukilaani na kukikemea kabisa kisitokezee. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, jengine ninalotaka kulizungumzia ni kuhusu watoto. Watoto hawa wanaobakwa wazazi pamoja na mimi

tunachangia watoto wabakwe. Mtoto anakuja ana miaka 18 ndani ya nyumba ana simu ya laki tatu, wewe baba, wewe mama, unaridhika na hilo jambo tena unamwambia hebu nichatie, anakulia nyimbo na wewe unacheza. Jamani tumejisahau.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mussa Ali Mussa, malizia una dakika mbili za kumalizia.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Tutatunga sheria hizi lakini tusijisahau na ulezi nao tuusimamie vizuri. Ulezi jamani tuusimamieni vizuri, tuache kuwadekeza watoto. Kama una pesa nyingi basi katoa sadaka Msikitini usimtunukie mtoto simu ya laki tatu, sheria itakuwa tunazitunga tu lakini makosa yatakuwa bado yanaendelea. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ndogo nikaweza kutoa mchango wangu mdogo na naunga mkono hoja hiyo kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mussa Ali Mussa ahsante. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Hamza Hassan Juma na ajitayarishe Mhe. Panda Ali Abdalla.

Mhe. Hamza Hassa Juma: Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia machache katika mswada huu muhimu sana kwa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwakweli katika mswada ambao unatakiwa umakini mkubwa katika kuujadili na kuupitisha ni mswada huu. Mswada huu unachangamoto nyingi, miongoni mwa miswada ambayo tuliyoipitisha hapa Barazani uliyogusa maisha ya wananchi ya kila siku basi ni mswada huu, ili kumpunguzia *vi–memo* Mhe. Mwanasheria Mkuu, Mhe. Jaji Mkuu, Mhe. Mkurugenzi wa Mashtaka basi ni vyema tukaujadili vyema sana mswada huu na tukaupitisha, ili uweze kuja kutekelezeka usije ukatukwaza huko mbele ya safari.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza nilikuwa nataka nimuunge mkono sana Mhe. Mussa Ali Mussa, kwa kile kifungu cha *violent* ndani ya nyumba baina ya mke na mume. Sisi tunatunga sheria hapa lakini vile vile kunasheria mama inayotuzunguuka siku ambayo tuliyofungishwa mkono pale, ukakabidhiwa ukaambiwa *zawijuka,* mmoja akaitikia na vitu kama hivyo. Tukiangalia sheria hii kunamaeneo tunaweza tuka *violent* ile Sheria Mama ambayo sisi wengi Waislamu huwa tunaitumia. Nadhani ile hoja aliyoizungumza Mhe. Musa Ali Mussa, sina haja ya kuirejea nadhani Mhe. Mwanasheria Mkuu hizo taarifa utazipata kupitia kwa Mhe. Naibu Waziri ambaye alikuwepo alipokuwa akijenga hiyo hoja, kimsingi wengi waliipigia makofi inaonyesha kwamba wengi waliiridhia.

Mhe. Naibu Spika, naendelea moja kwa moja na mchango wangu kutokana na muda. Mimi kwanza nilikuwa nataka nipate jawabu kwamba katika sheria zetu nyingi tunazozitunga kuna hawa Mawakili hasa wanasimamiwa na sheria gani ambayo ina-*guide.* Mara nyingi tunapokwenda Mahakamani inabidi Mawakili wanahusika moja kwa moja katika kusimamia hizi kesi zetu, sasa wao hasa kuna sheria gani na miko gani ambayo *inawa–guide* katika kusimamia hizi kesi zetu.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 13 cha sheria hii kinachozungumzia umri mdogo, hapa kuna kifungu cha 13(1),(2),(3). Mhe. Naibu Spika, naomba kunukuu.

“Kifungu cha 13(1) kinasema hivi:-

> “Mtu mwenye umri wa chimi ya miaka 12 anachukuliwa kuwa hawezi kuwajibika kijinai kwa kutenda au kuacha kutenda …”

Sasa kifungu cha (2) kimetofautisha tu baadhi ya umri. Mimi nadhani ilikuwa kwa urahisi kabisa tungelijaribu kuangalia "Sheria ya Mtoto", mtu anapotajwa mtoto anakuwa ni kutoka umri gani mpaka umri gani. Kwa sababu hapa hawa watoto wamewekwa katika *category* tofauti. Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwasababu wao ndiyo waatalamu wa sheria, nadhani hapa moja kwa moja ingeelezwa kwamba mtu ambaye yupo chini ya umri fulani au sheria fulani inayozungumzia umri wa watoto, kuliko kuongeza maneno mengi sana ikawa mswada mkubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, la pili katika kifungu cha (17) ambacho pia mwenzangu Mhe. Mussa Foum Mussa amekizungumza mimi nitaomba nikirejee kwa njia tofauti kidogo. Kifungu hicho kinasema Matumizi ya Nguvu Katika Kujilinda. Hichi kifungu cha 17 (3) Mhe. Naibu Spika, naomba kunukuu.

Kifungu cha 17 (3) kinasema hivi:-

> "Mtu yeyote atakayesababisha kifo cha mtu mwengine kutokana na matumizi ya nguvu kupita kiasi katika kujilinda atakuwa ametenda kosa la kuuwa bila ya kukusudia."

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kama walivyosema wenzangu kwamba katika kupambana kuna mambo mawili, inategemea na yule mtu ambaye uliyepambana nae. Kwa mfano, kama alikuja na silaha unaweza ukatumia ile ile silaha yake ukamgeuzia yeye. Nadhani ichukuliwe kwamba huyu mtu ameuwa bila ya kukusudia. Nafikiri hapa ndiyo ilivyowekwa, nafikiri itakuwa haina tatizo sana. Unajua mazingira yetu hasa mtu anavyokuvamia usiku akaja na silaha na usiku unajua unakuwa kiza, ukishtuka tu unamuona tayari yule mtu ameshakuvamia inabidi na wewe sasa utumie njia yoyote ya kuweza kujilinda.

Hapa iwe yule aliyetoka kwenda kumvamia mtu nyumbani kwake kwa kosa lolote litakalojitokeza aidha akijeruhi yeye au akijeruhiwa yeye basi yeye pale ndiyo awe mkosa, lakini siyo kuhukumiwa yule ambaye aliyefuatwa nyumbani kwake.

Mhe. Naibu Spika, lakini kifungu cha 27 nazungumzia Sura ya Sita uhaini na makosa mengine dhidi ya serikali. Mimi hapa nampongeza sana Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. Kumekuwa na maneno mengi sana kwamba Zanzibar hakuwezi kufanyika uhaini. Mimi nadhani hiyo tafsiri ilikuwa inapotoshwa, Zanzibar uhaini unaweza ukafanyika kwa sababu Zanzibar ina dola yake kamili ina Serikali, ina Baraza la Wawakilishi na ina Mahakama zake, lakini vile vile inavikosi ambavyo tunaviita Idara Maalum lakini kwa mujibu wa sheria vimeruhusiwa kumiliki silaha. Inamaana hii ni dola kamili, sasa haiwezekani mtu akaja tu akataka kufanya vitendi vya uvunjifu wa amani kutaka kuiondoa serikali halali halafu akaambiwa aah! Maana yake, maana yake zimekuwa nyingi. Mhe. Naibu Spika, kwa kupitisha sheria hii leo kwakweli tutakuwa tumeyalinda yale Mapinduzi ya Zanzibar. Kwahiyo, nawapongeza sana kwa kuwa na ujasiri wa kuleta sheria hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba ninukuu kifungu cha 27 hapa kidogo kuna mambo nataka kushauri.

Kifungu cha 27 kinasema:-

"Mtu ambaye anapanga, anaazisha, azusha, au anakusudia tendo lolote, jambo au dhana na kueleza, kutamka au kutangaza mpango, kuanzisha, kuzusha au kukusudia huko kwa kuchapisha chapisho lolote au maandishi au kwa tendo lolote la dhahiri au kwa kutenda tendo lolote ambalo, linakusudia kuleta au kusababisha kuondosha au kuleta mabadiliko ya Serikali ya

Zanzibar kinyume cha utaratibu wa Katiba ya Zanzibar atakuwa ni mkosa atakuwa na kosa la uhaini na atapewa adhabu ya kifo".

Sasa hapa nilikuwa na *option* mbili. Mhe. Naibu Spika ikiwa vitendo hivi vilivyofanyika vitachukuliwa labda watu kama ilivyosema katika vifungu vyengine kama wameingiza silaha wameshawishi watu kutaka kupindua lakini tuchukulie mfano uliokuwa hai mfano kama mtu ambaye anamua kujitangaza kwamba yeye ni Rais kinyume cha Katiba na Sheria ya Zanzibar, sasa kwa tendo hilo kwa kusema kuweka adhabu ya kifo mimi nadhani ndio pale niliposema kwamba tutunge sheria ambayo inatekelezeka.

Mhe. Naibu Spika, nadhani ushauri wangu hapa tungeliweka kifungo cha maisha, kwasababu mtu anafanya kosa la kisheria na kuna sheria mbalimbali sheria ya vyombo vya habari vimeelezwa kwamba visijihusishe na uvunjifu wa amani, lakini mtu akatumia nguvu zake na mabavu yake akenda akatumia chombo kujitangazia sasa unapozungumzia kumuhukumu kifo hapa tunamtia kwenye mitihani rais kwasababu hukumu ya kifo lazima atiye saini rais. Lakini kifungo cha maisha jaji akishamaliza kazi keshamaliza mtu anaajaitangaza rais kesho asubuhi anachukuliwa anapelekwa lupango maisha hatoki.

Lakini sasa mtu unaposema kwamba akuhukumiwe kunyongwa sasa ile kwasababu kwanza pale hiyo serikali yenyewe itakuwa bado haipo. Mhe. Naibu Spika, nadhani ndio maana nikasema tujaribu kutunga sheria ambayo itakuwa utekelezaji wake ni rahisi tusimtie mtihani mtu mmoja, tusimtia hapa mtihani rais mimi nafikiri tungeliweka hapa kifungo cha maisha kule kwengine wanoingia na silaha kutaka kupindua na mambo mengine kule wacha mtu ahukumiwe kifo.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 30 vilevile kuna nyongeza nilikuwa nataka niongeze hapa kwamba mtu yoyote ambaye anaficha uhaini baada ya kutokea au anafahamu kwa mtu yoyote ana nia ya kutenda kosa la uhaini au kufanya uhaini na hakutoa taarifa kwa njia yoyote kwa Rais wa Zanzibar kwa Waziri wa Serikali ya Zanzibar au Afisa Tawala au Jaji wa Mahkama Kuu ya Zanzibar au Hakimu au Afisa dhamana wa Kituo cha Polisi au hakufanya jitihada ya kuzuia kufanya kosa atakuwa ni mkosa kwa kosa la kuficha uhaini na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Hapa mimi nilikuwa liongezwe neno Mhe. Naibu Spika kwasababu kwanza mtu kufichua lile tendo la kesi ya uhaini ni jambo kubwa sana linataka ujasiri kwa sababu wanaofanya uhaini wanaoandaa uhani ni watu ambao wanakuwa magwiji amejiamini anajiandaa kwa hujuma zozote na akisikia kwamba umetoa siri zao basi wanaweza wakakuhujumu. Kwahiyo, naomba liongezwe neno Sheha kwasabau hapa ametajwa tuu Rais, Waziri wa Serikali, Afisa Tawala, Jaji wa Makhama Kuu lakini kuna mtu muhimu ambaye yeye ndio anakuwa rahisi sana kwa mawasiliano kwa na wananchi Sheha kwa maana Sheha akishapewa taarifa kuna watu wanataka kufanya uhaini au kuna jaribio la uhaini lilifeli ina maana akienda kwa Sheha yeye atakuwa ni rahisi kufika katika ngazi zote.

Lakini kwa mwananchi wa kawaida umwambie aende akatowe taarifa kwa Afisi ya Rais hii kidogo hii sheria tunaifanya ngumu kidogo lakini hapa tukiongeza neno "Sheha" ina maana ule mtiririko wa kupata taarifa za hujuma iliyokuwa inataka kufanyika kwa kweli inakuwa tumeirahisisha hii kazi na tuna amini taarifa zitafika kwa wepesi kabisa.

Jengine kifungu cha 44 mtu yoyote ambaye bila ya dharura ya kisheria amechapa au amesambaza au katika mkusanyiko wowote

ametoa kauli au maneno yanoashiria yanomaanisha kwamba itakuwa ni lazima inahitajika.

a) Inasema kufanya kitendo kinachokusudiwa kuleta kifo au madhara ya kimwili au mtu wa tabaka lolote au jamii ya watu.

b) Kufanya kitendo kinachokusudiwa kutokeza au kuharibu mali itakuwa ni kosa atapewa adhabu ya kifungo cha kipindi cha miaka miwili au mtu hatoshitakiwa kwa kosa chini ya kifungu hiki bila ya ruhusa kwa maandishi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Sasa Mhe. Naibu Spika, hapa nataka yale maneno ya mwanzo kwamba kuna suala la uchochezi ambalo huwa linafanywa hasa katika masuala ya mitandao ya kijamii *social media*. Kwahiyo, hasa hapa nafikiri pia iongezwe kwamba katika hayo machapisho hayo basi pia ilikuwa iongizwe *social media* kwasababu sasa hivi ukiangalia hata *arrest* zilokuwa zinafanyika Mashariki ya Kati kwa asilimia kubwa hawakutumia magazeti, walitumia *social media* watu wanakwenda ma *group* kwenye *WhatsApp* kwenye *Twitter* kwenye mitandao na matokezeo yake inatokezea mkusanyiko, watu wanasabisha mpaka nchi zinavurugika zinakuwa mpaka leo hazitawaliki.

Lakini kifungu cha 55 Mhe. Naibu Spika mtu yeyote anayeshiriki katika mkusanyiko usio halali atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungu kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja. Mhe. Naibu Spika, naomba kuongeza hapa neno na faini ya shilingi milioni moja kwasababu mara nyingi adhabu zetu zinakwenda sambamba pamoja na faini sasa hapa imewekwa adhabu ya kipindi kisichozidi mwaka mmoja, hivyo, naomba liongezwe neno na faini isiyopungua shilingi milioni moja kwasababu kosa lenyewe ni kubwa ukisema isizidi anaweza kupigwa faini shilingi

elfu tano, kwa hiyo hapa iwe adhabu isyopungua shilingi milioni moja.

Vilevile, katika kifungu cha 61 wafanya fujo kubomoa majengo Mhe. Naibu Spika hili ni zoezi ambalo tumekuwa na utamaduni hapa Zanzibar kifungu chenyewe kinasema vipi watu ambao wamekusanyika kinyume cha sheria kufanya fuyo wanabomoa na wanaharibu....

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hamza Hassan Juma, zimebakia dakika mbili.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, basi wacha nitamalizia. Sasa hapa napendekeza hawa ambao waliokuwa wamekusanyika bila ya taratibu wanataka kufanya fujo hapa pia hukumu yao imeandikwa watapewa adhabu ya kifungo cha maisha, mimi nilikuwa naomba kifungo cha mimi nilikuwa naomba kifungo cha maisha Mhe. Naibu Spika, hii kwa kweli kwasababu haya matukio mara nyingi yanakuwa kama yana ushawishi fulani ukiangalia kama watu waliokuwa wanachoma mapira ya magari barabarani wengine ni watu ambao wala hawajijui wanafanya nini. Sasa ukiweka kifungo cha maisha kwa kweli ukiweka kifungu cha maisha inaweza ikawa fujo kubwa gerezani lakini hapa mimi nadhani tunaweza kukaweka kifungu kisichopungua miaka mitano na kisichozidi miaka kumi.

Lakini nimalizie cha mwisho kwa ruhusa yako suala la umilikaji wa silaha. Mhe. Naibu Spika, kifungu hiki naomba nimalizie kina mtu yoyote anayetembea na silaha hadharani kinyume cha sheria kwa namna ambayo inasababisha hofu ya mtu atakuwa ni mkosa ana atapewa adhabu ya kifungu kisichozidi miaka miwili na silaha hiyo itachukuliwa na serikali.

Mhe. Naibu Spika, hapa tunacheza na roho zetu Zanzibar hapa kwetu ukiacha vyombo vya ulinzi na usalama wengine wote tuliobakia raia hatuna uwezo wa kumiliki silaha wenzetu Bunge la Jamhuri ya Muungano Wabunge wao sheria yao imewaruhusu kumiliki silaha sisi wengine tumeomba sana Baraza la Wawakilishi tumekataliwa, tunaambiwa silaha sasa sisi wawakilishi wa wananchi tumenyimwa kumiliki silaha leo mtu anakamatwa na silaha afungwe miaka miwili kwa kweli hii haiwezekani.

Mhe. Naibu Spika, mtu yeyote na hapa nitakuja ng'ang'ana kweli kweli Mhe. Waziri hapa mtu anakamatwa na silaha afungwe kifungu cha miaka kumi si chini ya miaka kumi na si zaidi ya miaka ishirini, kwasababu silaha ndio uhai wa nchi yetu haya mambo sijui nini katukana kafanya fujo yote mchezo, lakini unapokamata silaha mtu Mhe. Naibu Spika, silaha moja inaweze ikayayusha umati kwa dakika moja.

Kwahiyo, baada ya hayo Mhe. Naibu Spika haya mengine yaliobakia nitajaribu kuyaandika haraka haraka kwa maandishi, lakini kwakweli naunga mkono mswada huu na Mhe. Naibu Spika nasema huu ndio mswada ambao utalinda Mapinduzi ya Zanzibar. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Hamza Hassan Juma mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mhe. Bi Panya Ali Abdalla.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika awali ya yote nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia uhai tukaweze kukutana mahala hapa jioni hii, lakini pia nichukuwe fursa hii ambayo ya kuweza kuchangia machache katika mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nichukuwe fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote *DPP*, Mwanasheria Mkuu ambao wote wamechangia kwa asilimia kubwa mswada huu kuweza kuletwa mbele ya Baraza lako hili tukufu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niseme mswada huu kwakweli umekwenda mbali sana yaani, ni sheria moja kubwa na kali sana. Kwahiyo, naomba nichukuwe fursa hii kuishajihisha jamii yetu kuiomba kuinasihi jamiii yetu kwamba sheria hii iliyo mbele yetu, inatutaka sote tuwe waangalifu sana kuhusu sheria hii kwasababu inakwenda mpaka katika dhana, ukidhamiria tu jambo basi unaingia katika hatia, kwahiyo ni sheria moja ambayo inatutaka sana inatujenga katika imani na hii ni imani ambayo adimu dini sote zinashajihisha waumini wake kutenda mambo mema kwasababu ndio tulioshushiwa katika vitabu vyetu. *(Makofi)*

Kwahiyo, hii sheria mimi nasema imejikita sana katika kuona sasa waumini ndani ya dini zao zote, basi wanaheshimu sana sheria kwasababu sheria zetu za kidini zimekataza kulidhamiria tu hilo jambo ovu licha kulitenda, kwa hiyo sasa na hao wamejikita kuona katika mtu ambao tayari dhana yake inampelekea kutaka kufanya uovu basi wameanza kuweka adhabu ili sisi tuanze kujishurutisha kutii sheria.

Mhe. Naibu Spika, niwashukuru na niwapongeza sana na kabla sijaendelea niseme naunga mkono kwa asilimia mia sheria hii, ili iweze kupita na sisi tuwe tayari katika kutii sheria ili tuepukane na haya makosa, tukijiepusha na makosa maana sheria hii inaweze isimkumbe mtu yoyote kwa hiyo tukijitahidi na naomba sana sana tuendelee katika jitihada hiyo.

Lakini pia sheria hii ni sheria ambayo inatugusa jamii. Kwahiyo, naomba sana ndani ya kuwa tunaipitisha sheria hii na ni sheria

inayogusa maisha ya kila wakati maana siyo kitu siku, kila wakati mwanadamu yumo katika makosa, basi naomba elimu itolewe kwa wingi sana, ili iweze kutuzindua kila mara sisi tunapoisikia ile elimu inatolewa kuhusu sheria hii iweze kutuweka katika marekebisho ya kuwa tunaepukana na hayo makosa.

Mhe. Naibu Spika, niingie katika mswada huu niende katika kifung cha 136 ambacho kimeelezea maswali mazima ya vitendo ya usagaji. Mhe. Naibu Spika, kuna wenzangu wamevielezea hapa na mimi napenda nichukuwe fursa hii kungana nao mkono kwa kuyapinga na kuyakemea sana masuala haya kwasababu ni masuala ambayo Mwenyezi Mungu ameyataja kwa ukali sana kutukemea waja wake tusifanaye mambo ambayo yako kinyume na maumbile ambayo ametuwekea Mwenyezi Mungu. Kutokana na hali hiyo, naungana na wenzangu ambao walinyanyuka kwa kulipinga suala hilo mimi nasema bado vitendo ambavyo viko maana kuna vitendo vibaya na vibaya zaidi hivi ni vibaya zaidi. Kwahiyo, vitendo vinavyokuwa vibaya zaidi na adhabu yake izidi zaidi hivyo hivyo, ili iweze kutuweka sisi katika mfumo mzuri wa kuachana kabisa na masuala haya. *(Makofi)*

Kwahiyo, Mhe. Naibu Spika, nataka nikazie hili kwamba vitendo hivi vya usagaji kwa wanawake vinatudhalilisha wanawake na hatuvipendi hata kuvisikia na tunakemea na tunasema kwamba Mwenyezi Mungu anasema kitu kama hukipendi kemea na kama hufanikiwi katika kukemea kichukie, tunavichukua vitenda hivi ambavyo vinafanywa na wenzetu. Mhe. Naibu Spika, tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie atuongeze katika nchi yake ya haki, ili tuweze kwenda vizuri tuachana na mambo haya ilitukapate ridhaa ya Mwenyezi Mungu mwisho wa siku yetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ndani ya vitendo hivyo pia kuna vitendo ambavyo vinaelezea ndoa za jinsia moja. Mhe. Naibu Spika,

vitendo hivi bado nasema pamoja na adhabu zilizoweka lakini naomba adhabu iongekezeke kwa matendo haya, ili iwe ni fundisho ya kutufunza sisi kuachana na masuala haya ambayo yanakatazwa sana na dini zetu, adhabu iliyoweka izidi kidogo kwasababu ya kuwa matendo haya Mwenyezi Mungu ameyakataza, kwahiyo na sisi tuweke adhabu iliyokali Mwenyezi Mungu aweka adhabu siku ya malipo, lakini watu waliofanya vitendo vya *Kaumu Lutti* walianza kuadhibiwa hapa duniani na ilifudikizwa nchi ile sasa lazima tuone ukali wa Mwenyezi Mungu juu ya masuala haya. *(Makofi)*

Sasa, Mwenyezi Mungu leo anatuadhibu tuko hapa duniani na hatujajua adhabu yake kubwa ambayo ameiweka huko Akhera. Kwahiyo, Mwenyezi Mungu atulinde na awalinde watoto wetu katika kufanya vitendo hivi viovu na sisi Mwenyezi Mungu atuongoze kwenye kheri, ili tuachane kabisa na masuala haya. (*Amin*)

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mswada huu nitaka pia nieleze kuhusu taarifa za uwongo ambazo zinaweza kuchapishwa katika ni taarifa za uwongo nieseme mfano kama kuna gazeti labda limeshapisha taarifa za uwongo ambalo hapa katika nchi yetu pengine liko Tanzania Bara ambapo kule kuna sheria nyengine ya muungano. Kwahiyo, nataka kujua taarifa kama hizi sisi pengine tunaweza tukajikaza hapa tukasema labda tulifungie gazeti hili kwasababu sisi limeshatusemea mambo haya ya uwongo, lakini vipi ataweze kuadhibiwa mtu yule ambaye sisi tayari ameshachafua jina letu katika nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri atakapokuja aweze kutupa ufafanuzi kuhusu suala hili ili na sisi tuone haki inatendeka katika yake ambayo yako nje yetu.

Mhe. Naibu Spika, nikienda katika mswada huu kifungu cha 53 ambacho kinaonesha kuchukua mali, kifungu kinasema kwa

mujibu wa masharti ya kifungu cha 52 nembo, mabango, silaha, vitabu, karatasi, nyaraka na mali nyengineyo ya jumuiya ikiwa halali itataifishwa na serikali.

Mhe. Naibu Spika, nilitaka kujua kuna jumuiya nyengine tunazo hapa zinafanya mambo yake hapa, lakini pengine vina vifaa ndani ya nchi lakini vifaa vyake vyengine viko nje ya nchi nitaka kujua hapa taasisi hiyo utaifishaji wake kwa mali zile ambazo ziko nje ya nje yetu itakuwaje.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nikienda kifungu cha 57 kinaeleza kutoa tangazo kwa wafanya fujo waliotawanyika sioni vizuri hapa. Mhe. Naibu Spika, kifungu hiki kinasema afisa yeyote wa polisi wa ngazi ya juu au afisa yoyote wa ngazi ya juu au afisa yoyote wa ngazi ya juu wa Jeshi la Ulinzi ndani ya Zanzibar atakayeona watu kumi na mbili au zaidi wamekusanyika kwa ajili ya fujo au ana wasiwasi kuwa fujo linataka kufanywa na watu kumi na mbili au zaidi anaowaona anaweza kutowa au kuwezesha kutolewa tangazo kwa jina la Rais wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, hapa ndio nataka kujua labda niseme tangazo kwa jina la Rais hebu hili tungelifanunulia kwasababu Rais ni mtu mwenye mambo mengi, kwahiyo hili tangazo lingetolew ufafanuzi, ili tukaweza kujua mtu asiweze akachukua fursa ambayo ikio nje ya uwezo wake.

Mhe. Naibu Spika, nikienda katika kifungu cha 64 (1) kinacholeza mtu yoyote anaetembea na silaha hadharani kinyume na sheria kwa namna ambayo inasababisha hofu kwa mtu anakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozi miaka miwili na silaha hiyo itachukuliwa na serikali.

Mhe. Naibu Spika, huyu mtu ambaye ilielezwa hapa yeye silaha tayari anayo hadharani lakini kuna watu wanazo silaha kwa siri

jee, mtu huyo ambaye atagundulikana anayo silaha ile ameimiliki kisiri yeye tunamchukulia vipi au sheria itamchukulia vipi. Lakini nataka kujua hii sheria ambayo tunayo sisi inayo umiliki inaturuhusu sisi kumuliki silaha, lakini kama haituruhusu kumiliki silaha maana yake ndio nataka niende katika kifungu cha 69 ambacho kinasema kutishia kwa kutumia nguvu ambayo hapo nayo inataka kutumika hiyo silaha ya mto.

Mhe. Naibu Spika, kifungu kinasema mtu yeyote ambaye kwa nia ya kumuogepesha au kumkasirisha mtu atanatisha kuvunja au kuharibu nyumba ya kuishi au kwa nia ya kumshitua mtu katika nyumba ya makaazi anatoa silaha ya moto yenye risasi au anafanya kitendo chengine chochote cha uvunjishi wa amani atakuwa..

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Panya Ali Abdalla, zimebakia dakika mbili.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Naibu Spika, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo ya kipindi kisichozidi mwaka mmoja. Mhe. Mwenyekiti napata wasiwasi kwamba mtu huyu ametumia ametaka kutishia kwa kutumia silaha ya moto ambayo ina risasi lakini adhabu inayoonekana hapa ni ndogo na kukutwa na silaha tu hilo ni kosa moja tena la jinai lakini je nakutaka kumtishia mwenzake kwa ajili ya kutumia hii silaha ya moto.

Mhe. Naibu Spika, kifungu hiki adhabu ni ndogo naomba napendekeza adhabu hii izingatiwe iongezwe kwasababu pana makosa mawili hapa kwa wakati mmoja.

Mhe. Naibu Spika baada ya kusema haya machache naomba niungane na wenzangu katika kuunga mkono kwa asilimia mia moja ya sheria hii tuweze kuipitisha lakini na tunakuomba

Mwenyezi Mungu sheria hii atujaalie tuwe watiifu ili tusije tukakumbana na vikwazo hivi ambavyo viko. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Bi Panya Ali Abdalla. Waheshimiwa Wajumbe, bado nina wachangiaji watano ambao natarajia yeyote ambaye atakauwepo hapa atawapa nafasi ya kuweza kuchangia. Wachangiaji wenyewe mchangiaji mmoja ambaye atakuwa mmoja katika wajumbe wa kawaida ambaye atakuwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub, halafu kutakuwa na wachangiaji wengine ambaye ni Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Said Soud Said) na atafuata Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya) na baadaye atafuata Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, na kabla ya Mhe. Waziri kuja kufanya majumuisho atachangia Mhe. Waziri Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na baada ya hapo atakuja Mhe. Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, mnatakiwa mniletee hapa na nyie kwamba mtachangia ndio utaratibu si ndio haya sawa kwa hiyo ni hao kwa ufupi ni hao.

Waheshimiwa Wajumbe, niwashukuru sana kwa michango yetu pamoja na utulivu wenu sasa naakhirisha kikao hadi Jumatatu saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:42 usiku kikao kiliakhirishwa hadi tarehe 12/02/2018 saa 3:00 asubuhi)